**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 12 Aprili, 2007**

**D U A**

*Spika (Mh. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Controller and Auditor General's Report on the Financial Statements of Local Government Authorities for the Year ended 30th June, 2006).*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA (MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA):**

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa Mwaka Ulioishia tarehe 30 Juni, 2006 *(The Annual Report and Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the Year ended 30th June, 2006)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa Fedha Ulioishia 30 Juni, 2006 *(The Controller and Auditor General's Report on the Financial Statements of the Central Government for the Year ended 30th June, 2006)*.

Hati ya Matumizi ya Ziada kwa Mwaka 2003/2004 *(The Statement of Excess for the Year 2003/2004).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 26

**Uhaba wa Majengo – Hospitali za Mikoa na Wilaya**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliliza:-

Kwa kuwa hospitali nyingi za Mikoa na Wilaya zikiwemo hospitali za Mkoa wa Singida zinakabiliwa na uhaba wa majengo hasa wodi za akina mama na watoto; na kwa kuwa hospitali hizo zimekuwa na maeneo madogo na mazingira magumu ya miundombinu:-

(a) Je, ni lini Serikali itakuwa na ramani ya kitaifa ya ujenzi wa ghorofa?

(b) Kwa kuwa hospitali ya Mkoa sasa inakabiliwa na tatizo la nyumba za Madaktari zilizo karibu na hospitali kwa ajili ya huduma za haraka. Je, Serikali inasema nini juu ya tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya hospitali za Mkoa na Wilaya nchini zinakabiliwa na uhaba wa majengo. Aidha, hospitali nyingi zimejengwa zamani na hivi sasa tunafahamu kuwa idadi ya watu mijini imeongezeka mara dufu. Pia nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna matatizo ya majengo ya wodi za akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na msongamano katika hospitali ya Mkoa wa Singida, Serikali iliongeza wodi mpya ya kisasa ya wazazi yenye *theater* ndogo na ina uwezo wa vitanda 18 kwa gharama ya shilingi milioni 155 na kukamilika mwaka 2005/2006. Majengo mbali mbali yamefanyiwa ukarabati kuanzia mwaka 2002 – 2006/2007 kwa jumla ya gharama ya shilingi 324,699,290/=. Majengo yaliyokarabatiwa ni pamoja na jengo la Utawala, wodi ya wagonjwa wa kifua kikuu na ukoma na jengo la *MCH* Kliniki. Aidha ili kupunguza msongamano katika hospitali ya Mkoa, Kituo cha Afya cha Sokoine kimepanuliwa kwa kuongeza wodi moja ya wagonjwa wa kawaida *(Clinical Ward)* katika mwaka wa Fedha wa 2006/2007 kwa shilingi 110,000,000/= na tayari shilingi 100,000,000/= zimeishatolewa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa ujenzi wa hospitali za Mikoa ana Wilaya, Serikali haina sera ya kujenga hospitali za Mikoa na Wilaya kutumia ramani ya ghorofa. Mkoa na Wilaya inapoona kuwa inahitaji na ina uwezo wa kujenga hospitali mpya ya Mkoa au Wilaya, kinachotakiwa ni kutafuta eneo linalotosheleza majengo yanayotakiwa. Jukumu la Wizara ya Afya ni kutoa miongozo mbali mbali kuhusiana na *specifications.*

Aidha katika miongozo iliyopo, hakuna suala la ramani ya majengo ya aina gani itumike. Hata hivyo, Serikali hivi sasa inaboresha miongozo hiyo kwa kutumia Mshauri Mwelekezi na taarifa hiyo itawasilishwa Serikalini mwezi Mei, 2007. Katika uboreshaji huo, suala la majengo ya ghorofa litafikiriwa. Hata hivyo, iko Mikoa kama Arusha ambayo iliamua kujenga hospitali ya ghorofa kutokana na kutokuwa na eneo kubwa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Serikali iliamua kukopesha baadhi ya nyumba zake kwa watumishi waliokuwa wanaishi humo. Hivyo, Madaktari tisa wa hospitali ya Mkoa wa Singida nao kama watumishi wa Serikali wakaipata bahati ya kukopeshwa nyumba tisa walizokuwa wanaishi. Hata hivyo, ili kuhakikisha kuwa Daktari anayepangiwa Mkoa wa Singida anapata nyumba ya kuishi, Mkoa unatafuta nyumba za watu binafsi za kukodisha na kuwapangia. Kwa sasa iko nyumba ambayo ni *rest house* ya kuwaweka watumishi kwa muda wakisubiri nyumba za kuishi. Hata hivyo Serikali inaendelea na sera yake ya kujenga nyumba za watumishi kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pmaoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na kujenga wodi ya akina mama yenye *theater* ndani yake, lakini bado tatizo ni kubwa sana la wodi ya akina mama kwani mpaka sasa hivi akina mama wanalala wawili wawili na watoto wanalala wanne wanne. Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka ukilinganisha sasa hivi kuna magonjwa ya kuambukiza ya kusaidia hospitali ya Mkoa wa Singida ili tatizo la kulala wagonjwa wawili wawili au watoto wanne wanne liishe?

(b) Kwa kuwa Madaktari waliouziwa nyumba walikuwa siyo Madaktari wa kudumu katika hospitali ya Mkoa wa Singida, wengine wamestaafu na wengine wamehama; na kwa kuwa nyumba hizo zilikuwa eneo la hospitali ya Mkoa wa Singida, suala ambalo lilikuwa linasaidia Madaktari kuokoa maisha ya wagonjwa hata kwa kwenda kwa miguu panapokosekana miundombinu ya usafiri; na kwa kuwa sasa hivi ni tatizo kubwa la nyumba za Madaktari mpaka Madaktari wengine wanakataa kwenda Mkoa wa Singida kwa mfano juzi Daktari Bingwa amekaa kuja Singida.

Je, Serikali ina mkakati gani wa makini utakaowatia moyo Madaktari watakaopangiwa Singida ili waweze kwenda wawe na matumaini kwamba watakapata nyumba? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba mkakati wa Serikali ni kupanua huduma za afya. Kwa sasa Serikali ina programu maalum ya ukarabati wa Vituo vya afya, zahanati ili kupunguza msongamano katika hospitali za Mikoa.

Sasa hivi pia Serikali ina mkakati wa ukarabati wa hospitali za Mikoa na hospitali za Wilaya. Kwa mwaka huu katika bajeti hii ambayo tutapitisha Mungu akijalia, hospitali mbali mbali za Mikoa zitakarabatiwa moja wapo ambayo itapewa kipaumbele ni hospitali ya Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza humu Bungeni, Ofisi ya Rais ilikuwa imeteua Kamati ya kufanya mapitio ya zoezi zima la uuzaji wa nyumba za Serikali kwa nchi nzima na lengo lilikuwa ni kuona pale ambapo zoezi hilo halikutekelezwa kwa misingi iliyowekwa. Lengo ni kusahihisha makosa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na nyumba za Madaktari katika hospitali Mkoa wa Singida, hii itakuwa ni sehemu ya zoezi hilo tuone kama kweli nyumba ambazo Madaktari hao waliuziwa zilizingatia taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na baada ya kufanya hivyo, tutasahihisha na taarifa itatolewa kwa wahusika. Nashukuru sana! *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, nilikuona. Swali la nyongeza!

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, swali nililotaka kuliuliza, tayari Mheshimiwa Waziri kalijibu. Ahsante!

Na. 27

**Soko la Dengu na Alizeti**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha dengu na alizeti kimeshamiri sana katika Tarafa ya Itigi; na kwa kuwa wananchi wamepania kulima kwa wingi mazao hayo ya biashara:-

Je, Serikali imejiandaa vipi kuwatafutia soko la uhakika na lenye bei nzuri ili wakulima hao wasihangaike kwa kutegemea zaidi walanguzi?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John P. Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mazao ya dengu na alizeti pamoja na mengine ya aina yake kama vile karanga, nyonyo, kunde n.k. hulimwa sana katika maeneo mengi ya Mikoa ya Kanda ya Kati ikiwemo Tarafa ya Itigi Wilayani Manyoni, Mkoa wa Singida. Mazao hayo yanayotegemewa sana kibiashara na wakulima wengi wa maeneo hayo hujumuishwa kwenye kundi moja lijulikanalo kama Mazao mchanganyiko *(Mixed Crops)*.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanzishwa mfumo wa soko huru nchini, soko la mazao mchanganyiko lilisimamiwa na Shirika la Serikali lililojulikana kama *GAPEX* ambalo lilikuwa mnunuzi pekee wa mazao hayo. Shirika hilo la *GAPEX* lilifungwa na Serikali baada ya kufilisika kibiashara.

Mheshimiwa Spika, baada ya hatua hiyo ya Serikali, biashara ya mazao ya kilimo yakiwemo yale ya kundi la mazao mchanganyiko liliachwa kujiendesha Lenyewe kwa msingi wa ushindani wa soko ambapo wanunuzi binafsi waliruhusiwa kununua mazao toka kwa wakulima chini ya utaratibu wa soko huria.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia upatikanaji wa masoko ya uhakika na bei nzuri kwa mazao mchanganyiko ya wakulima yakiwemo dengu na alizeti toka Tarafa ya Itigi, Serikali itafanya yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha wakulima wadogo wadogo kujiunga katika vyama vya ushirika au vikundi vya uzalishaji ili kuwa na nguvu ya pamoja kibiashara *(Collective Bargaining)* pamoja na kuwavutia wengi kutokana na urahisi wa mazao mengi katika eneo moja.

(b) Kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kuandaa mazingira ya ushindani katika ununuzi wa mazao kwa kuhakikisha kuwa ununuzi na uuzaji wa mazao unafanyika katika magulio na masoko yaliyotengwa kwa ajili hiyo na kusimamia magulio hayo yanatumika ipasavyo.

(c) Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzuia mtindo mbaya wa ununuzi holela wa mazao ya wakulima ambapo baadhi ya wanunuzi huwafuata wakulima mmoja mmoja, mtindo unaotoa mwanya kwa wakulima kulanguliwa.

(d) Kuhamasisha na kuweka mazingira mazuri ya usindikaji wa mazao ya mbegu za mafuta ikiwamo alizeti na hivyo kuwapatia wakulima soko la uhakika. Lakini pia Serikali imeweka ushuru katika uingizaji wa mafuta ya kupikia yasiyosafishwa ili kuhamasisha usindikaji wa mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini.

(e) Kutoa taarifa za masoko ya mazao kwa lengo la kuwawezesha wakulima na wadau wengine kuelewa mwenendo wa bei za mazao ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, Serikali imepitisha mkakati wa kuimarisha juhudi za kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje *(Export Development Strategy)*. Mkakati huo ni hatua ya kuiwezesha Tanzania kutatua matatizo ya uzalishaji na kukuza mauzo nje yakiwemo mazao asilia na yasiyo ya kilimo kama alizeti na dengu.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza: Kwa kuwa ushauri unaotolewa kuhusu bei ya mazao mchanganyiko hautofautiani sana na mazao mengine kama vile korosho na mazao mengine makuu; na kwa kuwa tumejionea jinsi ulivyokuwa na matatizo kwenye mazao kama hayo hayo ya korosho ambapo wengi wa wakulima walibaki nayo majumbani bila kuyauza kwa sababu ya utata wa bei. Je, Serikali ina mfumo upi hasa mbali ya huu wa soko huria na huu wa ushirika ili tuweze kujikwamua katika tatizo hili la bei?

Mheshimiwa Spika, katika kilimo suala la miundombinu ni suala mtambuka. Tumelima sana kwa kweli zao la alizeti na dengu na mazao mengine. Lakini, kutokana na mvua zilizonyesha msimu huu, miundombinu yetu, barabara zetu ziliharibika kiasi kwamba wakulima wana mashaka jinsi gani wanaweza kuyafikisha mazao haya katika masoko ambayo yanaweza kuwapatia bei nzuri. Kwa hivyo, ningependa kujua Serikali inatamka nini kuhusu maeneo haya ambayo kwa kweli wakulima wana mashaka watajikwamuaje? Mheshimiwa Spika, Ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza juu ya mfumo wa soko unaotumika kwamba pengine ungeangaliwa mfumo mbadala. Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeeleza tu kwamba mfumo tuliokuwa nao pale awali ambapo Serikali ilikuwa inajihusisha na biashara na kusimamia uchumi moja kwa moja, ndio huo ambao ilikuwa inatumia mashirika yake ambayo yalikuwa yananunua mazao na kusimamia bishara ya mazao kwa ujumla.

Sasa, chini ya mfumo huu wa uchumi wa soko, utaratibu wa soko huria unaruhusu ushindani ambapo kinachotakiwa ni kusimamia tu zile njia bora kuweza kuwafikisha wakulima kwenye soko waweze wakauza mazao yao. Na njia ya ushirika tunadhania kwamba ndio njia muafaka zaidi kwa sababu inawapa wananchi nguvu ya pamoja kwanza, kutafuta masoko, lakini vile vile kuwa na ile *collective bargain* ili kuweza kufanya ushindani ambao ni mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nadhani sasa hivi njia muafaka zaidi ni kuwahamasisha wakulima wetu waweze kuanzisha vyama vya ushirika ambavyo vitawapa nguvu zaidi ya kutafuta na kuweza kusimamia bei kwa nguvu yao ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili juu ya miundombinu, hili ni suala ambalo liko katika nchi nzima na si katika Mkoa wa Singida na Tarafa ya Itigi peke yake na kama ambavyo Serikali imekuwa ikisema hapa mara kwa mara na sisi wote tunavyoshuhudia kwamba ziko jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu hapa nchini ili kuhakikisha

kwamba wakulima wanafikisha mazao yao sokoni pamoja na huduma zingine ambazo zinahitaji usafiri. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge, naomba tu awe na subira katika jitihada hizi za Serikali zinazoendelea kufanyika hivi sasa.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuongezea jibu zuri sana la Mheshimiwa Waziri kwa swali la Mheshimiwa Lwanji kama ifuatavyo kwamba katika aya ya mwisho ya jibu letu, tulisema kwamba Serikali sasa iko mbioni kutekeleza mpango unaitwa *Export Development Strategy*. Mpango huu una mambo mawili:-

Kwanza, ni kuongeza uzaklishaji wa mazao ili kusudi yawe mengi na tuweze kuyauza katika masoko ya dunia. La pili ni kuanzisha mfuko maalum utakaoondoa kitu katika taaluma wanaita *supply side constrains* yaani matatizo yanayotokana na uzalishaji na usafirishaji wa mazao hadi kwenye masoko. Katika hayo, ziko barabara za vijijini ambazo zitaunganisha wazalishaji ndani ya vijiji na barabara kuu za kwenda kwenye maasoko makuu ya Wilaya, ya Mkoa nay a Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba chini ya utaratibu huo ambao utekelezaji unaanza mara moja, kutakuweko kipengele cha kutafuta fedha za wafadhili kwa ajili ya kutengeneza barabara za vijijini ili ziweze kupitika wakati wote ili mazao yaweze kwenda kwenye masoko.

**SPIKA:** Nimemwona Mheshimiwa, Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mbunge wa Kwela! Swali la nyongeza!

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, hasa kutokana na majibu ya sasa ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, anaweza akatuthibitishia malengo hayo yatafikiwaje wakati hakuna mipango inayowahusisha wakulima wenyewe na Mikoa katika kulima mazao haya ya mbegu?

**MHE. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, mipango ya kulima mazao hayo yaliyotajwa katika swali hili ipo! Tunachohimiza ni kwamba kila Wilaya iwe na mpango unaitwa *District Agricultural development Plan (DADEP)* ambapo kila Wilaya inapanga namna ya mazao ambayo yanastahili kulimwa katika maeneo yao na mipango hii ikioanishwa na mipango ya masoko, inakamilisha mzunguko wa uzalishaji ambao ni kuzalisha kwa wingi, kuuza kwa masoko ya ndani na kuwezesha *export drive.* Kwa hiyo mipango ipo na inaendelea kusimamiwa, lakini inaanza katika ngazi ya Wilaya kwa sababu kilimo kinafanyika Wilayani na kijijini. *(Makofi)*

Na. 28

**Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mbeya**

**MHE. BENSON M. MPESYA** aliliza:-

Kwa kuwa kuwepo kwa hospitali ya Mkoa Mbeya kumesaidia sana kuboreha huduma za matibabu ndani ya Jiji hilo hali iliyopunguza msongamano wa wagonjwa hospitali ya Rufaa ya Mbeya:-

Je,. Ni lini Serikali itajenga wodi za kulaza wagonjwa katika hospitali ya Mkoa ya Mbeya ili kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitali ya Rufaa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mbunge wa Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuungana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kuwepo kwa hospitali ya Mkoa Mbeya kumesaidia kuboresha huduma za matibabu katika Jiji la Mbeya na hivyo kupunguza msongamano wa wagonjwa usio wa lazima katika hospitali ya Rufaa ya Mbeya, hususan wagonjwa wasiohitaji huduma ya Madaktari bingwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hospitali ya Mkoa wa Mbeya bado iko katika hatua za ujenzi na hivyo bado haijakamilika. Mpaka sasa hospitali hiyo ina majengo ya huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)*na maabara ambayo yamekamilika na yanatumika kutoa huduma za matibabu.

Mheshimiwa Spika, ili hospitali hiyo ianze kutoa huduma ya kulaza wagonjwa katika mwaka wa fedha 2007/2008, TAMISEMI kupitia Ofisi ya Katibu Tawala Mbeya imetenga kiasi cha shilingi milioni 470 kwenye bajeti ya maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya kulaza wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi huo ili kuhakikisha kuwa wodi za kulaza wagonjwa kwenye hospitali hiyo zinajengwa kulingana na viwango vinavyokubalika. Aidha, baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, Wizara yangu itasaidia upatikanaji wa vifaa-tiba na watumishi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa utekelezaji wa mradi huu utasaidia kuboresha utoaji wa huduma za afya katika hospitali hiyo na hivyo kuondoa kabisa tatizo la msongamano katika hospitali ya Rufaa ya Mbeya.

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya kutoka kwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Spika, kwa sababu tatizo la hospitali ya Mkoa wa Mbeya linatokana na maamuzi ambayo mimi naweza kuita mabaya ya kuvunja hospitali ya Mkoa iliyokuwepo kwa ajili ya kuipisha hospitali ya rufaa kitendo ambacho kimesababisha wananchi wa Mbeya takriban 400,000 kushindwa kupata huduma zinazostahili. Kwa kiwango hiki, kwanza nishukuru kwa hiki ambacho kimetengwa.

Je, Serikali haioni kwamba inatakiwa isukume zaidi badala ya kuiachia TAMISEMI kupitia Mkoa kwa sababu hospitali hii ilivunjwa na Serikali?

Mheshimiwa Spika, la pili: Kwa kuwa ili hospitali ya Mkoa ifanye kazi kwa karibu zaidi na kwa ubora zaidi na kwa ufanisi, hospitali ya Wilaya inahitajika na Mbeya kama Jiji halina hospitali ya Wilaya. Halmashauri ya Jiji la Mbeya imeamua sasa kujitahidi kugeuza kituo cha afya cha Igawilo kuwa hospitali ya Wilaya.

Je, isingekuwa vema kwa Serikali sasa kuhakikisha juhudi hizi na yenyewe inaziongezea nguvu hasa kwa kuzipatia fedha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba tumevunja hospitali ya Mbeya. Ni kwamba tumepanua hospitali ya Mbeya kuwa hospitali ya Rufaa.

Mheshimiwa Spika, mimi ningefikiria kwamba kule kuipanua hospitali na kuifanya ya rufaa ni kwamba watu wa Mbeya wamenufaika zaidi kwa sababu huduma zimekuwa ni za kitaalam zaidi na za kitaaluma kuliko hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nafikiri Mheshimiwa Mbunge, mimi naomba tu tukubaliane kwamba kwa sababu Serikali inatenga pesa na kwa sababu hospitali ya Mkoa inatengenezwa, basi tushukuru kwamba sasa kule Mbeya tutakuwa na hospitali ya Rufaa na vile vile tutakuwa na hospitali ya Mkoa.

Kwa hiyo, wananchi wetu wa Mbeya watapata huduma bora zaidi na wale ambao wanauzunguka ule Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa hospitali ya Wilaya kwamba Mbeya hakuna hospitali ya Wilaya na kwamba wamepandisha Kituo cha Afya cha Mbeya kiwe hospitali ya Wilaya. Mheshimiwa Spika, katika sera za afya kwanza huwa hatupendezewi kubadilisha Kituo cha Afya ibadilike kuwa hospitali au zahanati kwenda kituo cha afya.

Tunachoshauri ni kwamba iweze kujengwa hospitali kama wenyewe Halmashauri au Jiji kama litaamua. Ninachoweza kutoa ushauri ni kwamba fedha zinazotoka kujengea hospitali zikiwa zinapitia TAMISEMI kwenda Mkoa wa Mbeya ni Serikali ile ile ndiyo inayotoa zile fedha ni katika tu kule kupitia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge akiona kwamba ile fedha imekwenda kupitia kwa *RAS* ajue ni kwamba inatoka Serikalini vile vile. Lakini hata hivyo nashauri kwamba Jiji bado halikatazwi kujenga hospitali yao na kupanga katika mipango yao ya Bajeti.

**MHE. MUSSA AZAN ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuboresha huduma za afya nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye kikao chako cha Bajeti ya mwaka jana kilio cha Mkoa wa Dar es Salaam ni kuwa hospitali hizi tatu za Kinondoni, Ilala na Temeke, huduma za *X-Ray* ni za kiwango cha chini sana kutokana na uwingi wa wagonjwa

wanaohudumiwa kwenye hospitali hizi. *X-Ray* hizi zimepitwa na wakati na *speed* yake ni ndogo. Mimi siulizi Serikali ina mikakati gani, bali naiomba Serikali kwenye Bajeti ya mwaka huu na mwaka ujao, wazifikirie hospitali hizi tatu ili tupate huduma za *X- Ray* mpya ili wananchi wapatiwe huduma ya kuridhisha na safi. (*Makofi*)

Je, Serikali itakubali ombi langu? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu ombi hilo.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zungu kama ifuatavyo; ni kweli nakubali. (*Makofi*)

Na. 29

**Madhara Yatokanayo na Dawa za *ARVs* kwa Watumiaji**

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inatilia mkazo matumizi ya dawa za kurefusha maisha na kupunguza makali ya maumivu na masumbuko kwa watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi *ARVs* na kwa kuwa kati ya dawa hizo imo dawa inayojulikana kwa jina la *EMTRI (TM) – 40* kutoka India ambayo inakubalika na *MSD*, ambayo vile vile inalalamikiwa na baadhi ya watumiaji kuwa, badala ya kumwongezea muda wa kuishi, dawa hiyo imekuwa ikiwapunguzia maisha kutokana na athari zake kwa afya ya mtumiaji:-

(a) Je, Serikali inayo habari juu ya tatizo hilo na malalamiko yanayotolewa na baadhi ya watumiaji wa dawa hizo?

(b) Kama Serikali inaelewa, au haielewi. Je, iko tayari kulifanyia ufumbuzi haraka?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mbunge wa Muyuni, napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianza kutoa huduma ya dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa Ukimwi, tangu mwezi Oktoba 2004. Dawa hizi hununuliwa kutoka makampuni mbalimbali ya Dawa ambayo dawa zake zimethibitishwa ubora wake na kusajiliwa na mamlaka ya chakula na dawa Tanzania.

*EMTRI 40* ni moja ya dawa ambazo zimethibitishwa na mamlaka ya chakula na dawa na zilinunuliwa na Serikali kwa ajili ya huduma ya kupunguza makali ya Ukimwi

kwa wananchi wenye virusi vya Ukimwi waliofikia kiwango cha kupewa dawa hizi. Dawa hii ina mchanganyiko wa dawa *stavudine, Lamuvudine* na *Nevirapine.*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako tukufu, naomba ifahamike kwamba dawa za kupunguza masuala ya Ukimwi kama dawa nyingine zozote zina faida kwa wagonjwa wanaozitumia dawa hizo kwani hupunguza kuzaliana kwa virusi vya ukimwi ndani ya mwili wa mgonjwa.

- Aidha, kama dawa nyingine zozote, dawa hizi zinaweza kuleta madhara kwa baadhi ya wagonjwa, madhara kama vile ngozi kuwasha, mwili kufa ganzi, matatizo kwenye ini, kupungukiwa damu, mwili kuvimba baadhi ya sehemu kama mgongo, matiti na kadhalika.
- Taarifa zote kuhusu matatizo yanayotokana na madhara ya dawa zinazotumiwa na wananchi huwasilishwa Mamlaka ya Chakula na Dawa ili kuratibu madhara haya na kutoa ushauri kwa Serikali na makampuni husika. Uko utaratibu wa mtumiaji kutoa taarifa katika kituo alichopatiwa dawa na kujaziwa fomu maalum au kadi inayoainisha matatizo ambayo kitakwimu hutumwa Mamlaka ya Chakula na Dawa. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kumekuwa na malalamiko kuwa dawa za kupunguza makali ya Ukimwi aina ya *EMTRI 40* zinawaletea matatizo magonjwa wanaozitumia dawa hizo. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tayari imepokea taarifa hii. Kuanzia mwanzoni mwa mwaka 2006, Wizara yangu kupitia taasisi zake za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi na Mamlaka ya Chakula na Dawa ilianza kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhusu malalamiko hayo. Aidha, mpaka sasa mamlaka ya chakula na dawa imewasiliana na kiwanda kinachotengeneza dawa hizi kuhusu athari zinazoripotiwa kujitokeza kwa watumiaji wa dawa hizi *EMTRI 40.*

Mamlaka ya Chakula na Dawa pia imepanga kufanya utafiti kwenye hospitali ambako dawa hizi zimekuwa zikitolewa ili kufuatilia kwa karibu ufanisi wa dawa hizi kwa wagonjwa ambao wamekuwa wanazitumia pamoja na madhara yake kwa magonjwa kutokana na dawa husika. Wizara inawasiliana na nchi jirani kama Kenya na Uganda ambapo pia hutumia dawa hizi za *EMTRI 30&40* kuona kama tatizo hili linajitokeza kule kwani wanaoleta dawa hizi ndiyo wanaouza hata nchi jirani. Hata hivyo, mamlaka ya Chakula na dawa inaendelea kufanya tathmini ya takwimu zinazopokelewa na taarifa rasmi ya tathmini hiyo inatarajiwa kutolewa mwezi Agosti, 2007.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo kama haya yaliwahi kujitokeza kwa mganga fulani kuhusu matibabu ya kisukari. Katika Bunge lililopita lalamiko hilo lilikuja katika Bunge hili na vile vile kulikuwa na malalamiko mengi yanayohusiana na dawa ya *SP* ambao watu wengi waliathirika kutokana na matumizi haya. Je, Serikali katika muda huu haioni kwamba ipo haja ya ulazima kabla ya kuingiza dawa hizi na kuzingatia ipasavyo masuala ya uingizaji wa dawa ambazo hutumia majina ya *generic* kuliko *brand names* ili kuokoa maisha ya watu

wengi na kupunguza malalamiko yanayotokana na matumizi ya madawa? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba matatizo yalijitokeza kwa daktari ambaye amemtaja yeye ambaye pia na mimi namfahamu na suala la dawa kama *SP*.

Lakini nataka kumwambia na kumhakikishia kwamba sera ya taifa tunachokifanya Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii tunaponunua dawa tunatumia *generic names* wala hatutumii *brand names* ndiyo nimesema hapa nilitaja kwamba hizi *empty* ni kuwaelewesha kwamba ina nini lakini katika kununua dawa tunatumia *generic names* na siyo *brand names. (Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dawa hizi tunasema kwamba zinapunguza makali na zinarefusha maisha. Kwa hali hiyo, pia mgonjwa inamsababisha aweze kufanya ngono na kwa kuwa wakati unatumia dawa hizi na kuweza kufanya ngono kwa yule ambaye hana maradhi na kumtia maradhi ina maana dawa yoyote atakayotumia haiwezi kufanikisha.

Je, Serikali, haioni kwamba njia hizi za kutumia dawa pia inachangia maradhi haya? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, dawa hizi wanazopewa wale waathirika wanapewa kupunguza makali na kurefusha maisha ili waweze kuishi maisha salama na sawa kama wananchi wengine. Suala la yeye kufanya tendo la ngono ni haki yake kimsingi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba tufahamu kwamba kumtia maradhi na suala la ngono mimi sioni kama lina uhusiano. Dawa tunazompa nia yake ni kuweza kumrefusha maisha awe anaishi maisha ya kawaida. Suala la kusema kwamba kumpa dawa ni kuhasmasisha suala la ngono mimi sioni kama lina mahusiano kwa sababu maradhi kama atapata, dawa za maradhi mengine ambayo ni nyemelezi ataweza kutibiwa lakini si sababu kwamba dawa hizi tunamfanya ili aweze kufanya mambo mengine ambayo anatakiwa kufanya kimsingi. (*Makofi*)

Na. 30

**Matumizi ya Kadi Tofauti kwa Wagonjwa Waishio na Virusi vya Ukimwi**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa bado sehemu kubwa ya jamii inawanyanyapaa watu waishio na virusi vya UKIMWI:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa matumizi ya kadi za matibabu tofauti kwa wagonjwa wa UKIMWI kama ilivyo sasa ambapo kadi za *blue* hutumika wakati wa matibabu ni aina moja ya unyanyapaa?

(b) Je, Serikali itasitisha lini matumizi ya kadi hizo tofauti zinazotumika kwa watu wa kawaida wakati wa matibabu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga Mbunge Viti Maalum, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Unyanyapaa ni tatizo kubwa katika jamii hususan kwa wagonjwa wa UKIMWI. Chimbuko la unyanyapaa katika jamii linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo zifuatazo:-

(i) Uelewa mdogo wa jamii kuhusu jinsi maambukizi ya virusi vya UKIMWI yanavyotokea na mazingira yote yahusuyo Ukimwi yakiwemo yale ya kijamii na kiimani.

(ii) Ukimwi kuhusishwa na dhambi, laana, mateso haswa kuwepo kwa dhana kuwa ugonjwa wa Ukimwi unaotokana na zinaa ambayo ni kinyume na maadili mazuri ya kidini na kijamii pia.

(iii) Kutokuwepo na tiba ya kuponya ugonjwa wa Ukimwi hivyo kuwafanya watu kuwanyanyapaa wagonjwa wa Ukimwi kwa hisia kuwa hawana muda mrefu wa kuishi.

Mheshimiwa Spika, huduma za afya hapa nchini hutolewa kwa kuzingatia aina na hali ya ugonjwa na hivyo kuna mifumo mbalimbali na tofauti ya kufuatilia magonjwa ambayo kila moja inakuwa na kadi maalum za ufuatiliaji. Aidha, tiba ya ugonjwa wa Ukimwi ni ya maisha kama ilivyo tiba ya magonjwa mengine sugu kama kisukari na shinikizo la damu. Kutokana na usugu wa magonjwa haya, zipo kliniki maalum ambazo huwahudumia wagonjwa husika. Kila kliniki ina mfumo wake wa ufuatiliaji ikiwa na pamoja na kutoa kadi maalum kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba kliniki zinazotoa huduma na tiba ya ugonjwa wa Ukimwi hutoa kadi maalum kwa wagonjwa wa Ukimwi ambazo zina rangi ya *blue*. Serikali ilitoa kadi hizo maalum kwa nia njema ya kuweza kuwafuatilia wagonjwa wake kama inavyofanya kwa wagonjwa wengine bila kujali kama rangi ya kadi hizo inaweza kuleta hisia za unyanyapaa kwa mfano wagonjwa wa kifua kikuu wanapewa kadi za kijani. Kadi hizo zinawawezesha wagonjwa wa Ukimwi kupata huduma kwenye kliniki maalum zilizopo nchini kote bila usumbufu wowote na bila kulazimika kujisajili upya kila wanapokwenda kupata huduma sehemu tofauti na ile ya awali. Hata hivyo, kutokana na unyanyapaa uliopo katika jamii kwa wagonjwa wa Ukimwi na sababu nilizozitaja katika

maelezo yangu ya awali, wagonjwa hao wamekuwa wakinyanyapaliwa hata kabla kadi hizo hazijakuwepo.

(b) Kutokana na ukweli kwamba rangi ya kadi haileti unyanyapaa bali unyanyapaa unatokana na sababu nilizozitaja awali, Serikali bado haijaona sababu ya kusitisha matumizi ya kadi hizo kwa sasa. Hata hivyo, Bunge lako tukufu litakubaliana nami kwamba iwapo jitihada za kuondoa unyanyapaa katika jamii hazitafanikiwa hata kama Serikali itabadilisha rangi ya kadi hizo, pindi wananchi watakapoifahamu rangi hiyo mpya wataendelea kuwanyanyapaa wagonjwa hao.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Mkanga pamoja na Waheshimiwa Wabunge, wenzangu katika Bunge lako Tukufu wataungana na jitihada za Wizara yangu, Serikali pamoja na wadau wengine kupiga vita unyanyapaa ambao ni kikwazo kikubwa cha jitihada za Serikali za kupambana na ugonjwa wa Ukimwi hapa nchini.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekiri rasmi na kutokana na hali halisi kwamba ugonjwa huu wa ukimwi hauna tiba wala dawa. Je, Serikali itachukua hatua gani na inasema nini kwa taasisi za Dini hasa katika jiji la Dar es Salaam, zimekuwa zikitumia vyombo vya habari hasa luninga na kujitangaza kwamba zina uwezo wa kutiba maradhi haya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikizungumza kwamba ugonjwa wa Ukimwi, hauna tiba wala dawa. Tumekuwa tukikemea si tu taasisi za kidini lakini taasisi zote na watu wote ambao wanatoa dawa za asili au za aina nyingine kwamba ni marufuku kutangaza kwamba wanaweza kutibu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kupitia Bunge lako tukufu niwakumbushe wananchi wote na wale wote wanaotoa huduma kwa wagonjwa ambao wameathirika wasitoe matangazo yao ya kusema kwamba ugonjwa huu unaweza kutibika.

Naomba nitoe vile tahadhari na kuwakumbusha ndugu wananchi kwamba ugonjwa wa Ukimwi hauna tiba na kwamba wote kwa pamoja tushirikiane kuweza kujikinga na maambukizo na wale ambao wameshapata maambukizo waendelee kutumia dawa ili kupunguza makali na kuishi zaidi. (*Makofi*)

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, aidha namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Kwa kuwa sisi tunaoshughulika na maeneo haya ya huduma kwa watu walioathirika tunapokea malalamiko kuhusu hizi kadi na kwa kuwa unyanyapaa unaoelezwa hapa unatokana hasa na wale wahudumu wenyewe wa afya wanapoona tu zile kadi wanaanza kuwasemea lugha ambayo labda siyo inayostahili ambayo inaleta ile hisia kwamba kwa kuona tu hawapati ile huduma. Sasa Waziri, amesema kwamba unyanyapaa ni suala la elimu duni. Lakini hao wanaofanya hivi ni watu walioelimika na ni watalaam wa Wizara yetu. Je,

Serikali iko tayari kutoa kali kwa watumishi wake ambao wanatoa hii dalili ya kunyanyapaa kwa watu ambao kwa kweli wanahitaji upendo zaidi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, lugha yoyote kwa watumishi wanaotoa huduma za afya si kwa wagonjwa ambao ni waathirika tu lakini kwa wagonjwa wote wanaokwenda katika vituo vya kutoa huduma wanapaswa kupewa lugha na maelekezo bila kujali kwamba anaumwa nini. Kama wapo watumishi wanaoendelea kutoa hizi kauli, napenda kusema kwamba Serikali haitasita kuwachukulia hatua kali sana ikiwa ni pamoja na kuwafukuza kazi. (*Makofi*)

Na. 31

**Upimaji wa Vijiji vya Wilaya ya Bukombe**

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali, katika Kikao cha Nne cha Bunge la Bajeti la mwaka 2006/2007 ilipitisha mpango kabambe wa kupima vijiji 3,104 Tanzania, vikiwemo vijiji vya Wilaya ya Bukombe.

Je, Serikali itaanza lini kupima Vijiji vya Wilaya ya Bukombe, ili kuwawezesha wananchi kupata hati miliki zitakazowasaidia katika suala zima la kujipatia mikopo kutoka kwenye mabenki na taasisi mbalimbali za fedha kwa lengo la kuboresha maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Luhahula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na Maendeleo ya Makazi iliweka lengo la kupima vijiji 3,104 katika mwaka wa fedha 2006/2007. Katika hotuba yangu niliorodhesha idadi ya vijiji vitakavyopimwa katika kila Mkoa. Kwa Mkoa wa Shinyanga ni vijiji 150 vinavyokusudiwa kupimwa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika Bajeti yangu 2006/2007 Wizara yangu iliahidi kupima vijiji 3,104 katika nchi nzima. Aidha, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, itapima mipaka ya vijiji katika Wilaya ya Bukombe, katika mwaka huu wa fedha. Upimaji wa mipaka ya vijiji 112 vya Wilaya ya Bukombe, itaanza mara baada ya kukamilisha upimaji wa vijiji vya Mkoa wa Kigoma mwezi huu wa Aprili/Mei 2007.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya Kijiji ikipimwa, kijiji hicho hupatiwa cheti cha Ardhi ya Kijiji. Baada ya hapo Serikali ya Kijiji kwa kushirikiana na watalaam wa Sekta ya Ardhi waliopo katika Halmashauri, watatambua mipaka ya maeneo ya wana kijiji

mmoja mmoja ili hatimaye mwananchi huyo aweze kupatiwa Hati ya kumiliki ardhi kimila. Hati hizo zinaweza kutumiwa kama dhamana kwenye taasisi za fedha ili kupata mkopo.

Hivyo ni matumaini yangu kuwa baada ya kupima mipaka ya vijiji, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, itaendelea na zoezi la kutambua maeneo ya mwananchi mmoja mmoja ili hatimaye kuwawezesha wananchi kupata hati miliki za ardhi za kimila. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa kazi nzuri anazofanya katika jimbo lake katika kushughulikia masuala ya ardhi. (*Makofi*)

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi huo mzuri ambao pengine najua wananchi wa Bukombe sasa wataweza kupata hata mikopo katika mifuko ya pembejeo ambayo ilikuwa imeshindikana. Baada ya kusema hayo kwa kuwa Wilaya ya Bukombe ni moja ya Wilaya mpya na kwa kuwa utaratibu huu unakuwa mgeni katika Wilaya ile.

Je, Serikali inaweza ikakubalina na mimi aidha Waziri au Naibu Waziri atembelee Wilaya ya Bukombe aweze kufanya mkutano ili aongee na wananchi kuweza kuwaelimisha suala hili ikiwa ni pamoja na kutatua matatizo mbalimbali yanayosababishwa na kupanuka kwa mji? (*Makofi*)

**SPIKA:** Na kwa ziara hiyo nadhani unataka ufuatane naye? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa elimi inahitajika kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ili kuwahamasisha wakubali maeneo yao kupimwa na hasa Halmashauri zikubali pia kuchangia katika upimaji wa mashamba ya hao wananchi. Nakubali kabisa kwamba nitapenda kwenda Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Shinyanga na nitafuatana na Mbunge wa Wilaya hiyo kuhakikisha kazi inafanikiwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujua ni vigezo gani vinatumika kuchagua maeneo yapi yaanze na yamaliziwe katika kupima vijiji na ni lini kwa utaratibu huo wataenda kupima vijiji katika Wilaya ya Ludewa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Mwalyosi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyojibu vizuri sana Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba nchi nzima ina vijiji vijiji 14,000 lakini vijiji ambavyo tayari vilikuwa vimeshapimwa hadi sasa hivi vilikuwa ni vijiji 6,000 na kwa mwaka juzi vilipimwa vijiji 119 katika Wilaya ya Iringa vijijini.

Kwa hiyo, hakuna taratibu zozote zinazotumika katika kuchagua mahali. Lakini kwa zoezi hili ambalo tumelianza katika mwaka huu tumepanga kupima vijiji 3,104. Kwa sasa hivi wapimaji wako katika Wilaya ya Mufindi.

Lakini pia wako katika Wilaya ya Kasulu wanamalizia kule. Kwa leo hii nilikuwa nazungumza nao wamemaliza katika Mkoa wa Rukwa na mpaka sasa hivi vimeshapimwa vijiji 1,615. Kwa hiyo, nataka kumdhibitishia Mheshimiwa Mbunge Mwalyosi kwamba Mkoa wa Iringa nao unahusika katika kupimwa vijiji vinavyohusika ikiwa ni pamoja na Wilaya yake na jimbo lake. (*Makofi*)

Na. 32

**Mikopo ya Shilingi Bilioni Moja**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imetenga shilingi bilioni moja za mkopo, ili kupunguza umaskini kupitia wajasiriamali watu binafsi vikumbi na *SACCOS* na kwa kuwa wananchi wengi wamehamasishwa na wamejiandaa kukopa fedha hizo:-

Je, hadi tarehe 31 Machi, 2007 ni wajasiriamali wangapi, vikundi na *SACCOS* ngapi zimechukua mikopo hiyo kwa takwimu kutoka Wilaya za Geita, Moshi, Ilala na Urambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naona una hamu ya kujibu upesi sana umefika hapo kabla sijakuita lakini endelea. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH SOLOMON SUMARI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Nyang'wale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31/3/2007 idadi ya Wajasiriamali, vikundi na *SACCOS* zilizopata mikopo kutoka Wilaya za Geita, Moshi, Ilala na Urambo ni kama ifuatavyo:-

Wilaya ya Geita idadi ya Mikopo iliyokuwa imetolewa ni 100 thamani ya mikopo hiyo ni shilingi milioni 114,600,000 na maombi ya mikopo ambayo yalikuwa yamepokelewa Benki lakini ambayo yalikuwa bado kwenye tathimini ni ya wajasiliamalia 776 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,314,764,000.

Wilaya ya Moshi idadi ya mikopo ambayo ilikwishatolewa ni 98 yenye thamani ya shilingi milioni 99,420,000 mikopo ambayo ilikwishapokelewa na benki ambayo iko kwenye tathimini ya wajasiriamali 2,192 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,475,420,820.

Wilaya ya Ilala walikwishapewa mikopo wajasiriamali 113 mikopo yenye thamani ya shilingi 285,300,000. Mikopo ambayo imepokelewa kama maombi ambao iko kwenye tathimini ni ya wajasiriamali 1830 na thamani yake ni shilingi bilioni 5,076,470,000.

Wilaya ya Urambo wajasiriamali 46 walikwishapata mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 78,550,000 na mikopo ambayo iko kwenye ngazi ya tathimini ni ya wajasiriamali 16 yenye thamani ya shilingi milioni 29,575,000. (*Makofi*)

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Serikali ilihamasisha wajasiriamali na vikundi vya *SACCOS* wachangamkie mikopo hiyo ikatoa miongozo na kwamba hawatakahitajika kuwa na dhamana na masharti ya kibenki. Na kwa kuwa mabenki yaliwakatalia hasa wale wakulima na wafugaji na kwa hiyo wakasononeka wanachanganyikiwa na wengine wamenuna.

Je, Serikali iko tayari kuwaomba radhi hawa wajasiriamali mmoja mmoja wakulima na wafugaji na baadaye itoe ahadi kwamba itarekebisha kasoro hizo ili wafaidike na mkukuta?

(b) Kwa kuwa fedha hizi za mkukuta zilikuwa kwenye mabenki makuu mawili *CRDB* na *NMB* na kwa kuwa *NMB* ndiyo iko karibu sana na wananchi kwa maana ya kwamba iko karibu Wilaya zote na kwa hiyo ikawa na mlundikano wa mikopo ya wajasiriamali vikundi na *SACCOS* na wewe hujikuta unamaliza fedha mapema wakati *CRDB* bado walikuwa bado na fedha.

Je, Serikali iko tayari kurekebisha sasa kwamba *NMB* ipelekewe fedha nyingi zaidi kuliko *CRDB* kwa sababu ndiyo iko karibu na wananchi Wilayani? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwanza katika mpango mkuu ambao umeandaliwa na Serikali wa kuwawezesha wananchi hakuna dhamana inayohitajika. Dhamana inatolewa na benki na ilikwishatolewa kiasi cha shilingi bilioni 10.3. Kinachotakiwa ni mwananchi atengeneze mchanganuo ambao ni rahisi tu kujaza fomu kupitishia kwenye kijiji ama mtaa halafu baadaye kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata yake halafu kuyapeleka maombi hayo benki. Yanapofika kule, benki nayo ni lazima ifuate taratibu za kibenki. Maana hii mikopo ndugu zangu siyo bure. Alipotangaza kwa mara ya kwanza utaratibu huu Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema mambo mawili ya msingi. La kwanza ni kwamba mikopo hii ingekuwa na thamani ya shilingi bilioni 21 kwa nchi nzima kwa wastani wa shilingi bilioni 1 kila mkoa.

Pili, hii mikopo ingepitia benki na kwamba taratibu ambazo zingefuatwa ni taratibu za kibenki. Sasa kwa hiyo pale ambako wakulima, na hapa tunahimiza kwamba

wakulima ndiyo wapewe hizi pesa na hii mikopo ni kwa ajili ya uzalishaji, wamekwamishwa. Siyo kwa sababu lazima kuna hitilafu na kama kuna kesi ambayo ni dhahiri ambayo amenyimwa na anastahili, tunaomba tufahamishwe na tuifuatilie na tuone kama tunaweza kumsaidia kupata hiyo mikopo.

Jambo la pili ni fedha kwisha. Fedha hazijakwisha mpaka sasa hivi, kiasi cha mikopo ambacho kimetolewa na benki hizi mbili ni shilingi bilioni 4.6 tu. Jumla ya fedha ambazo bado benki hizi mbili zinaweza kutoa kama mikopo ni shilingi bilioni 31. Hicho ndicho kiasi ambacho benki inaweza kutoa kwa makubaliano kati ya Serikali na benki zenyewe. Kilichotokea ni kwamba mpaka kufikia tarehe 19 Machi, kwa sababu ya uhamasishwaji wa wananchi benki ya NMB ilikuwa imepokea maombi yapatayo shilingi bilioni 105.

Kwa hiyo, kwa kushauriana na Serikali ikaonekana si vema kuendelea kupokea maombi zaidi isipokuwa isitishwe ili yale ambayo yamekwishapokelewa yaende yafanyiwe tathmini halafu yakimalizika ndiyo mikopo mingine, maombi mengine yaendelee kupokewa. Kwa upande wa *CRDB* kufikia tarehe 31 walikuwa wameshapokea maombi yanayofikia shilingi bilioni 8. Kiasi ambacho walikuwa wamekwishatoa ni shilingi bilioni 1 na milioni 76 tu. Kwa hiyo, bado hatujafika popote katika kuzimaliza pesa ambazo zimetolewa na Serikali kwa ajili ya huu utaratibu.

Tukumbuke Waheshimiwa kwamba ni miezi miwili na nusu tu tokea hii mikopo ilipoanza kutolewa. Kwa hiyo, ni muda mfupi sana hata wa kufanya tathmini ya kina ambayo itatuwezesha kuelewa upungufu upo wapi na turekebishe wapi. *(Makofi)*

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kuwafikia wajasiriamali wengi ambao wengi wapo kule vijijini na ndio maana ikaainishwa Benki ya *NMB, CRDB*, Aspsi na nyingine kama *SCULT*. Tunajua kwamba asasi kama *SCULT* wanao mtandao mkubwa wa kuweza kuwafikia wananchi hata vijijini; je, ni lini zile shilingi bilioni 10.5 zitatolewa kwa asasi kama hizo kusudi wajasiriamali wengi waweze kufaidika na mpango huo wa Serikali? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwamba katika mpango huu wa Serikali wa kuwawezesha wananchi kuna mifumo miwili. Mfumo wa kwanza, ni huu ambao tayari umekwishaanza kufanya kazi ambapo shilingi bilioni 10.5 zimewekezwa kama dhamana kupitia hizi benki zetu mbili za CRDB na NMB.

Mfumo wa pili sasa hivi unafanyiwa kazi na Benki Kuu ambao thamani yake ni shilingi bilioni 10.5. Tathmini ya Benki Kuu na kutayarisha utaratibu wa kuwapa wananchi wetu mikopo kupitia mfumo huu bado haijakamilika. Sababu mojawapo ya kinachoonekana kuchelewa kuanza kwa mfumo huu wa pili ni kwamba tujipe muda angalau kidogo tuweze kuelewa huu tulioanza nao unakwendaje, ingawaje kwa kweli hii

mifumo miwili tofauti, kwamba mmoja ambao unapitia Benki Serikali imetoa pesa na ndizo zinakuwa dhamana. Huu wa pili, lengo ni kwamba *SCALT, Pride* na zile benki za wananchi kama Mufindi, Mwanga zitakapokuwa zimepewa pesa hizi zenyewe zitakopesha wananchi moja kwa moja.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba bado mpango huo upo. Upo kwenye maandalizi na tegemeo la Serikali ni kwamba mara Benki Kuu itakapomaliza kuandaa basi na wenyewe utaanza kazi na kwamba kutakuwa sasa na mipango miwili ambayo inakwenda sambamba. *(Makofi)*

Na. 33

**Ujambazi katika Daraja la Kilumi – Mara**

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI** aliuliza:-

Kwa kuwa daraja la Kilumi lipo Mkoa wa Mara kwenye barabara itokayo Sirari Wilayani Tarime kwenda Mwanza na kwa kuwa daraja hilo limekuwa halina ulinzi kiasi kwamba upo ujambazi uliokithiri ambapo wananchi huibiwa mali zao na magari huporwa;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuokoa maisha ya wananchi wa Mkoa wa Mara na Watanzania kwa ujumla dhidi ya ujambazi huo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, daraja la Kilumi ni daraja muhimu ambalo ni kiungo kati ya Mkoa wa Mara na Mkoa wa Mwanza. Daraja hili lipo umbali wa kilomita 24 toka kituo cha polisi Musoma Mjini. Katika kipindi cha Julai, 2006 mpaka sasa hakuna ujambazi wowote uliotokea kwa mujibu wa taarifa ya jeshi la polisi Mkoa wa Mara. Pamoja na hali hiyo, Jeshi la Polisi linaendelea kuimarisha ulinzi katika eneo hilo na vijiji vya jirani kwa kufanya doria pamoja na kuwashirikisha wananchi wa maeneo hayo katika ulinzi shirikishi.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Nianze tu kwa kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Lakini ningependa tu Mheshimiwa Naibu Waziri aelewe kwamba tunapoleta maswali ndani ya Bunge hili tayari tunakuwa tumepata malalamiko kutoka kwa wananchi wetu na vile vile tumefanya uchunguzi kuhusiana na tatizo ambalo tumewasilishiwa na wananchi wetu. Pale darajani zipo nyumba mbili ambazo zilikuwa zinatumika wakati wa ujenzi wa daraja lile lakini nyumba zile zimeachwa na sasa hivi hazitumiki na kitu chochote. Kwa nini nyumba hizi zisitumike na kukarabatiwa na Wizara husika ili

ziweze kutumika na polisi ili kupunguza ile adha ya polisi kutoka Musoma Mjini kuja kulinda daraja hilo au kutoka Tarime Mjini kuja kulinda daraja hilo?

Swali la pili, katika daraja hilo hilo kuna tangazo ambalo linasema kwamba hairuhusiwi kupiga picha darajani hapa. Lakini pale kumekuwa na watalii ambao wanatoka Kenya wakielekea mbuga za wanyama Serengeti, wamekuwa wakisimama darajani pale na kupiga picha. Je, Wizara husika haioni kwamba suala hilo ni hatari kwa nchi hususan Mkoa wa Mara na wananchi wake wanaoishi katika maeneo yale? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli upo umuhimu mkubwa wa kuimarisha ulinzi hasa katika maeneo nyeti yakiwemo madaraja. Lakini ni ukweli usiopingika katika nchi yetu yapo madaraja mengi sana. Kwa hiyo, tukiamua kila kwenye daraja kupeleka askari polisi sifikiri kama tutakuwa na uwezo wa askari hao kuweza kufanya kazi nyingine za kupambana na uhalifu.

Nafikiri Mheshimiwa Mbunge ungekubaliana na mimi kwamba hii mbinu inayotumika sasa ya kufanya doria na ulinzi shirikishi pamoja na mbinu zingine za kiaskari ziendelee kutumika. Hata ushauri wake kuhusiana na nyumba hizo tumeuchukua, tutautafakari ili tuone nini tunaweza kufanya kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. *(Maokfi)*

Kuhusu watalii wanaopiga picha pale darajani mahala ambapo pameandikwa si ruhusa kupiga picha, maana yake si ruhusa kupiga picha. Kwa hiyo, hatua na utaratibu wa kisheria utachukuliwa ili kukomesha jambo hilo.

Na. 34

**Mafunzo ya *HIV* na Uelimishaji rika sehemu za Kazi**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa katika kipindi cha bajeti ya mwaka 2005/2006 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto iliweka kitengo cha wawezeshaji wa mafunzo ya HIV na Uelimishaji rika sehemu za kazi katika Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia; na kwa kuwa Waziri alisema utekelezaji wa kazi hiyo haujafanyika kutokana na kuchelewa kwa fedha za maendeleo (TMAP):-

Je, fedha zinazohusiana na mafunzo hayo zinategemewa kufika lini na kama hazijafika ni hatua gani zitachukuliwa za kufanikisha jukumu hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Said, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Bajeti ya mwaka 2005/2006, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto haikuwahi kuanzisha kitengo cha wawezeshaji wa mafunzo ya HIV na uelimishaji rika sehemu za kazi katika Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu, swala la kudhibiti UKIMWI mahali pa kazi chini ya *Tanzania Multi-Sectoral Aids Project (TMAP)* ni jukumu la kila Wizara husika katika kuandaa na kuendesha mafunzo haya kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na *TACAIDS.*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa upande wake, ilipokea fedha za UKIMWI toka *TACAIDS,* robo ya mwisho ya mwaka 2005/2006 mwezi Machi 2006. Baada ya kupokea fedha hizo kutoka TACAIDS, ilianza na inaendelea kutoa mafunzo ya *HIV* na uelimishaji rika kwa watumishi wake katika ngazi mbalimbali, wakiwemo Wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Makarani, Wahasibu, Walimu na Wahudumu waliopo kwenye vyuo vinavyosimamiwa na Wizara.

Aidha, mafunzo ya unasihi yametolewa kwa wawakilishi wa kada mbalimbali katika Vyuo vya Wizara Kanda ya Kaskazini na Makao Makuu ya Wizara. Mafunzo haya huwawezesha wawakilishi kuendelea na utoaji wa ushauri na uhamasishaji kwa watumishi wanaoishi na VVU na wale ambao hawajapima afya zao waweze kupima. Mafunzo ya aina hii yanaendelea kutolewa kwa awamu katika Kanda zilizobakia kutegemeana na hali ya upatikanaji wa fedha.

Na. 35

Ada ya Uanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

**MHE. USSI AME PANDU** aliuliza:-

Kwa kuwa kila nchi mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hulazimika kuchangia ada ya uanachama:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kila nchi mwanachama hupaswa kuchangia kila mwaka?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha Zanzibar hupaswa kuchangia ikiwa kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Mtoni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kiasi cha mchango hutegemea ukubwa wa bajeti ya mwaka husika. Kwa mfano, mwaka 2006/2007 kila nchi inapaswa kutoa mchango wa dola za Kimarekani 4,054,973 katika bajeti ya Jumuiya.

Ni dhahiri kwamba makadirio ya mapato na matumizi ya jumuiya hupangwa kulingana na mahitaji ya mwaka husika. Baada ya hapo kiwango cha matumizi hugawanywa kwa nchi wanachama sawia. Kwa hiyo, hakuna kiwango maalum cha michango bali hubadilika kulingana na bajeti ya jumuiya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mchango wa Zanzibar, Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Treaty)* unaitambua Tanzania kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikimaanisha kwamba Zanzibar ni sehemu ya Tanzania. Kwa mantiki hiyo, Zanzibar haiwajibiki kutoa mchango katika Jumuiya kama nchi peke yake. Kwa hiyo, mchango katika Jumuiya ya Afrika Mashariki unaolipwa na Wizara ya Fedha kupitia kwenye bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki unajumuisha Zanzibar pia. *(Makofi)*

Na. 36

**Mchakato wa Kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza:-

Kwa kuwa mchakato wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuelekea Shirikisho la Afrika Mashariki una sehemu kubwa nne, yaani Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Matumizi ya Sarafu Moja na kuunda Shirikisho; na kwa kuwa sasa wananchi wa Kenya, Uganda na Tanzania wametakiwa kutoa maoni yao kuhusu kuharakishwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki:-

(a) Je, kwa nini maoni hayo ya wananchi yasitolewe katika hatua tatu kabla ya Shirikisho?

(b) Kwa kuwa muundo wa Umoja wa Forodha umekamilika na unatekelezwa; je, ni matatizo gani makubwa yanayolalamikiwa miongoni mwa wafanyabiashara katika utekelezaji huo kwa nchi za Kenya, Uganda na Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mhesihmiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, ningependa kutoa maelezo yafuatayo:-

Shirikisho la Kisiasa ni hatua ya mwisho katika mchakato wa ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Chimbuko la kuangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki ni Mkutano wa Kilele *(Summit)* wa Wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Nairobi, Kenya, tarehe

27-29 Agosti, 2004. Wakuu hao walishawishika kuangalia iwapo Shirikisho la Kisiasa baina ya nchi wanachama linaweza kuharakishwa au hapana.

Wakuu hao wa nchi za Afrika Mashariki waliunda Kamati ya kuangalia uwezekano wa kuharakisha uanzishwaji wa Shirikisho katika kipindi kifupi kadri iwezekanavyo. Kamati hiyo iliongozwa na Mheshimiwa Amos Wako, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya na iliwasilisha Taarifa yake kwa Wakuu wa nchi wanachama katika mkutano wao wa kilele mwaka 2005. Wakuu wa nchi wanachama waliipokea Taarifa husika na kukubaliana kwamba wananchi washirikishwe kutoa maoni na mapendekezo juu ya kuharakishwa Shirikisho. Kwa hatua hii, Viongozi Wakuu wa Jumuiya walikusudia kutoa fursa kwa wananchi kushiriki katika kuamua hatima ya mtangamano wa Jumuiya na maendeleo yake kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 7 cha Mkataba wa Jumuiya.

Zoezi la kukusanya maoni lilizinduliwa rasmi na Wakuu wa nchi wananchama wa Jumuiya sawia katika miji ya Dar es Salaam, Nairobi na Kampala, tarehe 13 Oktoba, 2006. Baada ya hapo wananchi wameendelea kutoa maoni. Zoezi hili litahusisha Mikoa na Wilaya zote za Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Mntangi, kama ifuatavyo:-

(a) Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeainisha hatua za mtangamano kuanzia Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Sarafu Moja na hatimaye Shirikisho. Hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni ya msingi kwamba ingewezekana wananchi wakaulizwa uharakishaji wa hatua za kati za mtangamano. Hoja hii ilijibiwa na Kamati ya Wako ambayo kwa kuzingatia uharakishaji wa Shirikisho ilipendekeza pia kufupisha muda wa kutekeleza hatua za Soko la Pamoja, Sarafu Moja na Shirikisho. Kwa maana hiyo kuharakisha Shirikisho si lazima kuruka hatua za mtangamano nilizoainisha bali kuangalia uwezekano wa kuzifupisha.

(b) Vikwazo visivyo vya kodi katika biashara ni miongoni mwa kero kubwa zilizojitokeza katika kutekeleza Itifaki ya Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki. Vikwazo vilivyopo ni pamoja na miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji isiyoridhisha, vizuizi vya barabarani *(road blocks)* visivyo vya lazima na taratibu ngumu za forodha na ukiritimba. Mwezi Agosti, 2006 nchi wanachama zilibuni mfumo wa kukabiliana na vikwazo visivyo vya kodi. Chini ya mfumo huu, Kamati za kitaifa zimeundwa kuratibu vikwazo na Kamati zitazinduliwa hivi karibuni. Aidha, wafanyabiashara watapewa fomu maalumu ya kujaza vikwazo wanavyokumbana navyo safarini na kuwasilisha katika Kamati za Kitaifa ambazo zitachukua na kupendekeza hatua zifaazo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa hatua inayofuatia baada ya Umoja wa Forodha ni Soko la Pamoja na kwa kuwa Tanzania na Uganda zina viwanda vichache ukilinganisha na Kenya; Je, Serikali inasema nini kuhusu hofu ya Watanzania kwamba

kwa sababu hiyo ya kutokuwa na viwanda vya kutosha uchumi wa Tanzania utadhoofika ndani ya Shirikisho? *(Makofi)*

Swali la pili, katika mfumo wa EPA ambapo sasa hivi yanaendelea makubaliano kati ya nchi za Afrika na Umoja wa Nchi za Ulaya *(European Union.),* Tanzania, Kenya na Uganda kwa pamoja zilikubaliana kwamba wafanye ushauri huo kwa pamoja kama Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini Kenya na Uganda wakajitoa na wanaendelea wao peke yao na majadiliano hayo na *European Union* hivyo kuilazimisha Tanzania kuingia katika kundi lingine la *SADC, EPA* kuendelea na majadiliano. Je, kitendo hicho cha Kenya na Uganda hakionekani kwetu kama kinaweza kikadhoofisha Jumuiya ya Afrika Mashariki? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ukiangalia kiviwanda, kwa haraka haraka utaona kwamba kiviwanda Kenya wanaonekana kuwa mbele ya Uganda na Tanzania. Lakini vile vile ukiangalia kwa takwimu ni kwamba viwanda kwa Kenya vinachangia asilimia 15 ya pato la Taifa na Tanzania na Uganda vinachangia wastani wa asilimia 14 kwa pato la Taifa. Kwa hiyo, pamoja na ukweli huo lakini tofauti si kubwa sana ya kutisha. Pamoja na hayo mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki una kitu kinaitwa *Asymmetric Principle.* Ni kwamba katika masuala yote ya ushirikiano pale inapoonekana kwamba nchi fulani ikitekeleza makubaliano ya ushirikiano itapatwa na matatizo makubwa basi jitihada za makusudi lazima zichukuliwe na ndiyo maana wakati wa mazungumzo ya kuanzisha Ushuru wa Forodha wa Pamoja ilikubalika kodi za bidhaa kutoka Kenya kuja Tanzania ziendelee kutozwa kodi inayopungua taratibu na baadaye tutafanya tathmini ni jambo gani linaweza likafanyika. Kwa hiyo, sera za Afrika Mashariki zinatoa fursa ya kulinda viwanda vyetu. Lakini vile vile siyo kulinda tu lazima tuchukue na hatua za kuhakikisha kwamba tunaimarisha viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kwamba nchi za Afrika Mashariki zilikubaliana kwamba zijadiliane kwa pamoja, naomba niseme katika hili hakuna makubaliano rasmi ambayo yalikwishafanyika kuhusu hiyo. Kwa hiyo, huwezi ukasema kwamba Kenya ilijiondoa, au Uganda ilijiondoa, isipokuwa yapo makubaliano.

Mazungumzo yanayoendelea hivi sasa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuangalia uwezekano wa Afrika Mashariki kama Afrika Mashariki jinsi gani tunavyoweza kujenga hoja kwa pamoja kama ambavyo tulipokwenda Geneva na tukatetea sera za Tanzania za uchumi na mambo mengine kama Afrika Mashariki. Ni matarajio yetu kwamba masuala ya *EPA* na yenyewe tutayaweka vizuri lakini hivi sasa mazungumzo yanaendelea vizuri na hakuna tatizo lolote. *(Makofi)*

Na. 37

**Ubinafsishaji wa Benki ya NMB**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2003 Bunge lilipitisha mabadiliko ya Sheria ya *National Microfinance Bank* ili kuiwezesha Serikali kuibinafsisha Benki hiyo kwa kuuza kwa wakati mmoja asilimia 49% ya hisa za NMB kwa mwekezaji kiongozi (Benki yenye uzoefu) na asilimia 21% ya hisa za benki hiyo kwa Watanzania/Kampuni zinazomilikiwa kikamilifu na Watanzania na kwa kuwa tangu mabadiliko ya Sheria hiyo yapate kibali cha Mheshimiwa Rais mwaka 2004 ni asilimia 49% tu za hisa za benki hiyo zimeuzwa kwa Mwekezaji Kiongozi Benki ya Rabo ya Uholanzi:-

(a) Je, kwa nini mpaka sasa Serikali haijauza asilimia 21% ya hisa za benki hiyo kwa Watanzania?

(b) Je, ni lini Serikali itatimiza matakwa ya Sheria ya kuwauzia Watanzania/Kampuni zinazomilikiwa kikamilifu na Watanzania asilimia 21% za hisa hiyo na kuiwezesha Benki hiyo kama inavyotakiwa kwa mujibu wa sheria hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H.MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali iliuza asilimia 49 ya hisa zake katika *National Microfinance Bank* yaani NMB kwa kundi la wawekezaji yaani *Consortium* linaloongozwa na Benki ya *RaboBank.*. Katika kundi hilo kuna kampuni za Kitanzania kama zifuatazo:-

| | |
|---|---|
| *National Investment Company Ltd. (NICO)* | *6.6%* |
| *Exim Bank Tanzania Ltd.* | *5.8%* |
| *Tanzania Chambers of Commerce Industries and Agriculture (TCCIA)* | *1.7%* |

Mwekezaji kiongozi *(Rabobank)* alinunua hisa asilimia 34.9% tu.

Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako tukufu likipitisha mabadiliko ya Sheria Na. 23 ya mwaka 2003 ya *National Microfinance Bank (NMB)* kuruhusu ubinafsishaji wa benki hii, Serikali ilidhamiria kuuza asilimia 21 ya hisa za Serikali katika benki hiyo kwa wananchi kupitia soko la Hisa la Dar es Salaam mapema iwezekanavyo.

Hata hivyo, kwa kuwa ni katika kipindi hicho hicho wawekezaji wa *Rabobank Consortium w*alikuwa wameteuliwa kuendesha uendeshaji wa benki hiyo, Serikali iliona ni muhimu kuhakikisha kwamba ufanisi wake chini ya Manejimenti hii unaimarika kwanza baada ya ubinafsishaji, ndiyo mchakato wa kuuza hisa wa asilimia 21 ufanyike.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuona ufanisi wa benki hii umeimarika katika kipindi cha miaka mitatu kama matakwa ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)* yanavyotaka, mchakato wa Serikali wa kuuza asilimia 21 ya hisa zake kwa wananchi kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE)* umeshaanza.

Serikali itahakikisha kuwa Watanzania wengi wananunua hisa za NMB pamoja na zile za Makampuni mengine yanayoendeshwa vizuri na yanayopata faida, na hivyo kupunguza uwezekano wa wananchi hao kupoteza fedha zao. Inatarajiwa kwamba mchakato wa kuuza hisa za Serikali asilimia 21 katika NMB utakamilka mwezi Julai, 2007.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu mazuri lakini ningependa nimrejeshe kwenye Sheria yenyewe. Sheria haikutamka kuuza *share* 21 kupitia soko la mitaji, Sheria inasema *share* 70% zitauzwa kwa utaratibu kama ilivyo swali lilivyouliza kwa mara moja. Kwa hiyo, kwa kitendo cha Serikali kutoziuza *shares* hizi kwa mara moja imefanya kosa la kisheria bila idhini ya Bunge. Sheria ninayo hapa na nadhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha atakuwa nayo, lakini Sheria ipo wazi kwamba *share*s hizi zilitakiwa mara ziuzwe mara moja zote kwa pamoja. Sasa maswali haya yafuatayo napenda yapate majibu:-

1. Kwa kuwa Sheria ilitaka *shares* hizi ziuzwe mara moja na mpaka leo asilimia 21 haijauzwa na thamani ya benki hii imepanda; Je, Serikali ipo tayari kuziuza *shares* hizo za asilimia 21 kwa bei ileile ambayo iliziuzia zile za 49? *(Makofi).*

2. Mheshimiwa Naibu Waziri katika jibu lake la msingi amesema watajitahidi wauze *shares* hizi kwa Watanzania, mimi napata wasiwasi kwa sababu benki hii ni ya nchi nzima. Elimu ya Watanzania juu ya masoko ya mitaji ni ndogo, na ni haki ya kila Mtanzania kutumia fursa hii kuwa na hisa kwenye benki hii yetu. Nilikuwa naishauri Serikali kama itakubalika mgao wa hizi asilimia 21 za benki hii *National Microfinance* ziuzwe kwa mikoa yote 21. Kila mkoa upate *percent* yake moja ya *ownership* kwenye benki hii. Hayo ndiyo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa nyongeza ya Sheria ambayo ilisainiwa na Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu, tarehe 30/1/2004, Section 6(A)(2), inasema hivi, *"where the shares or loan capital of the National Microfinance Bank Limited have been vested in the Treasury Registrar, the Minister shall cause to be sold seventy percent of the shares being: (a) forty nine percent to a consortium of strategic investors led by a commercial bank having proven experience in banking business; and (b) twenty one percent to citizens of Tanzania or a body corporate whose beneficial ownership is held by citizens of* Tanzania *or by companies whose share capital are wholly* owned *by citizens of Tanzania.. Section 6(B), inatamka, "upon the selling of seventy percent of its shares in the National Microfinance Bank Limited or upon the government ceasing....",* hiyo haina maana!

Sasa kwa sheria hii Serikali iliamua kwamba, tuanze kwanza zile s*hare* 49 kwa *strategic investor* ambaye tulimpa *World Bank*, mtakumbuka kwamba wakati tunabinafsisha NMB haikuwa katika hali nzuri, kwa hiyo, usingeweza kuuza zile *share* zote asilimia 70 wakati ule wakati benki ina matatizo. Sasa Serikali imeamua kwamba hizi asilimia 21 zinauzwa na mchakato umeshaanza, *prospectus* imeangaliwa, mthamini kateuliwa, wanasheria wameteuliwa na bei gani *share* hizi zitauzwa itategemea na mthamini atakavyotushauri. Kama mshauri atasema ziuzwe kwa bei ile ile ya mwanzoni Serikali itaziuza kwa bei hiyo. Kama mshauri atasema kwamba ziuzwe kwa bei kubwa, tutauza kwa bei kubwa. Niwape mfano, NMB is the *stronger bank* hapa nchini, tukisema tuuze kwa bei ya thamani ya benki hiyo leo *share* moja itakuwa si chini shilingi 2000.

Lakini kwa jinsi mnavyoelewa na mchakato unaofanyika, *shares* hizi zitauzwa kwa bei ambayo itakuwa ni ndogo kuliko hizo shilingi 2000. Kwa hiyo, ningeshauri tuwaachie wataalamu wafanye tathimini, waishauri Serikali na Serikali itaziuza *share* hizo kwa ushauri wa kitaalamu ambao tutakuwa tumeupata badala ya kujifanyia mambo.

La pili, namna pekee ya kuweza kuwafanya watanzania wengi wanunue hisa katika benki hii ni kwa kutumia soko la hisa, *shares* haziwezekani ukasema asilimia 21 ziko *shares* 420,000, basi uzigawanye kila mkoa upate *shares* zinazotakiwa, haiwezekani kufanya hivyo. Utaratibu uliopo ambao umetumika kwa makampuni yote ni kuziuza *shares* kwa kutumia soko.

Na. 38

**Kuunda Chombo cha Kusimamia Mazao ya Nafaka na Matunda**

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE** Aliuliza:-

Kwa kuwa mazao kama Korosho, Kahawa, Chai, Tumbaku n.k. yameundiwa Bodi ya maalumu za kusimamia uzalishaji, ubora na maendeleo ya mazao hayo; na kwa kuwa mazao yote ya nafaka na yasiyo ya nafaka kama zabibu na matunda kwa ujumla hayana chombo maalum cha Kiserikali cha kuyasimamia kama ilivyo kwa hayo mazao mengine, badala yake yameachwa mikononi mwa wakulima wenyewe na soko huria:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kwa kufanya hivyo uzalishaji bora na maendeleo ya mazao hayo unaendelea kuzorota?

(b) Je, Serikali ina mpango gani sasa kwa kuunda chombo maalumu cha kusimamia mazao yasiyokuwa na Bodi hasa nafaka na matunda?

**NAIBU WAZIRI KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA (MHE. CHRISTOPHER K. CHIZA)** Alijibu**:-**

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe lenye sehemu (a) na (b) ninapenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Suala la usimamizi wa maendeleo ya mazao ya nafaka na mazao mengine ni la msingi. Kinachotakiwa kufanywa ni kuboresha mazingira yatakayochangia kuongezeka kwa ubora na tija katika mfumo mzima wa uzalishaji wa masoko ya mazao hayo. Itakumbukwa kuwa kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa sera ya soko huria, vilikuwepo vyombo maalum vilivyohusika na mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko yaani *General Agricultural Products and Export Board (GAPEX*) kwa ajili ya mazao mchanganyiko na Shirika la Usagishaji la Taifa (*NMC*) kwa ajili ya mazao ya nafaka. Aidha, Shirika la Kilimo na Chakula (*NAFCO*), lilisimamia uzalishaji wa nafaka katika mashamba makubwa. Kutokana na uendeshaji dhaifu pia uhaba wa mitaji mashirika yote haya yalishindwa kuendelea na shughuli zake. Aidha, kutokana na mabadiliko ya kisera hususan sera za kiuchumi miaka ya 1980; Serikali ilijiondoa kwenye shughuli za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kuvunjwa au kubinafishwa kwa taasisi hizo kuliyaacha mazao ya nafaka na mengine ya chakula katika mikono ya mfumo wa soko huria kwa asilimia mia moja, ikiwa ni pamoja na udhibiti wa masuala ya ubora wa mazao hayo. Tunajua kwamba masuala ya udhibiti na usimamizi wa mwenendo wa soko huria yamekuwa siyo ya kuridhisha. Hali hii imedhihirisha umuhimu wa Serikali kuwa karibu zaidi katika usimamizi wa mwenendo wa soko huria, hususan katika mazao hayo.

Baada ya maelezo hayo ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, kama ifuatavyo:-

(a) Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kutokuwepo kwa chombo maalum cha kusimamia uzalishaji, ubora na maendeleo ya mazao ya nafaka na mazao yasiyo ya nafaka kwa kiasi kunachangia kuzorota kwa uzalishaji na ubora wa mazao hayo. Aidha, kutokuwepo kwa chombo hicho kumesababisha ukosefu wa usimamizi katika ununuzi pasipo kuzingatia madaraja; kutotumiwa kwa vipimo sahihi vya kuuzia mazao na udhaifu katika ufuatiliaji wa mwenendo wa masoko kwa lengo la kuweka mikakati inayomlinda mzalishaji. Hali hii inapunguza kasi ya kuendeleza mazao hayo kwa kuzingatia ubora ambao ni muhimu kwa chakula, kuongeza kipato cha wakulima na hivyo kupunguza umaskini.

(b) Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko zimekwishaanza kuchukua hatua za kuangalia uwezekano wa kuunda chombo kitakachosimamia mfumo mzima wa mwenendo wa masoko ya mazao ya kilimo zikiwemo nafaka na mazao mengine yasiyo ya nafaka. Mara maandalizi na hatua hizo zitakapokamilika Bunge lako tukufu litapatiwa taarifa na kuombwa kutoa maamuzi kwa ajili ya utekelezaji.

Na. 39

**Ujenzi wa Daraja Katika Mto Simiyu**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** Aliuliza:-

Kwa kuwa, Mto Simiyu kwa upande wa Jimbo la Sumve unapita Maligisu na kwa upande wa Jimbo la Magu unapita eneo la Kabila; na kwa kuwa, kati ya pande hizo palijengwa “drift” miaka thelathini (30) iliyopita; na kwa kuwa, mto huo hufurika sana nyakati za masika na kusababisha usumbufu kwa wananchi wa pande zote mbili kuvuka kwa sababu mto huo ni mkubwa mno; na kwa kuwa, hata aliyekuwa Balozi wa Japan, Mhe.

Sato aliwahi kuahirisha ziara yake alipofika kwenye eneo hilo na kushuhudia mafuriko makubwa, na wanawake na watoto wakivushwa kwa mtumbwi, jambo lililomfanya aahidi kutoa shilingi milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa daraja mahali hapo (fedha ambazo hazijatolewa); na kwa kuwa, tathmini ya ujenzi wa daraja hilo ilikwishafanyika chini ya Mhandisi wa Mkoa wa wakati huo:-

Je, ni lini daraja hilo litajengwa ili kuondoa adha kubwa iliyowapata wananchi wanaotumia njia hiyo?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU** Aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bukwimba – Maligisu – Kabila yenye urefu wa kilometa 32, ni Barabara ya Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kupitia wakala wa barabara Mkoa wa Mwanza yaani *TAN Road’s*. Mto Simiyu unakatisha barabara hii kwenye eneo la Maligisu (kilometa 26.4 kutoka Bukwimba.

Sehemu hiyo imejengwa daraja la chini *(vented drift*). Daraja la namna hii huruhusu maji kupita juu endapo mvua zitanyesha nyingi kupindukia. Mvua zikipungua, daraja hutumika kama kawaida. Madaraja ya namna hii yapo mengi nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, makisio ya ujenzi wa daraja sehemu ya Maligisu ni shilingi milioni 450. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haijaweza kujenga daraja la kawaida katika eneo hili. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutafuta fedha hizo ili daraja la chini lililopo sasa (*vented drift*) liweze kubadilishwa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa sababu ametaja kwamba kiasi ambacho kinaweza kutengeneza eneo hilo ni shilingi milioni 450 lakini amesema kwa sasa Serikali haina uwezo;

Kwa kuzingatia kuwa kazi ya kwanza lazima ifanyike kwa kazi ya usanifu, je, Serikali inaweza kutenga angalau shilingi milioni 50 ili usanifu ufanyike, na baadaye shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ombi lake litazingatiwa na tutaangalia uwezo wa bajeti, tuweze kufanya angalau usanifu.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipatia nafasi. Tukio la aliyekuwa Balozi wa Japan kushindwa kuendelea na safari ilikuwa tarehe 25/12/2001. Makisio ya daraja hilo yalifanyika mwaka 2001, ni kama miaka minne hivi imekwishapita.

Je, ni kweli kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu minne hivi imeshindwa kupata milioni 400 kwa kuwahurumia wananchi wa wilaya ya Kwimba Kaskazini, wilaya ya Magu? Kwa sababu siku hiyo mama mmoja alichukuliwa na maji akanusuriwa na wapiti njia, hivi kweli Serikali imeshindwa kuona huruma kwa watu hawa kwa kipindi chote hicho?

**NAIBU WAZIRI MIUNDOMBINU**: Mheshimiwa Spika, Serikali inawaonea huruma wananchi wake na ndiyo maana imekuwa ikijitahidi sana kuondoa matatizo ya wananchi katika nyanja mbalimbali za maendeleo. Lakini ni kweli kwamba bajeti ya taifa unaweza kuona shilingi milioni 450 kwamba ni ndogo lakini ukiangalia mahitaji ya nchi kwa ujumla na miradi ya maendeleo katika nchi nzima kiasi kile ni kikubwa. Sasa mimi nadhani nimshauri Mheshimiwa Bujiku Sakila kwamba tufuate ushauri aliosema Mheshimiwa Ndassa kwamba kwa mwaka ujao wa fedha basi tuanze kwa maana ya kufanya usanifu na baadaye tuangalie kuongeza hela katika bajeti zilizofuata tuweze kujenga daraja hilo. Matatizo anayoyasema ni kweli lakini nadhani uwezo ndiyo hapo tulipo na tutaendelea kwa utaratibu huo niliouelezea.

**SPIKA:** WaheshimiwaWabunge muda wa maswali umekwisha. Matangazo! Nninayo furaha, kwa heshima naomba nimtambulishe Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Lodovick Otouh, ambaye yuko kwenye *gallery* pale. (*Makofi*)

Nadhani ndiyo mara yake kwanza kuwapo ndani ya ukumbi, na tunamkaribisha sana, mimi kwa niaba ya Wabunge wote nakuahidi tutakusaidia na tutafanya kazi muhimu sana hiyo unayofanya ,kwa pamoja kwa faida ya wananchi wa Tanzania, karibu sana! (*Makofi*)

Hapo hapo katika *Speakers Gallery* tunao wajumbe kutoka nchi ambazo tunashirikiana nazo wakiwakilisha balozi mbalimbali ambazo ni *development partners* wetu wa Tanzania. Nitawataja halafu watasimama. Kwanza, ni bwana John Blatisho kutoka Ubalozi wa Uingereza, Bwana Hamis Babu kutoka *DFID*, Bi. *Chriza Christinesen* kutoka *European Union,* majina ya Ulaya haya magumu sana kidogo! *Thio Casperz* kutoka *European Union, Ditte Egineli* kutoka Ubalozi wa *Swiden, Ester Somsen* kutoka

Ubalozi wa Uholazi, Ummy Ali Mwalimu kutoka Ubalozi wa *Denmark*, na African Mlay kutoka *SIDA* Canada. (*Makofi*)

*On behalf of Parliament I wish to welcome all of you Development Partner Representatives, we are very happy with what you are doing in cooperation with our government and we wish that these programmes of cooperation will increase as we go ahead tackling the problems of Tanzania. We are honoured to have you with us, thank you! (Makofi)*

Wapo wanafunzi 35 kutoka Chuo cha Uandishi wa Habari, Dar es Salaam, ningewaomba wasimame, ni wale pale mkono wa kulia, karibuni sana. Natumaini kuanza kuhudhuria katika mikutano yetu ya Bunge tutawasaidia kuweza kupata utaalamu ulionolewa kuripoti mambo ya Bunge ambayo ni muhimu sana yaeleweke vizuri kwa wananchi.

Tunao wageni wengine watalii kutoka nchi rafiki, tunaye *Mr. Bryan Bow* kutoka Ufaransa, wametoka! Tuna Bi. *Tala Woden* kutoka Marekani, naona watalii wana haraka ya kwenda kuona Dodoma, tahadhari tu wasitumie nyama, na Bi. *Petra* naye kutoka Ujerumani. Hapo kwenye *Speakers Gallery* nina furahi kuwatambulisha watumishi na watangazaji kutoka *Radio Clouds FM* ya Dar es Salaam ambao ni kama ifuatavyo:-

Bwana Philip Simprian, ambaye kwa jina la kisanii anaitwa Kachero, huyu ndiye mtayarishaji mkuu wa *power breakfast*, kipindi cha asubuhi cha *Radio Clouds* ambacho ni maarufu sana hasa kwa kizazi kipya. Karibuni sana mje mara kwa mara kwa sababu tunawatazamia ninyi kutangaza shughuli za humu. Mwingine ni Bi. Fina Mango, ambaye naye ni mtangazaji, yeye kwa jina la kisanii katika maeneo ya Dar es Salaam, anaitwa ni *First Lady to be*, lakini Bi. Fina bahati mbaya kila anayegombea urais huwa ana mke tayari lakini endelea kutumaini tu. Yeye ni mtangazaji ambaye ni maarufu na wenzake wanamwita Bi. ubishi. Wa tatu ambaye si mdogo ni Ndugu Masoud Ali, yeye kwa jina la kisanii anaitwa Rais Mtarajiwa, naomba usimame! Sasa huyu umaarufu wake zaidi wale mnaosikia katuni za kipanya, ndiye kijana anayechora hizo, ukisoma mwananchi kila mara mtaona katuni ambazo zinaleta ujumbe wenye hisia wa kila namna. Ahsante sana Masoud kwa kazi nzuri sana unayoifanya, karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

*Colonel* Saleh Farrah, ameniomba nitambulishe wageni ambao ni familia yake, mkewe Bi. Masha Farrah na watoto wao watatu, Lutithia, Abdallah na Taric Aziz sijui wako wapi hao, basi naona hawakuwa na subira. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Viti Maalum Rukwa ameniomba niwatambulishe wageni wake mama Mgawe, Mwenyekiti wa UWT, mkoa wa Rukwa, karibu sana na pole sana kwa safari ndefu. Bi. Lucy Manda, Mjumbe wa Baraza la Taifa la UWT kutoka Rukwa, na mwalimu Mwajuma Haruna, shule ya msingi ya Nyerere Mpanda. Karibuni sana sana, najua mmesafiri safari ndefu na ngumu, lakini ndani humu kuna uwezo wa kutatua matatizo yenu, muwe na subira barabara za Mpanda na za Sumbawanga zitashughulikiwa, kitu muhimu ni kuweza kuhimiza yafanyike hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Juma Kilimbah, Mbunge wa Iramba Magharibi, ameniomba nitambulishe wageni wake wawili ambao ni Mheshimiwa Diwani Hamis Mambo, Diwani wa Kata ya Mtenkete. Nimetaarifiwa kwamba huyu ndiye Diwani anayewakilisha kata ambayo imevunja rekodi kwa ujenzi wa shule za sekondari katika Mkoa wa Singida, hongera sana Diwani natumaini sasa mtavuka lengo mwende sasa kwenye kujenga *high school,* kwa sababu naona hizi sekondari sasa zimeanza kuwa ni nyingi mno hizi za *form four*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mbunge Viti Maalum, ameniomba niwatambulishe wageni wake ambao ni wanae Hiliam, Giptisam, na Shinuna. Hhaya majina ya Zanzibar magumu, karibuni sana vijana, mimi kama Spika nawahakikishia kwamba mama anachapa kazi kweli kweli hapa Bungeni. Mheshimiwa John Lwanji, ameniomba niwatambulishe wageni wake, Stansilausi Kawinga, Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Rungwa, karibu sana Mwenyekiti, na Wema Abdallah, Mwenyekiti wa UWT kata ya Rungwa, karibu sana Mheshimiwa.

Mwisho wa utambulisho, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya ameniomba niwatambulishe wadogo zake ambao ni Jalia na Nasra, wale pale bado wadogo sana hawa, ahsante karibuni sana Bungeni natumaini mtafuata mfano wa dada yenu, ambaye ameingia kwenye siasa kwa kishindo kabisa.

Matangazo ya mikutano, Mheshimiwa Anna Abdallah, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, ameniomba nitangaze kuwa Wajumbe wote wa Kamati hiyo wakutane saa tano asubuhi katika chumba Na.231, ghorofa ya pili, mkutano ni mfupi tu. Kamati ya Bunge Mambo ya Nje, mkutano saa tano asubuhi hii, chumba 231. Pia Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi ukiacha wale wa upande wa Serikali, tunaombwa tukutane na *development partners* saa saba na robo pale kwenye *conference room* ya Spika. Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi tafadhalini tukutane na wenzetu hawa waliotoka mbali kuja kuzungumza na sisi mambo yanayohusu maendeleo ya Bunge letu. Mheshimiwa George Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ameomba kwamba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala leo tarehe 12/4/2007 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo, mara baada ya kipindi cha maswali katika ukumbi Na. 432.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, ameniomba nitangaze kuwa saa tano asubuhi katika ukumbi Na. 428 kuna kikao muhimu cha kujadili Muswada wa Sheria ya Barabara, 2007, *Roads Bill* 2007 ili wajumbe waweze kumaliza kazi waliyokwishaianza. Wakati nawatambulisha vijana wa *Clouds FM*, nilisahau kutamka kwamba moja ya matunda ya *Clouds FM* ni Mheshimiwa Mbunge Amina Chifupa Mpakanjia, ahsante sana. *(Makofi)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswa wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa na Kutekeleza Masuala mbalimbali yanayohusu Mipango miji *(The Urban Planning Bill, 2006).*

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 *(The Town Planners (Registration) Bill, 2006).***

**Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi *(The Land Use Planning Bill, 2006).***

*(Majadiliano yanaendeleia)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi ya Miswada mitatu kama ilivyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nitachangia kwa kujibu hoja za Wabunge waliotupatia maoni yao kwa maandishi na kabla sijachangia napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri ambayo wametupatia. Moja kwa moja nitakwenda kwenye hoja ya Mheshimiwa Mwinchoum, Mbunge wa Kigamboni ambaye ametushauri kwamba ni muhimu sana kuandaa mpango wa kupima maeneo haraka mkoa wa Dar es Salaam kabla ujenzi holela haujaendelea.

Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia hoja hii, na napenda kumfahamisha kwamba Serikali kupitia Wizara ya Ardhi imechukua jukumu hili na tayari tumekwishaanza kupima maeneo kadhaa yakiwemo katika Wilaya ya Temeke, na Mheshimiwa Mbunge ni shahidi wetu. Vilevile tumekwishaanda mpango wa kupima pembezoni mwa jiji la Dar es Salaam ambako tutaweza kuyapanga maeneo kabla wananchi hawajaanza kujenga kiholela. Vilevile ametoa masikitiko yake kwamba wakati mwingine Halmashauri inapima ardhi lakini baadaye Wizara inakuja kuchukua na hayo maeneo bila kuwaarifu Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara inasaidiana sana na Manispaa na Halmashauri kuwezesha upimaji wa viwanja na baada ya kupimwa hugawiwa katika Halmashauri husika kama inavyofanyika. Sasa hivi tumepima viwanja Kibada, na tayari tumekwishawakabidhi Manispaa ya Temeke wavigawe. Kwa hiyo, mpango huo utaendelea, kama kuna matatizo yaliendelea tutarekebisha. Mpango wa fidia pia naona Mheshimiwa Mbunge amejaribu kutuasa kwamba tujaribu kutazama fidia izingatie mapato na vilevile iwe kwa kiwango ambacho kinakubalika.

Mheshimiwa Spika, thamani ya ardhi na mimea ya ardhi yenyewe inazingatiwa wakati ambapo uthamini unafanyika na inalingana na hatua ya maendeleo yaliyo kwenye hiyo ardhi. Kwa kushirkiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara imeweza kupata viwango vya uhakika vya kufidia mazao na mimea mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis naye pia ametoa hoja kutuasa kwamba tujaribu kutoa mafunzo kwa Wananchi ili kuepukana na maafa ya utumiaji wa ardhi. Wananchi waelewe kutumia kwa faida ya Watanzania na Serikali. Napenda kusema kwamba Muswada wa Sheria wa Matumizi Bora ya Ardhi na Mipango Miji imezingatia hilo na mafunzo yatatolewa kwa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mariam Mfaki, ambaye pia kuna Wabunge wengine wametoa michango yao kwa kuongea kuhusiana na Mji wa Manispaa ya Dodoma kutokuwa na Manispaa, ipo Manispaa isipokuwa madaraka yamekabidhiwa *CDA*. Hili ni suala la Kitaifa na kisheria, *CDA* ilipewa mamlaka ya kuendeleza Makao Makuu ya Dodoma lakini kama kuna utata unatokea hili suala kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI italitazama upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Omari Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro naye amechangia na akatuonyesha tatizo la ugawaji viwanja kwa watu zaidi ya mmoja, ile *double allocation*. Kusema kweli tatizo hili lilikuwa baya sana na limeathiri watu wengi. Sasa, hivi tatizo hili linatatuliwa kwa kuhakiki milki na kumpa haki yule anayestahili, tumefanikiwa kutoa kwa watu wengi na tutaendelea na zoezi hilo.

Vile vile ameonyesha ubomoaji wa majengo, watendaji wanasubiri mpaka jengo limeshafika juu ndio wanabomoa, hili siyo jambo la kufurahisha lakini tutalizingatia na limetokea kwa sababu mara nyingi unakuta uwezo wa kifedha, wale watendaji wa Halmashauri wanakuwa hawana wa kuweza kuwafikia katika maeneo mbalimbali kwa kutumia pikipiki na magari lakini tutazingatia ili pasitokee masuala kama hayo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwanne Mchemba ametueleza kwa kirefu na ametoa hisia zake kwamba kuna watu wamepewa hati za kijiji katika hifadhi ya misitu na kupewa fidia ndogo, wanapokuja kuondolewa wanapewa fidia ndogo. Lakini ningependa kumwambia kwamba suala hili tunazingatia sheria na fidia inatolewa kwa misingi ya sheria, nitalifafanua zaidi lakini ningeomba kwa sasa akubaliane na sisi hayo. Ametupa wazo zuri sana kuhusu kukasimu madaraka ya kusajili hati kwa mikoa ili kupunguza urasimu na Serikali ina mpango wa kuanzisha usajili katika Kanda, hilo tumeliona na kweli tunasema kwamba tutajitahidi lakini sasa usajili unafanyika katika ofisi za Kanda zilizopo Moshi, Mtwara, Dodoma, Dar es Salaam na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine tumepata kutoka kwa Mheshimiwa Charles Kajege, Mbunge wa Mwibara, anasikitika wathamini wa Wizara yetu wanapothamini viwanja *TRA* nayo inapeleka *valuer* wake ambaye haikutuamini lakini Wizara inatarajia kuandaa sheria itakayosimamia wataalam wa uthamini *(Valuers)* ambayo itawawezesha kufanya kazi yao kikamilifu na kutambuliwa na vyombo vyote wakiwemo *TRA*.

Mheshimiwa Janet Kahama, tunashukuru kwa ushauri wake mzuri ambao ameonyesha maeneo ya wazi pamoja na maeneo ya bustani yamevamiwa na kupimwa na kugawa na kujengwa viwanja.

Mheshimiwa Spika, hili tumelizingatia sana, tumeanza kuorodhesha maeneo yote ya wazi nchi nzima pale ambapo yalitolewa kwa makosa yatarekebishwa na pale ambako yalitolewa kwa ubabe au kwa kuvunja sheria, sheria itachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, naye pia ameongolea wakati wa uboreshaji wa maeneo yaliyojengwa kiholela, miundombinu ikiwekwa anauliza kwamba wahanga

watalipwa kiasi gani iwapo ni sehemu tu ya nyumba imeathirika? Napenda kumfahamisha kwamba fidia itazingatia sheria ya Ardhi namba 4 na sheria ya utoaji wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Madgalena Sakaya, ametushauri vizuri sana, Serikali itatekeleza haraka mpango wa kupima ardhi vijijini pamoja na maeneo yanayomilikiwa na wananchi ili wapate hatimiliki na ili ardhi iwe na thamani. Tunakubaliana naye kabisa na tumesema hata nilipokuwa najibu maswali asubuhi kwamba Serikali itapima ardhi vijijini na kumilikisha wananchi wapate hatimiliki za kimila kulingana na bajeti itakavyokwenda. Lakini tunategemea tuliweka mpango wa miaka minne kwamba ifikapo mwaka 2008 tungekuwa tumemaliza kupima vijiji vyote japo kumetokea dharura hapa na pale ikatuchelewesha lakini Serikali imekuwa makini kabisa kwa suala hili na tutazingatia kwa uwezekano wa bajeti itakavyopatikana. *(Makofi)*

Pia ameonyesha kwamba gharama za upimaji wa maeneo mijini na vijijini ni kubwa kwa wananchi kumudu na vile vile ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanamiliki ardhi yenye hati, tunakubaliana na yeye na tumepunguza gharama kutokana na utaalam na gharama ya kupima vijiji imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, ametushauri tuangalie upya majengo yaliyojengwa kiholela hasa Dar es Salaam na hili nimeshalisema na kazi ya kurasimisha ujenzi holela inaandaliwa na maoni hayo yatazingatiwa. Ningependa pia kumjibu Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, ameonyesha kwamba wapimaji wa ardhi wa Wilaya ya Lindi au Mkoa kwa ujumla ni wachache na inachelewesha ujenzi, tutaihamasisha Halmashauri ya Wilaya ya Lindi na Miji kuajiri wapimaji ardhi zaidi na sisi tuko tayari kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwa Mheshimiwa Mwanne Mchemba ambaye amependa zaidi kuongelea kuhusiana na fidia, nadhani hili nimeshalijibu.

Ningependa sasa kuongelea kuhusu Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro ameongea kwa masikitiko kabisa kuhusiana na hekta 94,000 ambazo ni maeneo ya vijiji yamechukuliwa na wageni watalii kwa ajili ya uelewa mdogo wa wananchi. Kisheria wawekezaji hawaruhusiwi kuwadanganya wananchi na kuchukua maeneo. Mwekezaji anapokuja anapitia *TIC* na kule kuna sheria ambayo imewekwa na Wizara inawakabidhi *TIC* maeneo na *TIC* inawapa wawekezaji kutokana na watakavyohitaji kwa mfano mtu anahitaji kwa miaka 25, 33, 99 lakini kutokana na atakavyohitaji pamoja na mbia ambaye pia atapenda kufanya awe mwekezaji na *TIC* inatoa hati inaitwa *Derivative Right of Occupancy.*

Kwa hiyo, utaratibu huo ndio ulipaswa kwa wale watalii waliokuja Ngorongoro lakini kama waliingia kimwamba hayo ni makosa. Vile vile kuna ardhi za aina tatu, kuna ardhi za jumla, ardhi ya hifadhi na ardhi ya kijiji, kama ni ardhi ya jumla hiyo sisi tunahusika kuja kuifuatilia lakini kama ni ardhi ya hifadhi tungeomba Mamlaka ya

Hifadhi walisimamie na kama ni ardhi ya kijiji Serikali ya kijiji inaweza ikalitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa nimebakia na dakika tatu naomba nigusie kidogo kabisa, Mheshimiwa Charles Keenja aliongelea kuhusu maeneo ya Dar es Salaam ili kuondoa *squatters*. Kwanza, kama tulivyosema maeneo ya *squatters* ambayo yako kwenye *long standing occupation* hayatavunjwa isipokuwa tutaboresha na tuna mpango wa kuyaboresha yale yaliyopo kwa mpango ambao tumeuongolea sana kupima maeneo ya pembezoni kama mpango uliopo katika Jimbo la Mheshimiwa Charles Keenja, kule Mbezi Luguruni ambako sasa hivi tunahakiki na hatimaye tutapima kama kituo cha mfano ili kuboresha maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, ningependa kugusia kwamba ametulinganisha na Botswana na *South Africa* kwamba tungepaswa tuweke barabara. Miundombinu tutajitahidi lakini ningependa kumwonyesha kwamba gharama ni kubwa sana, kwa sasa hivi tunajitahidi, katika viwanja 33,000 tulivyopima katika Jiji la Dar es Salaam tumechonga barabara japo ni za moramu lakini Serikali imezingatia hilo. Ningependa pia nimkumbushe Mheshimiwa Charles Keenja kwamba tangu mwaka 1998 mpaka 2003 vilipimwa viwanja 76,000 tu katika Tanganyika au Tanzania Bara. Lakini kwa mwaka 2003/2004 mpaka sasa hivi vimepimwa viwanja 33,000, hiyo ni dhahiri kwamba Serikali inafanya juhudi kubwa sana katika upimaji wa viwanja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kumalizia kwamba tunashukuru kwamba Mheshimiwa Charles Keenja amesema atasaidiana na sisi ili kuyatatua matatizo ya Mkoa wa Dar es Salaam na kwa vile ana uzoefu mkubwa hilo tutapenda tulizingatie. Kwa kumalizia naongelea kuhusu Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka ambaye amemalizia *double allocation* natumaini nimeshaliongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, nashukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaanza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa, ningependa niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maneno na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi kwa kuwataja majina.

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maneno ni Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Gosbert Blandesi, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Abdalkarim Hassan Shah, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Ephram Madeje pamoja na Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa William Ngeleja na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia kwa wingi katika Muswada huu, Miswada hii yote mitatu inatokana na hali halisi kwamba imezaliwa baada ya kupitishwa kwa sera ya Makazi ya mwaka 1995, Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, Sheria Namba 2 ya mwaka 2000 iliyoanzisha Mahakama za Ardhi na Nyumba, lakini pia sera ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala kubwa ambalo limeweza kuleta Miswada hii mitatu ni kutokana na matatizo mengi na upungufu mwingi ambao umekuwa ukijitokeza katika masuala ya ardhi. Tulifikiri sisi Serikali kwamba kuna umuhimu wa kufanya mabadiliko makubwa na kutunga sheria mbalimbali ambazo zinaweza zikasaidia sana katika masuala ya ardhi na kuondoa migogoro na migongano ambayo imekuwa ikijitokeza. Wakati wa semina yangu juzi nilijaribu kutoa maelezo mafupi ya jinsi migogoro hii ilivyoanza na nilianza kwa kutoa takwimu za kuonyesha kwamba Tanzania yote tangu tupate Uhuru ina ukubwa wa kilometa za mraba 949,000 na wakati tukipata Uhuru, Watanzania tulikuwa kati ya 8,000,000 na 9,000,000 na mifugo ilikuwa pia ni michache kwa wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi karibu miaka arobaini na kitu imepita ukubwa wa ardhi umekuwa ni huo huo wa kilometa za mraba 949,000 na idadi ya watu kwa sasa hivi ni zaidi ya 36,000,000, idadi ya mifugo ni zaidi ya 35,000,000 lakini pia hata *rate* ya kuongezeka kwa idadi ya binadamu ni karibu 2.9% wakati idadi ya mifugo nayo imekuwa ikiongezeka kwa asilimia 2.7, kwa takwimu hizi ni dhahiri kwamba bila kuwa na mipango madhubuti katika masuala ya matumizi ya ardhi, migogoro itaendelea kutukumba katika nchi yetu na ndio maana ya umuhimu wa kuleta Miswada hii yote mitatu kwa pamoja katika kuhakikisha kwamba masuala ya migogoro na masuala ya ardhi yanazingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na waliochangia kwa maneno, maoni yao na maelekezo yao sisi yote tumeyazingatia kikamilifu sana. Wapo waliochangia ndani ya Muswada wenyewe, wapo waliochangia kwa masuala ya jumla wakitoa mapendekezo mbalimbali ambayo tunaamini kadri tutakavyokuwa tunaenda tutaendelea kuyazingatia kwa sababu mwanzo wa kupitishwa sheria hizi tatu ndio chanzo kikubwa pia cha kuleta sheria zingine ikiwa ni pamoja na sheria ya nyumba na sheria nyingine za upimaji wa ramani katika nchi hii. Lakini tunaamini baada ya kupitishwa kwa sheria namba 4 na namba 5 na

sheria namba 2 na sheria nyingine ambazo zilitangulia pamoja na sera ya ardhi na sera ya maendeleo ya makazi tunaamini kutungwa kwa sheria hizi tatu kutaleta manufaa makubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Napenda niwatoe wasiwasi ambao Waheshimiwa Wabunge wameuonyesha kwamba kupitishwa kwa sheria hizi kutaweza kuleta madhara makubwa kwa wananchi ambao tayari wanamiliki zao. Nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba wale wote ambao wana ardhi zao wanatambuliwa kwa sheria ya ardhi ya vijiji namba tano ya mwaka 1999 kwa hiyo, hawawezi kuathiriwa na kupitishwa kwa Miswada hii mitatu ambayo tumeileta, Miswada hii lengo lake ni kuboresha na kuhakikisha kwamba sheria zinazingatiwa katika masuala ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda pia nisisitize kwamba katika sera ya ardhi ya mwaka 1995 inasisitiza ardhi itatolewa kwa Watanzania tu na hii inasisitiza kwamba ardhi ni mali. Kwa maana hiyo mali kama ardhi itaendelea kutambuliwa kwa kila mmoja lakini pia chini ya sheria namba 5 ya mwaka 1999 inatambua uhalali wa milki za kimila. Kwamba ardhi inayomilikiwa ya kimila inayomilikiwa na Mheshimiwa John Cheyo kule Bariadi inatambuliwa na haiwezi ikachukuliwa na mtu yeyote na kama atatokea mtu wa kuichukua maana yake lazima aachie pesa kwa mujibu wa sheria na nilisema kipengele namba 3 (g) cha sheria namba tano ya mwaka 1999 kinazingatia hili fungu namba 13 lakini ni katika sheria zote. Kwa hiyo, msisitizo wa kuleta Miswada hii ni katika kuwawekea mazingira mazuri kwa wananchi na hasa wanyonge ambao wamekuwa wakidhulumiwa kwa kiasi kikubwa katika masuala ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kabisa Muswada huu baada ya kuupitisha na ndio maana pale jana watu walikuwa wamejitokeza watatu tu wa kuchangia mpaka ulipoweka changamoto, hii ni kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walielewa vizuri semina zilizotangulia na hata wadau tulipokuwa tukizungumza nao tarehe 16 Januari, 2007 walisema Muswada huu ulitakiwa uletwe miaka 10 iliyopita hata haya matatizo yasingekuwepo. *(Makofi)*

Mheshimia Spika, kwa hiyo, ninaamini kabisa na ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote waupitishe Muswada huu bila kuuchelewesha ili Mheshimiwa Rais akausaini tuweze kufanya kazi katika kuleta mabadiliko ya kweli katika masuala ya ardhi. Muswada huu kwa ujumla pia umepeleka madaraka zaidi kwa wananchi na nitajaribu kuvisoma baadhi ya vipengele ambavyo vinasisitiza hili, kwa sababu *Cap. No. 378* na sheria namba 3 ya mwaka 1984 ilikuwa imetoa madaraka kwa Waziri anayehusika na ardhi, sasa hivi Waziri anayehusika na ardhi ni msimamizi wa sera tu. Kwa hiyo, masuala yote yanarudi kwenye Tawala za Mikoa ambao ndio wasimamizi wa kweli wa masuala ya ardhi na katika masuala ya ardhi katika Muswada mzima huu umesisitiza pia kwamba akinamama wana haki ya kupata hati na kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ni masuala ya msingi lakini pia watu wenye ulemavu na kadhalika wote wamezingatiwa katika suala la kupata hati katika masuala ya ardhi. Hivyo, Muswada huu kama ambavyo wamekuwa wakichangia watu wengi

ulitakiwa uje miaka 20 iliyopita na inawezekana migogoro hii ambayo tunapambana nayo ingekuwa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Balozi Dr. Getruda Mongella na Mheshimiwa Kaika Telele, wamezungumzia kuhusu elimu itolewe na hili nakubaliana nalo kabisa kwamba kuna umuhimu wa kutolewa elimu ya kutosha kwa wananchi wetu na hii ni pamoja na sheria namba 4 na namba 5 za ardhi ambazo ni muhimu ili wananchi wasiweze kudhulumiwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi amezungumzia juu ya sheria ya upimaji wa ramani, tumezingatia ushauri huu kwamba sasa baada ya Muswada huu kupitishwa tutaanza kuandaa sera ya upimaji wa ramani ili nayo iweze kusaidia katika masuala haya. Lakini pia amezungumzia juu ya sekta ndogo ya nyumba itungiwe sheria, hili linawezekana kwa sababu mara baada ya kupitishwa sera ya makazi ya mwaka 2002 bado tunaamini kwamba sheria ya nyumba inaweza ikatungiwa sheria ili hata yale masuala ya Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, aliyoyazungumza ya mambo ya *mortgage system* yaweze kuzingatiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia amezungumzia Halmashauri ziwezeshwe vya kutosha ili kumudu majukumu yao, hili ni suala la Tawala za Mikoa, nina uhakika Wizara inayohusika italizingatia. Katika ushauri uliotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo na Ardhi wamesema bajeti iongezwe, mimi nafikiri Waziri wa Fedha atakuwa amesikia hili kwamba Bajeti ya Wizara ya Ardhi inatakiwa iongezwe kwa sababu siku zote tumekuwa tukizungumza ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Sasa katika bajeti iliyopita Wizara ya Ardhi ilikuwa ya mwisho kasoro mbili katika Bajeti. Sasa kwa sababu hili limeweza kujulikana kwa Waheshimiwa Wabunge na Kamati husika imehusika, mimi siwezi kulisemea sana lakini nafikiri Serikali tumelizingatia kwamba inawezekana katika Bajeti ya mwaka huu Wizara ya Ardhi itapewa Bajeti nzuri itakayoweza kuhimili haya masuala muhimu ambayo ni muhimu kwa wananchi kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kambi ya Upinzani wamezungumzia Wajumbe wengi wa Tume wateuliwe kutoka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na sifa zitajwe, hili bahati nzuri limefafanuliwa vizuri katika ukurasa wa 9(6) sura 1(b) na 10 imezingatia uwakilishi wa TAMISEMI ikiwa ni pamoja na sekta nyingine muhimu. Kwa hiyo, hili limezingatiwa, lakini pia Mheshimiwa Abdulkarim Shah, hili alilizungumzia.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, amezungumzia kuhusu Muswada hauonyeshi muda au kipindi ambacho Mjumbe wa Tume anatakiwa kutumika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, hili litawekwa kwenye Kanuni lakini hili pia limezingatiwa kwenye Ibara ya 7 (2). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia linapojitokeza suala la *conflict of interest* Muswada huo upo kimya, nini kifanyike, katika Ibara ya 9 inazingatia suala la migongano ya maswali, *conflict of interest* na ipo kwenye ukurasa wa 11, anasema Mtendaji Mkuu wa Tume

ateuliwe kutokana na ufahamu wake wa Serikali za Mitaa. Kifungu namba 10(2), Mtendaji Mkuu wa Tume huteuliwa na Mheshimiwa Rais na Rais anachaguliwa na watu wote akiwemo Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini pia hili limezingatiwa katika Ibara ya 10(3) nina amini atakayeteuliwa atakuwa anafaa kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka za Ardhi za Wilaya zisipewe uwezo wa kubadili matumizi ya Ardhi ya Vijiji, hili pia nalo limezingatiwa katika Halmashauri katika ukurasa wa 18, Ibara ya 21, ninajaribu kutoa ufafanuzi huu ili kusudi Waheshimiwa Wabunge waweze kupitia hii Miswada na katika Ibara husika zinazohusika. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Kabwe Zitto, amesema Tume isiwe na mamlaka ya upangaji wa matumizi ya ardhi, Ibara ya 19(2) majukumu ya Tume ni kuratibu na kuweka muundo wa mipango ya matumizi ya ardhi Kitaifa, hili lipo katika *page* namba 16. Msajili wa bodi ateuliwe kutokana na uelewa wake katika maadili ya taaluma, hili limezingatiwa katika maadili ya taaluma, limezingatiwa katika Ibara ya 7 (1) (a), *schedule of amendments* imezingatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wataalam wa mipango miji kuruhusiwa kutoza ada itakuwa ni mzigo kwa Watanzania, wataalam wa mipango miji walio katika Utumishi wa Umma watatoza ada kwa huduma za umma watakazotoa wenyewe. Kwa hiyo, kwa ujumla mawazo mazuri yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani, tumeyazingatia kwa sababu yako mengi tu mazuri yametolewa ushauri na mengine tayari tumeyajumuisha katika Miswada yetu katika *amendment,* kwa hiyo, nawashukuru sana na mimi nasema mawazo yenu ni mazuri, mkiendelea hivi ni kweli mtakuwa mkitekeleza vizuri sera za Chama cha Mapinduzi.

Pia Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah na Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe pamoja na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, wamezungumzia kuhusu hali halisi ya ulipaji wa fidia katika masuala ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba katika ardhi yoyote itakayochukuliwa, Sheria ya Ardhi namba 4 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 ya mwaka 1999 hazijafutwa. Kwa hiyo, kipengele namba 3 (g) na kipengele 3(g)(13) katika sheria hizo vitaendelea kuzingatiwa na ninataka nithibitishe hapa kwa ajili ya rikodi kwamba ulipaji wa fidia kwa mujibu wa sheria hizo ambazo nimezitaja utaendana kwanza na bei ya soko, ardhi na mazao yaliyopo. Hata kama ardhi ni tupu lazima ilipiwe fidia kwa sababu mwenye ardhi alitumika kufyeka, kama ni nyoka aliwafukuza, kama ni fisi aliwafukuza, ile ni thamani yake lakini mazao yaliyopo iwe mnazi, ziwe karanga yale yote yanalipiwa kufidia lakini pia usumbufu *(disturbance allowance)* ni kama anazolipwa mfanyakazi akihamishwa kutoka mahali fulani. Lazima yule mwanakijiji naye alipwe fidia ya usumbufu lakini pia kupoteza faida na manufaa kwa sababu ile ilikuwa ardhi yake, aliachiwa na babu yake, wamehangaika miaka yote

kwa hiyo, ni lazima kile nacho kipengele kipigiwe hesabu zake kwa ajili ya kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri, kwa sababu mhusika atahamishwa kutoka mahali fulani kwenda mahali pengine lazima pia alipiwe usafiri wa kutoka mahali hapo kwenda mahali anapohamia hii ndio sheria. Lakini kodi ya pango kwa miaka mitatu inazungumza hivyo kwa sababu kama yule mtu atahamishwa alikuwa na nyumba zake, zile nyumba zitabomolewa ziwe za matembe, ziwe na nini, ni nyumba zake na ndizo alikuwa anaishi, lazima alipwe fidia ya pango kwa miaka mitatu wakati atakapokuwa anaandaa nyumba zake.

Kwa hiyo, sheria hii inaonyesha ugumu wa namna gani watu watakavyokuwa wanahamishwa, yaani tumeweka vipengele vigumu kusudi watu wasihamishwe hamishwe na mimi nilifikiri hii sheria ilitakiwa ije miaka 20 iliyopita na Waheshimiwa Wabunge mnakubaliana na hilo.

Mheshimiwa Spika, pia umri wa zao husika ni lazima upigiwe mahesabu na kuangaliwa huu umri una miaka mingapi na; je, angepata faidia kiasi gani? Na ndio maana katika Wizara zinazohusika kuna *valuers* lakini kulipwa ni lazima pia alipwe kwa wakati ikishafanyika *evaluation* ni lazima alipwe ndani ya miezi sita, asipolipwa ndani ya miezi sita lazima pia ifanyike tathmini nyingine kulingana na wakati ule.

Kwa hiyo, Miswada hii ina-*support* ile sheria ya ardhi namba 4 na namba 5 ambayo imekuwa ni kama kuweka msisitizo katika kujenga haki za watu. Wakati nikitoa semina hapa nilieleza ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwamba hata mahali panapojengwa shule ya sekondari, hata panapojengwa hospitali, thamani ya hospitali ile au ya shule ile itajumuisha pamoja na thamani ya yule mwanakijiji aliyekuwa na shamba lile kumlipa fidia. Hii ndio sheria inavyosema na hii sheria haikutungwa na John Magufuli, sheria ni namba 4 ya mwaka 1999 kipengele namba 3(g) na sheria namba 5 ya mwaka 1999 3(g)(13) na sisi wote hapa tumeapa kulinda sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kitu kikubwa kinachotakiwa ni wananchi kupata elimu ya kutosha katika kuhakikisha kwamba mambo yao yanapatikana kwa haki. Lakini katika sheria hizi pia sheria namba 2 ya mwaka 2002 inaruhusu wanakijiji kushtaki na anayeshtakiwa ni mtu yeyote ukiona haki yako haijatendeka, hata katika sheria namba 47 ya utoaji ardhi ya mwaka 1967 inasisitiza pia ulipaji wa fidia, kwa hiyo, kila utakapogusa sheria ya ardhi lazima fidia inazungumzwa lakini kweli nikubali kwamba watu wetu vijijini wamekuwa wengi wakionewa kwa sababu wamekuwa hawazijui hizi sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anaambiwa ondoka hapa, nenda hapa tunajenga huduma hii na anaondoka na shamba lake aliliendeleza vizuri. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sisi Waheshimiwa Wabunge wote kuwaelimisha wananchi wetu kwamba sheria hizi zipo na pia tuchukue hizi *Hansard* ambazo zinatolewa leo na Serikali tuwapelekee wanakijiji waweze kudai haki zao kila mahali patakapokuwa panastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Peter Serukamba, amezungumzia Waziri na Mkurugenzi wa Makazi, wana madaraka makubwa mno. Sasa nilikuwa najaribu kuangalia katika Muswada huu ni mahali gani Waziri amepewa madaraka makubwa mno kwa sababu ukichukua *Cap. No. 378* na Sheria Na. 3 ya mwaka 1984, zile ndizo zilikuwa zinampa Waziri kwa kila mahali, lakini sasa hivi haya madaraka yote tumeyapeleka kwenye Tawala za Mikoa, kwenye Serikali za Vijiji na kadhalika. Nilitaka tu nimjulishe Mheshimiwa Peter Serukamba, kwamba Waziri na Mkurugenzi wamepewa madaraka ya kusimamia Sera, Sheria na viwango lakini wajibu wa kubuni na kupanga na kutengeneza mipango ni wa Serikali za Mitaa na hii imefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 7, ukurasa wa 87 na ninaomba kwa ruhusa yako ninukuu kidogo katika kumkumbusha Mheshimiwa Peter Serukamba. *(Makofi)*

Inasema "…. *every City Council, Municipal Council, Town Council, District Council and Township Authority shall each become a planning authority in respect of its area of jurisdictions."*

Namba 2 inasema "… *for the avoidance of doubts establishment confirms of the status and expansions of the boundaries of Local Government Authorities mentioned under sub-section 1, shall be made by the Minister responsible for Local Government who shall have the regards on matters prescribed in the fifth schedule."*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inazungumziwa tu mambo ya Tawala za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua Muswada huu usiangaliwe kwamba aliyepo Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Naibu wake ni Mheshimiwa John Magufuli na Mheshimiwa Rita Mlaki, lakini kesho anaweza akawepo Mheshimiwa Peter Serukamba, kesho anaweza akawepo Mheshimiwa John Cheyo na kadhalika. Tunachofanya hapa ni kuhakikisha kwamba Sheria hizi zinawagusa wananchi ambao ndiyo lengo letu kubwa kuwatetea. Kwa hiyo, si kweli kwamba Sheria hii imempa mamlaka sana Waziri lakini Waziri ana Mamlaka ya Sera ambazo ni katika Sheria zote na bahati nzuri Waziri anayetajwa hapa ni Waziri anayehusika na Tawala za Mikoa na haya yamefafanuliwa vizuri katika ukurasa wa 87, ningemwomba Mheshimiwa Peter Serukamba, akasome hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abdulkarim Shah, amezungumzia kukosekana kwa uhakiki wa milki za ardhi kutokana na mipango ya ardhi lakini pia amesema maeneo yenye kumbukumbu za historia, haya pia yamefafanuliwa vizuri katika ukurasa wa 106 katika Ibara ya 51 hadi 52, zote zinazungumzia maeneo ya kihistoria na masuala ya *environment* ambayo Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, amekuwa akiyasisitiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kabwe Zitto, amezungumzia juu ya *Town Authorities* zisimamiwe na *Urban Planning Bill, Trading Centres* ziwe chini ya *District Authorities*. Ushauri huu tumeuzingatia ni kwa bahati mbaya tu tuliusahau lakini wakati tutakapofikia katika kufanya hizi *amendment* tumeamua kuweka *amendment* ya maneno yafuatayo katika Ibara ya 33 ya *Land Use Planning Bill,* irekebishwe kwa kuongezwa Ibara ya 33 (5)

ambayo itasomeka kama ifuatavyo; *"... for the purpose of this section, the Village Land Use Plan shall include plan for minor settlements or trading centres reffered to in the sixth schedule to this Act."*

Mheshimiwa Spika, hii itasaidia katika miji midogo midogo inayokua kama Kibaigwa na kadhalika na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge katika Majimbo yetu kuna miji hiyo midogo midogo inayokua, tusipoweka hii *amendment* itapunguza ukuaji wa hii miji. Kwa hili tumelizingatia kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Gosbert Blandes, amezungumza kwamba Muswada hauonyeshi namna ya kumpata mwenye ardhi, isipopatikana au anapokataa ardhi yake kutwaliwa. Hili limefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 39 (1), imeeleza kufuata taratibu zilizowekwa chini ya Sheria ya Kutwaa Ardhi. *(Makofi)*

Lakini pia Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, amezungumzia mipango mizuri kwa vijiji. Hili pia limefafanuliwa vizuri na ushauri umezingatiwa katika Ibara ya 9 hadi ibara ya 27.

Suala la Mheshimiwa Ephraim Madeje, kuhusu *CDA*. *CDA* ilianzishwa kwa Sheria nyingine, kwa hiyo, ningependa kumshauri Mheshimiwa Ephrahim Madeje, ajaribu kuwasiliana na ofisi inayohusika na *CDA* ili kuona ni kwa namna gani nzuri inaweza ikawekwa katika kusaidia Manispaa ya Dodoma, nayo iweze kushiriki katika masuala haya, lakini ushauri wake mwingine tumeuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mengi yamezungumzwa, kwa mfano, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, amezungumzia kuhusu upangaji wa miji hauzingatii hali ya uchumi wa wananchi, miji ni lazima ipangwe kwa viwango ambavyo vitawezesha maisha salama kwa wananchi wote lakini pia ushauri wake ambao ameutoa wa kuhakikisha kwamba wananchi wasifukuzwe katika maeneo ya mijini tumeuzingatia kwa sababu unalinda maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Clemence Lyamba, amezungumza kutangaza miji midogo na ucheleweshaji wa utelekezaji wake, suala hili lipo kwenye TAMISEMI lakini pia limefafanuliwa katika Ibara ya 7 (2).

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, amezungumzia juu ya matumizi ya ardhi yazingatie *environment impact,* haya yote yamefafanuliwa katika ukurasa wa 106 lakini pia yamefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 52(1).

Mheshimiwa Herbert Mntangi, amezungumzia juu ya kanuni za urefu na upana wa barabara. Hizi barabara zinazozungumziwa ni zile zinazohusika na maeneo yale ya upimaji lakini hata hivyo kwa sababu hili lipo ndani ya *regulations* nina uhakika Serikali ni moja, Waziri anayehusika na kupitisha hizi Kanuni watashauriana na Waziri anayehusika na masuala ya barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Keenja, bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri lakini mipango ya matumizi ya ardhi imefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 7 (1) na (b). Lakini katika suala la Dar es Salaam mahali ambapo kuna ujenzi wa holela kuna hatua mbalimbali ambazo zimekuwa zikichukuliwa ikiwa ni pamoja na kutambua maeneo ya makazi ambayo hayajaendelezwa kikamilifu mpaka sasa hivi zaidi ya milki za watu 230,000 zimeshatambuliwa na leseni za makazi zaidi ya 67,000 zimeshatolewa kwa wakazi hao. Hii yote ni katika kujali na kutambua haki za hawa watu ambao wamejenga kwenye *unplanned areas* zaidi ya 75% kwa Dar es Salaam na kwenye miji mingine ni zaidi 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Juma Killimbah, amezungumza kwamba Muswada huonyeshi ambapo mdau anashirikishwa katika upangaji wa matumizi ya ardhi. Nilipojaribu kupitia katika Muswada huu tumeona suala la ushirikishwaji wa wadau umezingatiwa katika Ibara ya 6(1) ambayo ipo kwenye ukurasa wa 9. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Cheyo, amezungumzia Muswada wa Mipango ya Ardhi utawaboresheaje maisha ya wananchi? Hili limefafanuliwa vizuri katika Ibara ya 3 ambayo imetoa dira ya maboresho ya maisha ya wananchi. Lakini pia katika *Policy Frame Work Part II page No. 7, Land Use Planning* imeelezea vizuri kuhusu ni kwa namna gani wananchi wataweza kufaidika na huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, viwango vya adhabu ni vikubwa. Viwango vimezingatia athari zitakazotokea na ukiukwaji wa mipango ya matumizi ya ardhi lakini kwa wale ambao tayari wapo pale, wenye mashamba yao wale hawawezi kuwa *disturbed* kwa maana nyingine Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 inawalinda, Muswada huu ukweli ni kwamba umeletwa kwa ajili ya kuwalinda wale watu kwa sababu kuna Sheria ya Ardhi namba 4 inawalinda, kuna Sheria ya Ardhi ya Vijiji namba 5 inawalinda ambayo inatambua kazi ya wakazi asilia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Muswada huo ni katika kuendelea kuwalinda hao watu, kama patatokea kwa njia yoyote ile kwamba yule mtu labda panahitaji kupitishwa barabara na kadhalika ni lazima fidia sasa ndipo inalipwa kwa mujibu wa sheria ambazo zimezitaja hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa ujumla Miswada hii yote ni kulinda maslahi ya wananchi na hasa wananchi waliokuwa wanyonge ambao kwa siku zote za nyuma wamekuwa wakionewa. Nina mifano ambayo ni halisi kwa mfano kwenye viwanja, viwanja vinapopimwa pamekuwa na matatizo kwa mfano ukishaenda kuomba *building permit* ambayo nayo imekuwa ni tatizo kwenye Halmashauri zetu, ukishaomba wapo watu ambao wamekuja kulalamika pale Wizarani kwamba anapokwenda kuomba anaambiwa subiri, akishasubiri anatafutwa mtu mwenye pesa anakwenda kujenga usiku na mchana. Baadaye ukisharudi na kuuliza kwenye kiwanja changu mbona anajenga mtu? Unaambiwa kwa sababu kuna mtu, kwa hiyo, kiwanja hiki kina migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika matangazo tuliyoyatoa tumesema kwamba kwa mujibu wa kifungu namba 175 cha Sheria mtu ukijenga kwenye kiwanja

ambacho si chako unatakiwa ubomoe jengo lako, ubomoe jengo lako wewe uliyemfuata kwa sababu ni kweli wapo watu walioshindwa kuendeleza viwanja kwa sababu viwanja vyao vilivamiwa na watu wenye pesa. Kwa hiyo, ukienda ukavamia kiwanja cha mtu kwa mujibu wa kifungu cha 175 cha Sheria ya Ardhi unatakiwa ubomoe au ukubaliane naye kwa mujibu wa sheria umlipe pesa kwa sababu ardhi ni mali, hii ndiyo sheria.

Kwa hiyo, ninavyofahamu ni kwamba pamekuwa na matatizo mengi katika uelewa wa sheria lakini Wizara yangu itaendelea kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi na ningewaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu ili haki zao katika masuala ya ardhi waweze kuzipata kwa ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, amezungumza kwamba mipango izingatie hali halisi ya ndani. Haya yote yamefafanuliwa na kuzingatiwa katika Ibara ya 31(4), jedwali namba 2 linazungumzia hata *traditions* zinazotakwa kufuatwa hata mila na desturi zimefafanuliwa pia katika Ibara ya 33 na Jedwali namba 3 linazingatia haya yote. Kwa hiyo, Muswada huu na kwa vile umefanyiwa kazi kwa muda mrefu, na umefanyiwa kazi kwa kushirikisha wadau wote wa kila aina, nigewaomba sana Waheshimiwa Wabunge tuupitishe haraka ili kweli haki za wananchi wetu ziweze kuthaminiwa na kutekelezwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninajua muda wangu unakwenda kwa haraka haraka lakini ninafahamu mengine mengi yamezungumzwa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, nikienda tu kwa haraka haraka kwa wale waliochangia kwa maneno kwa mfano Kamati ya Kilimo imeelezea ni kwa namna gani *Public Hearing* ilivyofanyika tarehe 16 Januari, 2007 na wananchi wote waliohudhuria pale Karimjee walisema kwamba Muswada huu ulitakiwa uje miaka 10 iliyopita na mimi nakubaliana nao na nina uhakika hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na hao wadau wengine.

Lakini pia maoni ya Kamati ya Kilimo tumeyazingatia na bahati nzuri napenda niipongeze sana Kamati ya Kilimo chini ya Mheshimiwa Gideon Cheyo, kwa ushirikiano mkubwa na ushauri wao mkubwa sana ambao wamekuwa wakiutoa katika hii. Masuala yao mengi katika sisi Serikali hatukuwa *rigid* na tumefanya *amendment* na ndiyo maana kuna *schedule of amendments* tumezileta hapa, hizi zote zimezingatia wadau, Kamati na zimezingatia maoni ya wananchi wengi wakiwemo *ALAT* katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani pia imetoa shukrani na mimi naipa shukrani kweli, leo ni kwa mara ya kwanza naipa shukrani kweli wamefanya kazi nzuri sana. Kama nilivyosema tukienda hivi masuala ya ardhi yatamaliza mgogoro, kwa hiyo, ushauri wao mwingi ume-*reflect* hivi na hapa kweli ndipo tunafanya kazi kwa pamoja katika kuleta manufaa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Peter Serukamba, nimetoa ufafanuzi unaohusika lakini pia kwa maeneo ambayo tayari yameshapimwa vibaya tutaendelea kutumia zile taratibu ambazo tumeanza kuzifanya kwa Dar es Salaam kwa kutambua maeneo ambayo yamepimwa

vibaya kwa sababu katika Tanzania  kati ya 70% na 75% ya miji yetu imejengwa kwenye *unplanned areas.* Kwa hiyo, tutaendelea kuyatambua ili kusudi tusilete *disturbances* kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kabwe Zitto, naye amepongeza na amezungumza mengi, ushauri mwingi kama nilivyosema baadhi ya ushauri wake unaohusu maendeleo ya *settlement* tumeuzingatia. Mheshimiwa Gosbert Blandes, naye amezungumza mengi na ambayo tayari nimeshayajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia limejitokeza suala la kazi ya Bodi hii ambayo inasimamia. Bodi kwa ujumla ni suala dogo sana kwa sababu inasimamia *almost 2%* tu ya ardhi. Sehemu nyingine zote za maamuzi ya ardhi zitakuwa zinashughulikiwa kule vijijini na suala zima la ardhi sera tu ndizo zitakuwa zinasimamiwa na Wizara husika lakini mambo mengine yote yatakuwa yanafanywa na Halmashauri na Vijiji vinavyohusika na Sheria zitazingatiwa katika kuhakikisha kwamba mengi haya yanafanyika.

Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, amezungumza hivyo,  Mheshimiwa Abdulkarim Shah naye amezungumzia kuhusu matatizo ya Mafia, ninamwomba Mheshimiwa huyu kwamba Muswada huu upitishwe ili masuala ambayo yamekuwa yakijitokeza ya migogoro yaweze kutatuliwa kwani lengo letu ni kutatua migogoro na ndiyo maana nilieleza kwamba migogoro imekuwa ni mingi hivyo bila kuiundia Sheria hatuwezi tukafanya kazi. Ndiyo maana pia utaona katika Sheria hii wanamipango miji ambao wapo zaidi ya 700 katika nchi hii walikuwa hawana Sheria yoyote inayowabana, walikuwa wanaamua kufanya chochote na hakuna Sheria iliyokuwa inawabana.

Kwa mujibu wa Sheria hii ya *Planners Registration Bill* inawapa watu, kwa mfano, atakayejifanya Bwana Mipango Miji kufanya kazi ya Bwana Mipango Miji anaweza akafungwa jela hata miaka mitano. Lakini pia mtu mwingine anaweza akafungwa miaka miwili kama atashindwa kutimiza zile *conduct* zake, tunaamini kwa njia hii itaweza kusaidia hawa watu sasa kuanza ku-*regulate* Sheria na Miji yetu kuanza kupimwa katika kipindi kizuri na kwa kufuata misingi ya Sheria zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ephraim Madege, amezungumzia mengi lakini amepongeza kuhusu sheria shirikishi, kilio chake ni kilio cha Dodoma lakini ninachotaka kumweleza ni kwamba Sheria hii kwa sababu ni sheria ya Serikali itahusisha pia hata *CDA* na kwamba itatakiwa iifuate, siyo kwamba itakapofika hapa Dodoma basi hii sheria haitafuatwa. Sheria hizi ambazo zinapitishwa tatu kwa sababu ni Sheria Kuu ni lazima pia hata *CDA* itazifuata, sasa katika masuala mengine ya kubadilisha mamlaka ya *CDA* hiyo *CDA* ilianzishwa kwa mujibu wa sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa jina sahihi ni Madeje si Madege lakini Madeje ni watani wa wasukuma kwa hiyo Madeje na Madege ni yale yale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, ameipongeza sana Serikali kwa kupima sana vijiji vyao 101. Kama nilivyosema leo hadi sasa hivi kuna vijiji 1,616 vimepimwa

na katika Mkoa wa Mbeya vijiji vyote vimemalizwa. Katika Mkoa wa Kigoma tupo kwenye Wilaya ya Kasulu wanamalizia kule na baadaye watakuja Bukombe na sehemu nyingine. Katika Mkoa wa Shinyanga patapimwa vijiji zaidi 150, katika Mkoa wa Mbeya kwa vile vimeshamalizika na Rukwa napo wameshamaliza kupima vijiji kwani zaidi ya vijiji 424 vimeshamalizika. Kuna Wilaya nyingine na Mikoa mingine ambayo vijiji vyao vilikwishamalizika, kwa mfano, Arusha vijiji vyote vimeshamalizika vimebaki vijiji 34 katika Wilaya ya Ngorongoro, Manyara, nafikiri vimebaki vijiji 10 kupimwa, lakini vingine vyote vimeshamalizika. Kagera kuna vijiji kama 20 vilivyobaki, Mwanza karibu vijiji vyote vimeshamalizika, Iringa vilipimwa vijiji 119 katika Bajeti ya mwaka 2005. Sasa hivi wapo kule na *actually* wapo Mufindi wanaendelea kupima vijiji. Bahati nzuri gharama za kupima kijiji zimeanza kupungua kwani zilikuwa shilingi milioni moja na laki tano kila kijiji lakini sasa zimepungua mpaka shilingi laki saba na hamsini elfu kwa kila kijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba kama vijiji vyote tutavipima katika nchi hii ambavyo vipo zaidi ya 14,000 baadhi ya matatizo yanayohusu ardhi yatakuwa yamepungua sana kwa vile zaidi ya vijiji 6,000 vimeshapimwa. Ukiongeza na hivi ambavyo vimepimwa kwa sasa vijiji 1,615 sasa hivi kuna vijiji karibu 7,615. Katika bajeti ya mwaka huu tumeweka lengo la kupima vijiji 3,104, tukipima tena mwaka 2008 namna hiyo mkituwezesha kupata Bajeti na mwaka 2009, tunaamini katika miaka mitatu vijiji vyote 14,000 tutakuwa tumevipima.

Tangu tupate Uhuru kuanzia enzi la Karl Peters mwaka 1884 mpaka hivi karibuni ni vijiji 6,000 tu vilikuwa vimepimwa, kwa hiyo, ukivigawa kuanzia miaka hiyo ambayo ni miaka zaidi ya 120 maana yake kila mwaka tulikuwa tunapima vijiji 50. Lakini ukijumlisha vile vijiji vilivyopimwa kuanzia wakati tupate Uhuru ambapo ni karibu miaka 46, hivi sasa inaonyesha kila mwaka tulikuwa tunapima vijiji 122. Sasa katika miezi sita tu hii tumeshapima vijiji 1615. Kwa hiyo, mnaweza kuona *progress* tunayoifanya na hii ni katika kutekeleza sera na *speed* ya kweli kwamba tukifika miaka ile inayokuja mitatu vijiji vyote 14,000 viwe vimeshapimwa na hii tutakuwa tumeleta utajiri wa kweli kwa wananchi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, amezungumzia pia suala la kununua maeneo kwamba Serikali inanunua kwa bei ya chini halafu viwanja vinauzwa kwa bei ya juu lakini *compensation* zinalipwa kwa bei ya chini. Ushauri huu tumeuzingatia lakini kama nilivyoeleza katika Sheria namba 4 na 5 ya mwaka 1999 na Sheria nyingine kama namba 47 ya mwaka 1967 zimezingatia masuala yote ya ulipaji fidia kwa maeneo yatakayochukuliwa ni kama ambavyo nimeyafafanua na hayo ndiyo yatazingatiwa. *(Makofi)*

Lakini gharama ya upimaji viwanja vinakuwa ni kwa juu kwa sababu kupima viwanja ni gharama yake hata vifaa vinavyotumika ikiwa ni pamoja na kupiga picha za anga na ndiyo maana katika miradi ambayo ilianzishwa mahsusi kwa Dar es Salaam zaidi ya viwanja tulikopa shilingi bilioni 8.9 lakini hadi sasa hivi viwanja ambavyo vimeshapimwa kwa Dar es Salaam ni zaidi ya viwanja 33,000, Mwanza ni zaidi ya

viwanja 9500, Morogoro ni zaidi ya viwanja 4,000 na Mbeya vinatakiwa kupimwa viwanja zaidi ya 5,000.

Ningependa kutoa wito kwa Halmashauri zetu za Wilaya ambazo ndizo zina jukumu la kupima viwanja ziweke Bajeti zake katika Bajeti zao, hizi Bajeti ziwe mahsusi kwa ajili ya kupima viwanja na hivyo viwanja baadaye vitauzwa lakini wazingatie pia katika kulipa *compensation* za yale maeneo ambayo watakuwa wanayachukua kwa ajili ya kupima viwanja kwa sababu Ardhi ni Mali.

Mheshimiwa Spika, sifahamu nimebakiwa na dakika ngapi lakini Mheshimiwa Clemence Lyamba, amezungumzia kuhusu tatizo la mji wa Mikumi, tutalifuatilia lakini pia amezungumzia kuhusu wapimaji ambao wapo Mikumi anasema kwamba sasa tutafanyaje lakini hili tutalifuatilia tuone tatizo hili tunaweza kulitatuaje. Angependa kujua pia ramani zinazohusu Majimbo yote nchini hapa. Ninachotaka tu kumweleza Mheshimiwa Clemence Lyamba, ni kwamba kupitia *Government Notice* ambazo zilianzisha Halmashauri za Wilaya, wakuu wote wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya tuliwapa *Government Notice* zinazohusu mipaka yao, kwa hiyo, ni vizuri mipaka hiyo ikazingatiwa na ikasimamiwa vizuri kulingana na *Government* zilizoanzisha Wilaya na Mikoa ile.

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu mipaka ya Majimbo ningemshauri tu Mheshimiwa Clemence Lyamba, aangalie yeye anahudumia Kata ngapi kwa sababu inawezekana tukatoa leo mipaka ya Jimbo lakini kesho majimbo yakawa matatu au Jimbo lile likafutwa na kadhalika. Kwa hiyo, tuzingatie mipaka ya Kiwilaya na mipaka ya kimikoa ambayo ipo chini ya *Government Notice* zilizotolewa na Serikali. Sasa mipaka ya Majimbo izingatie kwenye Kata zetu tunazozitawala. Lakini pia anasema anaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, yeye amezungumzia kuhusu athari za mazingira ambazo bahati nzuri tumezifafanua vizuri katika *section number 52 and 51* ya Muswada huu. Lakini ushauri wake pia tumeuzingatia.

Mheshimiwa Herbert Mntangi, naye amezungumzia mengi ikiwa hata na suala la kuhusisha na wenzetu wanaohusika na barabara katika masuala ya uamuzi wa upana wa barabara hili tutalizingatia kwa sababu tutaliweka kwenye *regulations*. Yale mengi ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu *regulations* zitatungwa tutazingatia katika ushauri ule ili kusudi tuweze kuboresha Miswada hii yote mitatu vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Charles Keenja, amezungumzia vizuri kuhusu suala la Dar es Salaam na bahati nzuri yeye alikuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam inawezekana kuwa baadhi ya matatizo haya pia na yeye alipambana nayo na yalimshinda wakati ule na yapo mengine aliyatatua. Lakini hiyo ndiyo changamoto aliyotupa tutaendelea kuifanyia kazi. Lakini kwa Dar es Salaam bahati nzuri tumeanza kutambua yale maeneo ya pembeni katika kuyapanga vizuri. Ushauri wake mkubwa tunauzingatia na napenda kusema kama alivyoeleza Mheshimiwa Rita Mlaki, tutauzingatia katika kuhakikisha

kwamba masuala ya ardhi na hasa katika kuifanya Dar es Salaam isiendelee kuwa kwenye *unplanned areas,* inaenda vizuri na ndiyo maana kama tulivyosema mpaka sasa hivi tumeshatambua makazi zaidi ya 230,000 na tumekuwa tukishirikiana na wenzetu wa *World Bank* katika kuhakikisha kwamba hawa watu wanashirikishwa katika kuleta maendeleo ya maeneo yao badala ya kuwabomolea.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa ujumla ushauri wa Mheshimiwa Charles Keenja, tunauzingatia, tatizo ni kwamba fedha katika Bajeti ya mwaka jana ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, *development budget* ilikuwa ni shilingi bilioni mbili, sasa shilingi bilioni mbili unashughulikia kilometa za mraba 945,000, ni kazi kubwa. Kwa hiyo, tuna changamoto kubwa na mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge mtahakikisha katika Bajeti ya mwaka huu Wizara ya Ardhi inapata Bajeti ya kutosha ili masuala haya sasa tuanze kuyashughulikia kikamilifu.

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, ametoa pongezi nyingi lakini suala kubwa pia amezungumzia juu ya kuihusisha Benki ikiwepo *World Bank* kama walivyofanya katika Mji wa Kibera kule Nairobi. Nimeshazungumza naye lakini nimeeleza *UN Habitat* kwa ujumla huwa hawana fedha rasmi kwa ajili ya kuendeleza miradi. Tulichofanya na sisi *World Bank* wanatusaidia shilingi bilioni 37 katika miradi ya Dar es Salaam katika kutambua makazi holela lakini tunashirikiana vizuri sana na Mheshimiwa Profesa Tibaijuka na hasa kwa kutambua kwamba mimi ni mjumbe pia wa Kamati ya *UN Habitat* lakini pia mimi ni mmoja wa ma *Co-chair* wa *Third World Urban Forum Three* mpaka mwaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, pia amezungumzia kuhusu masuala ya *mortgage finance,* hili tunazungumza na wenzetu wa Wizara ya Fedha tumesha *draft points* ambazo tunafikiri zinaweza zikasaidia. *Mortgage Finance* ni muhimu sana katika kuleta, 70% ya nyumba zilizojengwa Marekani zimejengwa kwa ajili ya *mortgage finance.* Hakuna nchi yoyote duniani ambapo wananchi wake wanajenga kwa kutumia fedha kutoka mfukoni, wanakopa lakini hata mikopo yao ni ya muda mrefu. Kwa Tanzania kwa mabenki yetu ukitaka kukopa unapewa *duration* ya miaka mitatu wakati Marekani unapewa miaka 40 hadi 60 kulipa. Kwa hiyo, *interest* za mabenki yetu unaambiwa ni 15%, 20% mpaka 30% wakati nchi nyingine duniani kwenye *mortgage system* ya nyumba *interest* huwa ni *less than 10%* kwa hiyo, haya ni masuala ambayo yanatakiwa kujadiliwa na kwa vile tunaandaa sera ya nyumba na Miswada ya Nyumba, ninafikiri michango ya Waheshimiwa Wabunge inaweza ikatusaidia zaidi katika kuhakikisha kwamba suala hili linaweza likatuletea maendeleo mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini tumejaribu kufanya *amendment* mwaka 2004 katika Sheria namba 4 ya mwaka 1999 katika ile *foreclosure* tuliamua kuiweka kwa makusudi ile *foreclosure* na wakoloni, lengo lake kubwa lilikuwa mtu yeyote akishindwa kulipia nyumba yake ananunuliwa halafu anabaki nje kule lakini katika haki za binadamu napo hii si vizuri ndiyo maana katika *amendments* tulizofanya katika sheria namba 4 ya mwaka 2004 ya sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, tumesema kama ile nyumba ni ya makazi hakuja kuiuza lazima *process* za kimahakama zitumike, *otherwise* watu wenye pesa watawaonea wanyonge na sisi tupo hapa kwa ajili ya kuwatetea wanyonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama ni nyumba ya biashara ni ruhusa kufanya vyovyote lakini nyumba ya makazi tumefanya hivyo kwa makusudi kwa sababu tutajikuta watu wengi wanafukuzwa kwenye nyumba zao, wanauzwa kwenye nyumba zao labda kwa watu wengine wenye *interest* zao. Tunajaribu kuliangalia vizuri lakini suala la mabenki yetu kushindwa kuingia kwenye *mortgage system* inawezekana si tatizo tu kwamba Sheria zetu ni mbaya, inawezekana labda wana mahali pengine ambapo wanaweza ku-*make profit* kuliko kuingia kwenye masuala ya nyumba, inawezekana hata *treasury bills* ambazo wanapata hela bila usumbufu na kadhalika.

Sasa hili ni suala la jumla ambalo linatakiwa kuangaliwa na mabenki yetu yameanza kubadilika kwa mfano *Azania Bank* wameshaanza kukopesha watu kwa kutumia *mortagage system, CRDB* wameshaanza kukopesha watu, mimi ninajua kuna watu wamekopeshwa na wanajenga nyumba kupitia *CRDB Bank*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nina imani kubwa katika mabenki mengine yaliyobaki ambayo yapo karibu 26 yataanza kuingia kwenye mambo ya *mortgage system* ili Watanzania waweze kuendelea na Watanzania waweze kuondokana na umaskini. Suala la *mortgage system* kwanza lina-*create employment* na linajenga uchumi katika nchi ambazo zilifanikiwa. Sweden kwa mfano, ilifanikiwa kwa kujenga nyumba zaidi ya milioni moja, wakajengewa wananchi na Sweden ni moja ya nchi ambazo zimetoa tatizo la makazi duniani. Ninaamini mwanzo ni mgumu lakini kadri tunavyoenda masuala mengi yatajitokeza na yataweza kutatuliwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, michango ya Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, tunakubaliana nayo na tutaendelea kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, amezungumzia kuhusu suala la ardhi ya Rufiji Delta kule na kadhalika. Tumezingatia ushauri wake, lakini mengine tutaendelea kuzungumza ndani ya Serikali wakiwemo wenzetu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuona namna gani tunaweza tukasaidia wananchi wake wa Utete.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Juma Killimbah, nimekwishamjibu kuhusu suala lake linalohusika. Lakini pia katika Mkoa wa Singida baadhi ya vijiji vitaendelea kupimwa katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Cheyo, kaka yangu ametoa ushauri mwingi kama nilivyoeleza, tumeuzingatia na mengine tutaendelea kuyazingatia kadri tunavyoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella alizungumzia kuhusu ku-*maintain traditional areas* tumelizingatia. Lakini pia katika *percentage* ya akinamama tumelizingatia vizuri katika sheria kwa sababu tumesema *at least three unless* mniambie tubadilishe tuseme *at least three men*. Lakini tuliweka hivi kwa makusudi kwa sababu ukishasema *at least three* maana yake wanaweza kuwa saba, wanaweza kuwa wote kutokana na *professionals* zao na ninakubaliana na ushauri wake kwamba sasa

akinamama katika masuala haya ya *professional*s wako juu sana na mimi ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafikiri nimejitahidi kutoa ufafanuzi kwa haraka haraka ili kuhakikisha kwamba yale yote ya msingi yaliyochangiwa na Waheshimiwa Wabunge yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, niseme kwa uwazi kabisa mimi na Naibu Waziri pamoja na wataalam wangu tumefaidika sana na michango mizuri sana iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Michango yao ni mizuri na hii ilikuwa ikielezea hali halisi ya masuala yanayowagusa wananchi wa chini.

Mheshimiwa Spika, migogoro imekuwa ikijitokeza na njia pekee ya kutatua migogoro hii ni katika kuzipitisha hizi sheria tatu na baadaye tena tutaleta sera nyingine kwa mfano ya upimaji ramani na sera ya nyumba ili masuala ya ardhi yaweze kutatuliwa kikamilifu. Lakini pia tumezingatia mamlaka zinazohusika katika kutatua masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kama Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja wataukubali Muswada huu ninaamini masuala mengi yatatatuliwa. Kama nilivyosema katika wote waliochangia katika Miswada hii wameunga mkono, hata changamoto za kaka yangu Mheshimiwa John Cheyo ni katika uchungu tu, lakini ukweli alikuwa anaonyesha anaunga mkono Miswada hii mitatu, hata sasa hivi anaonyesha anaunga mkono tu. Kwa sababu Miswada hii mitatu ina lengo la kuwasaidia watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Miswada hii kama nilivyosema usiangalie kwamba kuna John Magufuli katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Miswada hii mitatu ni kwa ajili ya manufaa ya Watanzania wote. Tumekuwa na migogoro mingi. Katika Mabaraza ya Ardhi kwa mfano, hadi sasa hivi zimeshafunguliwa kesi zaidi ya 5,000 na migogoro iliyotolewa ni katika Halmashauri za Wilaya, kila Wilaya ina migogoro, ina migogoro na Wilaya inayoongozwa ina migogoro zaidi ya 1,200. Kwa hiyo, ukijumlisha katika Wilaya zote 113 unaweza ukajua ni migogoro ya aina gani.

Mheshimiwa Spika, pale Wizarani ukishaingia tu asubuhi, unakutana na watu wengine wamepata *stroke,* wengine wamedhulumiwa viwanja vyao, wengine wanalia, ni Wizara ya migogoro, ni migogoro kila siku asubuhi unaingia ni migogoro mpaka unatoka ofisini unashinda na migogoro, sijawahi kuona Wizara ya namna hiyo, ndugu zangu ni ngumu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini migogoro hiyo haiwezi ikamalizwa hivi hivi, ni lazima tutunge sheria zitakazoweza kusaidia kupunguza migogoro hiyo na kama si kuimaliza kabisa. Wanaopata shida sana ni wananchi wa hali ya chini, wenye pesa wamekuwa na jeuri ya kuchukua mahali popote hata maeneo yanayovamiwa sasa hivi yanavamiwa kwa sababu ya watu wenye jeuri ya pesa. Sasa tukishakuwa na sheria hizi, tukishawapa mamlaka wanavijiji wakapanga hili ni eneo lao la mifugo, hili ni eneo letu la kukaa, hili

ni eneo letu la kukata kuni, hakuna mtu mwingine atakayeweza ku-*disturb* kule. Kwa sababu sheria za Serikali za vijiji zinatambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua hata wewe kwenye Jimbo lako la Urambo Masahariki kuna migogoro. Nina matumaini makubwa na wewe utaunga mkono Muswada huu kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wote ili angalau Miswada hii iweze kupita na kumaliza migogoro kama siyo kuipunguza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa John Cheyo, ndugu yangu tuna lengo kubwa la kumaliza migogoro ikiwa ni pamoja na ya Bariadi na bahati nzuri Bariadi mwaka huu vijiji vyake vitaendelea kupimwa. Sasa kaka yangu usipinge tu wewe peke yako, jitahidi uunge mkono Miswada hii mitatu ili twende mbele katika kuleta maendeleo ya kweli ya masuala ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kulikuwa na masuala ya Mbezi ambayo yalikuwa na migogoro mikubwa, tulikuwa na maamuzi katika viwanja vyote 14,500 ambavyo tulivipiga picha. Wananchi wa kule tumewaongezea muda wa kujenga tena zaidi ya miaka mitatu na nusu kwa sababu tulijua kabisa yale yaliyokuwa yanazungumzwa kuna kesi nyingine zilikuwa Mahakamani, watu wengine walikuwa wanaonewa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tukasema miaka mitatu na nusu tunawaongezea na hati zao tunazibadilisha kuanzia miaka 33 sasa zitakuwa miaka 99. Sasa hii ni kwa Dar es Salaam tu, Wilaya moja ina viwanja zaidi ya 14,500 zidisha kwa Wilaya 113, zidisha kwa Mikoa yote, kila siku ni migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge tuipunguze migogoro hii kwa kunipitishia hii Miswada mitatu ili ipite mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo tutaiamua baada ya kazi ya Kamati ya Bunge Zima. Ningependa tu mwelewa tu kwamba Miswada hii mitatu tutaipitia kwa utaratibu ufuatao:-

Kwanza, siyo kama ilivyo kwenye *Order Paper* tunaanza na Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango Ardhi *(The Land Use Planning Bill, 2006),* pili, ni Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 *(The Town Planners (Registration) Bill, 2006* na hatimaye tutamaliza Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa na Kutekeleza Masuala Mbalimbali yanayohusu Mipango Miji *(The Urban Planning Bill, 2006).*

Nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi, *(The Urban Land Use Planning Bill, 2006)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 14

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Cheyo, Ibara ya 19!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo Ibara ya 19. Ibara ya 19(2): *"the Commission shall in their capacity...,"* kazi za *commission.*

**MWENYEKITI:** Endeleea Mheshimiwa John Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nangojea ruhusa yako.

**MWENYEKITI:** Sawa sawa unaweza kuendelea.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Waziri kwamba mambo ya sheria tunayoyazungumzia hayana uhusiano na mtu, *is not person,* tunazungumza mambo ya nchi. Kwa hiyo, siyo kwamba Mheshimiwa John Magufuli yuko pale kwa hiyo kuna ugumu wa aina yoyote, hapana, ni sheria. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi nimefurahishwa sana jinsi Mheshimiwa John Magufuli alivyotujibu Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani John Magufuli ni tofauti kuliko yule ambaye nilikuwa namfahamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mimi nataka kujua kitu kimoja tu. Wakati nachangia nilitoa tahadhari kwa mambo ambayo ni mipango mikubwa na ambayo inahusu watu wengi. Kwa mfano, kupanga kwamba Mlima wa Uluguru uwe ni Hifadhi au kupanga kwamba Mlima Kilimanjaro sasa umekuwa *declared* ni Hifadhi na watu

wote waondoke. Mipango hiyo Bunge hili lingehusishwa. Nafikiri kwa mambo ambayo ni makubwa ni vizuri Bunge likahusishwa kuliko kuwaachia kazi kubwa kama hiyo kwa uwezo wa Waziri tu au kwa uwezo wa Tume peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ningependa kama kuna tahadhari ya namna hiyo *then I think* watu wengi wata-*feel very comfortable*. Lakini Waziri amejibu vizuri na wengi waliokuwa wanamsikiliza zaidi juu ya mambo ya fidia. Ningependa kama hiyo *Hansard* ya leo ingeweza kuwa *published* watu waelewe vizuri jinsi ambavyo wanaweza wakapata *compensation* kwa ajili ya ardhi yao ambayo ni mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ufafanuzi tu juu ya hilo jambo; je, Bunge litahusishwa kwa mambo ambayo ni makubwa?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *National Land Planning Authority,* kwa ujumla itahusika na asilimia mbili ya eneo lote. Maeneo mengine yote *actually* asilimia 98 yatakuwa yanashughulikiwa Mikoani, Wilayani, kwenye mamlaka za Vijijini na kadhalika. Tuliweka hii *National Land Planning Authority* katika kushughulikia haya masuala kwa masuala ambayo yanahusika ya Kitaifa, kwa sababu Muswada huu kama tulivyouwasilisha hapa Bungeni lazima yale yote yatakayokuwa yanafanyika kwa mfano, wakati wa Bajeti kama kuna maamuzi ya Kitaifa yatakuwa yanaletwa na Waziri atakayekuwa anahusika na masuala ya ardhi anakuja kutoa taarifa hata kwenye Bajeti yake kwamba kuna hiki kimefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya Kitaifa kwanza hayatafanywa na hii *Authority,* kutakuwa na kushirikiana na mamlaka zinazohusika, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara zinazohusika zote zinakaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtoe wasiwasi kwamba hii inayohusiana ni asilimia mbili tu ya *land* na inawezekana ile *land* ikawa na mahusiano labda katika *investment*. Lakini kama nilivyosema ikijitokeza *land* ya namna hiyo. Kwa mfano, labda *land* ilikuwa ni Hifadhi ya Taifa inataka ikatwe eneo fulani liwe kwa ajili ya manufaa ya kazi fulani, pakishapelekwa mapendekezo hayo Serikalini kila kitu kikimalizika Bunge lazima litapata taarifa kwa sababu Mheshimiwa Waziri yeyote anawajibika kwa ajili ya kuja kutoa taarifa ya yale yaliyofanyika katika Wizara ile katika kipindi chochote hata wakati wa bajeti na kadhalika.

Kwa hiyo, ningependa tu nimtoe wasiwasi ndugu yangu Mheshimiwa John Cheyo kwanza hili linalohusu asilimia mbili tu. Lakini pia hii *National Land Planning Authorities* haina mamlaka ya kufuta sheria zingine zilizopo. Kuna sheria kwa mfano, za Maliasili ambazo zilianzisha Mlima Kilimanjaro na kadhalika. Hizo sheria zinaendelea kuwepo. Kwa hiyo, hii ni katika ku-*coordinate National wise* katika masuala ya Kitaifa. Lakini wakisha-*coordinate* na Serikali kukubaliana kwa vyovyote mhusika yeyote atakuwa anakuja kutoa taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge hata wakati wa bajeti au nini. Waheshimiwa Wabunge watakuwa na haki ya kutoa mawazo yao au kukataa na

kadhalika. Kwa hiyo, hili ni katika kujenga tu umoja wa kweli katika kushughulikia masuala ya Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Baada ya ufafanuzi huo, Mheshimiwa John Cheyo, hujaridhika?

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba ni *very simple* kwamba kile ambacho ni kikubwa na ambacho kina-*affect* watu wengi wanavyokaa na nimetoa mifano. Hili jambo haliko katika Jimbo langu, watu wa Morogoro kila mmoja ameambiwa ahame waachie Milima ya Uluguru, watu wameishia pale *years in years*. *Solution* siyo kuhama, *solution* ni kuangalia mazingira. Kama linawezekana hilo likafanyika kwa Waluguru kwa nini lisifanyike kwa Wachaga kwamba Wachaga wote wateremke au kwa nini lisifanyike kwa Wapare, kwamba Wapare wote wateremke. Kwa hiyo, haya ni maamuzi makubwa siyo kwamba Bunge litaarifiwe, ni kwamba Bunge liamue *when* inapokuwa kwa mambo ambayo ni makubwa. *I think to me* siyo ombi ambalo ni *outrageous, I think* ni ombi ambalo mimi naona ni muhimu. Kwa sababu kuchezea ardhi au kuiacha ardhi iko juu juu tu hivi, kusema kweli hatuwatendei haki watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nataka *very simple answer* kwa mambo ambayo ni makubwa kwa sababu yoyote ile je, Waziri anaji-*commit* kwamba Bunge litahusishwa siyo taarifa lakini kwa maamuzi.

**MWENYEKITI:** Kwa maana nyingine Waziri labda ule utaratibu kwamba ikiwa *gazetted* ile *intention* ya kufanya hivyo pengine kabla ya uamuzi wa mwisho anavyoshauri pengine mambo hayo yafikishwe Bungeni.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sifahamu kwa nini Mheshimiwa John Cheyo anazungumzia ukubwa wa namna gani. Kwa sababu kwanza Muswada huu haujapitishwa. Muswada huu tumesema kuna masuala ambayo yatashughulikiwa na vijiji. Kwa hiyo, katika vijiji vitakavyoshughulikiwa kutakuwepo na kijiji cha Chato, Bariadi, cha Uluguru na kadhalika. Hivi vijiji vitashughulika katika maamuzi yake kwamba hapa tunapanda miti, hapa tunafanya nini, eneo hili ni kwa ajili ya ufugaji. Muswada huu unazungumza hivyo. Kuna masuala yatakayoshughulikiwa kwa ngazi ya Halmashauri ya Wilaya, wana *power* ya ku-*decide* mambo yao. Kuna masuala yatakayoshughulikiwa na Sekretarieti ya Mkoa wanaamua ni mambo gani yatakayoshughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia hii *National Land Planning* ya *Authority* inashughulikia asilimia mbili tu ya *land* yote ya Tanzania. Sasa mimi nilifikiri Mheshimiwa John Cheyo angeuliza zaidi kuhusu ile asilimia 98 ya *land* ambayo itashughulikiwa kule badala ya kung'ang'ania tu asilimia mbili ambayo inashughulikia masuala yanayohusu Kitaifa. Nimweleze kwamba katika masuala yatakayokuwa yanachaguliwa na hii *National Land Planning Authority* na Mkurugenzi wake ni *Presidential appointee,* tutakuwa tunayaleta kutoa taarifa kwa Waheshimiwa

Wabunge. Sasa anauliza tu asilimia mbili kwa nini yale yanayoamuliwa kwenye vijiji hatuyaleti kwenye Bunge, kwa nini yanayoamuliwa kwenye Halmashauri za Wilaya hatuyaleti kwenye Bunge? Mimi nafikiri Mheshimiwa John Cheyo, aiamini Serikali. Lakini Serikali ina utaratibu wake kama ule ambao umeuzungumza kwa kupitia labda *Government Notice* inaweza ikatangazwa kwamba eneo hili litakuwa hivi na hivi na ndivyo Serikali imekuwa ikifanyika. Ningemwomba Mheshimiwa John Cheyo ndugu yangu na kwa vile leo amenipongeza sana kwamba mimi ni Magufuli tofauti wa miaka yote, basi utofauti ule athibitishe katika haya kwa kukubali hii *National Land Planning Use* iendelee katika masuala haya.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani maelezo ya Mheshimiwa Waziri yamejitosheleza kwamba Tume ile itafanyika chini ya uongozi wa Wizara. Waziri atakapopelekewa taarifa zile zitakuja Bungeni kama mambo mengine yote ya Serikali yanavyokuja Bungeni. Kwa hiyo, hili kwa kweli halina matatizo. Lakini la pili, kwa faida ya kumbukumbu napenda kumshauri Mheshimiwa John Cheyo, kwamba kinachofanyika Morogoro siyo kuwashusha tu wananchi Waluguru kama alivyosema kutoka Milimani wakati wamekuwa wakikaa huko siku zote, hapana. Kilichofanyika ni kwamba wapo watu waliovuka mpaka wamekwenda nje ya mpaka wa milima wamekwenda kujenga na kulima, hao ndiyo wanaondolewa kwa makubaliano ya uongozi wa Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:**Baada ya ufafanuzi huo Ibara hiyo inaafikiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapana.

**MWENYEKITI:** Nimekwishaamua na tumepitisha.

Kifungu cha 20

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 21

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 21 kuhusiana na *District Planning Authorities* na wakati nachangia nilizungumzia suala la *Township Authorities* na jinsi gani ambavyo Sheria hii imeshindwa kurandana na Sheria ya Serikali za Mitaa ambayo inatambua *Township Authorities* na katika hali ya kawaida *Township Authorities* mipango yake ya ardhi ni Mipango Miji. Kwa maana hiyo ni kwamba iwapo *Township Authorities* zitashughulikiwa chini ya *Land Use Planning Act,* ina maana zitaendelea kushughulikiwa kama vijiji na Waziri alipokuwa anatoa maelezo yake

hakuweza kulifafanua vya kutosha kwa vipi ambavyo Miji inavyokua kwa kasi na ninatoa mfano kama Kibaigwa, Miji kama Mwadinga, Miji kama Kalinzi jinsi gani ambavyo itaweza kushughulikiwa kwa sababu hakuna sheria inayowatambua aidha kati ya hii au nyingine itakayofuata ya *Urban Planning*. Nilikuwa naomba maelezo katika hili.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitishwa kwa Sheria hii ya *Land Use Planning Bill,* ina maana kwamba inafuta Sheria namba 7 na namba 8 ya Tawala za Mikoa. Tunajaribu kurahisisha mambo ili mengi yaweze kushughulikiwa kwenye ngazi za Tawala za Mikoa. Wakati nikijibu hoja nimejaribu kufafanua suala muhimu sana ambalo amelizungumza Mheshimiwa Kabwe Zitto, katika miji midogo inayokua na nilileta mapendekezo na nimeyasoma hapa yako kwenye *Hansard* kwamba kwenye miji midogo kama Kibaigwa, Kasulu, Mwadinga na kadhalika tuongeze kipengele namba 33(5) ambacho kitasomeka: *"For the purpose of this section, the village land use plan shall include plan minor settlements or trading centres referred to sixth schedule to this Act."*

Nilifanya hivyo kwa makusudi makubwa kwamba katika miji hii midogo inayokua Kibaigwa, Mwadinga, wapi iweze kuwa *included* ili kusudi tusiwafanye hao wananchi wakashindwa ku-*move* katika maendeleo yao. Sasa nilifikiri Mheshimiwa Kabwe Zitto, angepongeza hata kwa kusikiliza haya maoni yake na nimeyasoma kwenye *Hansard*. Sasa sijui alikuwa anasikiliza nini ndugu yangu. Mheshimiwa Kabwe Zitto tumelizingatia hili na tumefanya marekebisho. Kwa hiyo, ningeomba hiki kipengele kiwekwe.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Kabwe Zitto, ameridhika. Ahsante sana Waziri kwa maelezo mazuri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28

Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 32

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 40

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 50

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65

*(Vifungu Vilizotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 66

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

Kifungu cha 67

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Jedwali la 3
Jedwali la 4

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Jedwali la 5

Jedwali la 6

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, Kuendesha na Kutekeleza Sheria ya Mipango ya Ardhi wa mwaka 2006 *(The Land Use Planning Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya kuweka Mwongozo wa kuandaa na kutekeleza masuala mbali mbali yanayohusu Mipango ya Ardhi pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake ukubalike.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Kwa kuwa Miswada yote ilikwishatolewa maelezo, sasa namwomba Katibu tuingie katika hatua za Muswada wa pili.

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili wa Mipango Miji wa Mwaka 2006 (*The Town Planner's Registration Bill, 2006)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 6

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 7
Kifungu cha 8

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17
Kifungu cha 18
Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 23

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na  Marekebisho yake)*

Kifungu cha 24
Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji**
**(*The Town Planner's Registration Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Kuanzisha Bodi ya Usajili ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 *(The Planner's Registration Bill, 2006)* pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, na Kutekeleza Masuala Mbalimbali ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 *(The Urban Planning Bill, 2006)***

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2

*(Vifungu Vilichotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 3
Kifungu cha 4

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 5

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10
Kifungu cha 11

*(Vifungu Vilivyhotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 12

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 17
Kifungu cha 18

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21
Kifungu cha 22
Kifungu cha 23

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 24

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31
Kifungu cha 32
Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36
Kifungu cha 37
Kifungu cha 38
Kifungu cha 39

Kifungu cha 40
Kifungu cha 41
Kifungu cha 42
Kifungu cha 43
Kifungu cha 44
Kifungu cha 45
Kifungu cha 46
Kifungu cha 47
Kifungu cha 48
Kifungu cha 49
Kifungu cha 50
Kifungu cha 51
Kifungu cha 52
Kifungu cha 53
Kifungu cha 54
Kifungu cha 55
Kifungu cha 56
Kifungu cha 57
Kifungu cha 58
Kifungu cha 59
Kifungu cha 60
Kifungu cha 61
Kifungu cha 62
Kifungu cha 63
Kifungu cha 64
Kifungu cha 65
Kifungu cha 66
Kifungu cha 67
Kifungu cha 68
Kifungu cha 69
Kifungu cha 70
Kifungu cha 71
Kifungu cha 72
Kifungu cha 73
Kifungu cha 74
Kifungu cha 75
Kifungu cha 76

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 77

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 78
Kifungu cha 79

Kifungu cha 80
Kifungu cha 81

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Jedwali la 1
Jedwali la 2
Jedwali la 3
Jedwali la 4
Jedwali la 5

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja Marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa, na Kutekeleza Masuala Mbalimbali ya Mipango Miji wa Mwaka 2006 *(The Urban Planning Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Kuweka Mwongozo wa Kuandaa na Kutekeleza Masuala Mbalimbali yanayohusu Mipango Miji wa mwaka 2006 *(The Urban Planning Bill, 2006)* pamoja na marekebisho yake na kuukubali. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu pamoja na marekebisho yake sasa ukubalike. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA :** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa orodha ya shughuli zetu za asubuhi hii, shughuli nyingine naona zitaendelea kwa mujibu wa *Order Paper* hapo saa 11.00 jioni. Hakuna kingine zaidi ila nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.50 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kawaida ya *Order Paper* huwa tunakwenda kwa mtiririko uliowekwa. Sasa nadhani tumekosea mawasiliano, anayepaswa kusoma Muswada huu wa kwanza, *Supplementary Appropriation Bill* inaonekana hayupo. Aliyepo ni yule anayepaswa kusoma Muswada wa pili. Kwa hiyo, naomba rasmi niombe kibali chenu kwamba tuingie Muswada wa pili halafu wa kwanza utakuja baadaye.

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007** ***(The National Bank of Commerce [Reorganisation and Vesting of Assets and Liabilities) Bill, 2007 (Cap. 404])***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa marekebisho ya Sheria ya Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara, yaani *(The National Bank of Commerce (Re-organization and Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment) Act, 2007* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda - Mbunge wa Handeni kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba, tumezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi ambayo imesaidia sana katika kuuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada huu ni kukabidhi chombo kimoja cha Kiserikali kazi zilizoachwa na zitakazoachwa na mashirika hodhi ya *Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO)* na *SIMU 2000 Limited* pamoja na *Loans and Advances Realisation Trust (LART)* kwa lengo la kuipunguzia Serikali gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unakusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara Sura ya 404 *(The National Bank of Commerce (Re-organization and Vesting of Assets and Liabilities)Act CAP 404* iliyoanzisha Shirika la *Consolidated Holding Corporation (CHC)* ili kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha *CHC* kupokea na kufanya kazi za iliyokuwa *Loans and Advances Realisation Trust (LART), Air Tanzania Holdings Corporation (ATHCO)* na kazi zitakazoachwa na *SIMU 2000 Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CHC* ilianza rasmi shughuli zake tarehe 01 Oktoba 1997 kwa kuchukua mali zinazojumuisha majengo 443, magari 66 na samani mbalimbali zenye thamani ya Shilingi bilioni 20, Kesi na mashauri 1,000 yenye thamani ya Shilingi bilioni 148 na madeni 5,287 yenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 104 ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara *(NBC)*. Kwa mujibu wa Azimio la Bunge Na. 20/2002 uhai wa *CHC* utamalizika ifikapo mwezi Septemba 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CHC* imeonyesha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo hadi kufikia Desemba, 2006, Shirika limeweza kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 26 kutokana na uuzaji wa majengo 440, magari 66 na Samani mbalimbali; Shilingi bilioni 27 kutokana na ukusanyaji wa madeni 3,106 na Shilingi bilioni 25 kutokana na mapato ya pango na riba. Aidha, hadi kufikia Mwezi Septemba, 2006, *CHC* imeweza kuvuka lengo la mawasilisho ya fedha Hazina kwa kiasi cha Shilingi bilioni 29, ikilinganishwa na Shillingi bilioni 17 zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi hivi sasa *CHC* imebakiwa na madeni 2,181 yanayokadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi bilioni 66 ambayo bado hayajakusanywa; Kesi na mashauri 163 yanayoendelea katika Mahakama mbalimbali yenye madai ya Shilingi bilioni 33 na majengo matatu yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili ambayo bado hayajauzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufanisi huu ulioonyeshwa na *CHC* katika ukusanyaji madeni na ukamilishaji wa kesi za madai zilizopo Mahakamani, Serikali imefikia uamuzi wa kuhamishia *CHC* shughuli zilizobaki za *LART* iliyomaliza muda wake mwezi Juni, 2006 na kazi nyingine za aina hii zinazofanywa na vyombo vingine vikiwemo Shirika la *ATHCO* lililomaliza muda wake mwezi Desemba, 2006 na *SIMU 2000 Limited* itakayomaliza shughuli zake ifikapo mwezi Disemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za mashirika ya *LART* na *ATHCO* zilizobakia mpaka hivi sasa na zinazotarajiwa kuhamishiwa kwenye Shirika la *CHC* ni kama ifuatavyo:

Kwanza, kwa upande wa *LART* ni madeni 42 yenye thamani ya Shilingi bilioni 17, ufilisi wa mashirika 28 yenye thamani ya Shilingi bilioni saba na mashauri 74 yenye thamani ya Shilingi bilioni 111.

Pili, kutoka *ATHCO* ni madai 56 yenye thamani ya Shilingi bilioni tatu, madeni 123 yenye thamani ya Shilingi bilioni nne ambayo hayajalipwa kwa wadai, mashauri 28 yenye thamani ya Shilingi bilioni tatu, samani za Ofisi na vifaa mbalimbali 71 vya thamani ya Shilingi milioni 16, magari mawili yenye thamani ya Shilingi milioni 20, akaunti tano za Benki zenye thamani ya Shilingi milioni 320 na nyumba 11 na viwanja viwili vyenye thamani ya Shilingi milioni 332.

Kwa upande wa *SIMU 2000 Limited*, ambayo bado haijamaliza shughuli zake, hadi hivi sasa inasimamia uuzaji viwanja 19 vyenye thamani ya Shilingi milioni 31 ambapo vingi kati ya viwanja hivi vipo kwenye maeneo ya milima na vilikuwa

vinatumiwa na Shirika la Posta na Simu kwa ajili ya kusimika minara ya simu; majengo 13 yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili, kesi 12 zinazoendelea katika Mahakama mbalimbali, madeni yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili, kushughulikia madai ya wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta la Afrika Mashariki *(EAPTC)* na ufuatiliaji wa mikataba ya ukodishaji jengo la posta la zamani na jengo la Benki ya Posta lililopo Mkwepu. Shughuli zitakazosalia bila kukamilishwa na Kampuni hii ifikapo Mwezi Disemba, 2007 zitahamishiwa *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya muswada, ili kuiwezesha *CHC* kutekeleza majukumu yake mapya, inapendekezwa kuifanyia marekebisho Sheria ya *The National Bank of Commerce (Re-organization and Vesting of Assets and Liabilities) Act, CAP 404* ili; Kwanza, kuongeza muda wa uhai wa *CHC* kwa kipindi kingine cha miaka minne, baada ya uhai wake kumalizika itakapofika mwezi Septemba 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo muda wa miaka minne unakaribia kumalizika na *CHC* itakuwa haijamaliza majukumu yake, Sheria inapendekeza Bunge kuongeza muda wa uhai wa *CHC* kwa Azimio la Bunge baada ya Waziri wa Fedha kuwasilisha hoja Bungeni.

Pili, kuiongezea *CHC* majukumu mapya ya shughuli zilizoachwa na *LART, ATHCO* na zitakazoachwa na *SIMU 2000 Limited*.

Tatu, kuhamishia mali na madeni yaliyohusu mashirika haya kwa *CHC*. Aidha, kwa kuwa *LART* na *ATHCO* tayari zimemaliza muda wake na kuacha mali, madeni na kesi ambazo hazijashughulikiwa na zinapaswa kushughulikiwa mapema, yamependekezwa marekebisho ya kuanza kutumika rasmi kwa Sheria hii badala ya tarehe 01 Julai, 2007, badala yake inapendekezwa kuwa Sheria hii ianze kutumika mara baada ya Muswada kutiwa saini na Mheshimiwa Rais na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kesi zilizokuwa Mahakamani na kwenye Mabaraza *(Tribunal)* zinazohusu mashirika haya, zitaendelea katika Mahakama husika chini ya usimamizi wa *CHC*. Kwa upande wa wafanyakazi, baadhi yao walikwishalipwa mafao yao (wale wa *LART* na *ATHCO*).

Aidha, kwa upande wa *SIMU 2000 Limited* ambayo shughuli zake zitahamishiwa *CHC* hapo baadaye, wafanyakazi wake ambao wameajiriwa kwa mikataba watalipwa haki zao na hapatakuwa na uhamisho kwenda *CHC*, kama ilivyokuwa kwa wafanyakazi wa iliyokuwa *NBC*, kwa mujibu wa Sheria ya sasa ya *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni yafuatayo;-

(a) Kuweka bayana kwamba muda wa uhai wa *Consolidated Holding Corporation* utamalizika baada ya miaka minne na pia muda

unaweza kuongezwa baada ya kupata ridhaa ya Bunge kwa kupitisha Azimio la Bunge.

(b) Kuainisha kwamba, Shirika Hodhi la Benki *(Consolidated Holding Corporation)* litapokea na kusimamia kazi zilizosalia za *LART*, *ATHCO* na *SIMU 2000 Limited*.

Kesi mbalimbali zilizokuwa Mahakama zinazohusu *LART*, *ATHCO* na *SIMU 2000 Limited* zitaendelea katika Mahakama husika chini ya usimamizi wa *CHC*. Aidha, kesi ambazo hapo awali zilikuwa zinaendeshwa na *LART Tribunal* zitahamishiwa kwenye Mahakama zenye mamlaka ya kusikiliza kesi hizo chini ya usimamizi wa *CHC*.

Kuainisha kwamba, endapo *Consolidated Holding Corporation* itamaliza uhai wake kabla ya kumalizika kwa kesi zinazosimamiwa na shirika hili, basi kesi hizo zitasimamiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada huu yamegawanyika katika sehemu kuu mbili.

Sehemu ya Kwanza, yenye kifungu cha kwanza, inahusu masuala ya Utangulizi, kama vile jina la Muswada wenyewe.

Sehemu ya Pili ya Muswada, ina kifungu cha pili hadi cha tano. Kwanza, katika kifungu cha pili inapendekezwa tafsiri ya maneno mbalimbali na tarehe ya kuanza rasmi kwa Sheria hii, ambapo inapendekezwa Sheria ianze kutumika baada ya kusainiwa na Mheshimiwa Rais na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Pili, kifungu cha tatu kinapendekeza kurekebisha kifungu cha tano, kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara Sura ya 404, ili kuongeza muda wa kumalizika uhai wa *Consolidated Holding Corporation* kuwa ni baada ya miaka minne.

Tatu, katika kifungu cha nne, inapendekezwa kurekebisha kifungu cha sita cha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara Sura ya 404 ili Shirika Hodhi la Benki *(Consolidated Holding Corporation)* liweze kupokea na kusimamia kazi zilizosalia za *LART, ATHCO* na zitakazoachwa na *SIMU 2000 Limited*.

Nne na mwisho, Kifungu cha tano kinapendekeza kufanyia marekebisho kifungu cha nane cha Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara , Sura ya 404 ili kuainisha kwamba *CHC* ndio chombo pekee kitakachokuwa na mamlaka ya kushughulikia mali na madeni yatakayotoka *LART, ATHCO* na *SIMU 2000 Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liujadilii Muswada uliopo mbele yenu na hatimaye likubali kuupitisha kuwa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. DR. ABDALLAH OMAR KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa *The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Assets and Liabilities) (Amendment) Act, 2007* kwa mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya Kamati, naomba nianze kwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kutokana na ushindi wa kishindo alioupata Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura katika Jimbo la Tunduru. Ushindi huu ni ishara kuwa Sera za CCM ni endelevu na zinakubalika. Karibu Mheshimiwa Mtutura katika Bunge hili Tukufu tufanye kazi yetu ya uwakilishi kwa wananchi waliotupa dhamana hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha katika hotuba yake, Muswada huu unakusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara Sura 404 *The National Bank of Commerce (Re-organisation and Vesting of Assets and Liabilities) Act, CAP 404* iliyoanzisha Shirika la *Consolidated Holding Corporation* ili kuweka utaratibu wa kisheria utakaowezesha *CHC* kupokea na kufanya kazi iliyokuwa inafanywa na *Loans and Advances Realisation Trust (LART); Air Tanzania Holding Corporation (THCO)* na kazi zitakazoachwa na *SIMU 2000 Ltd*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba *Consolidated Holding Corporation (CHC)* iliundwa kufuatia uamuzi wa Serikali wa kuvunja iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara na kuunda *NBC*(1997) *Ltd*, *(*sasa *NBC Ltd); National Micro-finance Bank Ltd* na *NBC Holding Corporation* sasa *Consolidated Holding Corporation*. Kwa mujibu wa kifungu Na. 6 cha Sheria hiyo, pamoja na majukumu mengine *Consolidated Holding Corporation* ilikabidhiwa majukumu yafuatayo:-

Kwanza, kusimamia na kuuza mali zote walizokabidhiwa ikiwa ni pamoja na majengo 443, magari 66, samani na vifaa vya Ofisi iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara, ambavyo havikugawiwa kwa *NBC Ltd* na *National Micro-Finance Bank Ltd.* Mali hiyo ilikuwa na thamani ya Shilingi milioni 19,928.

Pili, kukusanya madeni sugu ya wateja wapatao 5,287 yaliyotolewa kwenye vitabu vya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara na kuwekwa kwenye vitabu vya kumbukumbu. Madeni hayo yalikuwa na thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 104,000.

Tatu, ulipaji wa madai pamoja na usimamizi na uendeshaji wa kesi zipatazo 1,000 zilizofunguliwa dhidi ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara. Kesi hizo zilikuwa na jumla ya madeni yenye thamani ya takribani Shilingi milioni 148,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Consolidated Holding Corporation* ilianza rasmi shughuli zake tarehe 01 Oktoba, 1997 ambapo hadi kufikia Desemba, 2006, Shirika liliweza kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 26 kutokana na uuzaji wa majengo 440, magari 66 na samani mbalimbali; Shilingi bilioni 27 kutokana na ukusanyaji wa madeni 3,106 na Shilingi bilioni 25 kutokana na mapato ya pango na riba. Aidha, hadi kufikia mwezi Septemba, 2006 *Consolidated Holding Corporation* imeweza kuvuka lengo la mawasilisho ya fedha Hazina kwa kiasi cha Shilingi bilioni 29, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 17 zilizokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi hivi sasa *Consolidated Holding Corporation* imebakiwa na madeni 2,181 yanayokadiriwa kuwa na thamani ya Shilingi bilioni 66 ambayo bado hayajakusanywa. Kesi na mashauri 163 yanaendelea katika Mahakama mbalimbali yenye madai ya Shilingi bilioni 33 na majengo matatu yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili ambayo hayajauzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeridhishwa kwa kiwango kikubwa kutokana na ufanisi ulioonyeshwa na *Consolidated Holding Corporation* katika ukusanyaji wa madeni na ukamilishaji wa kesi za madai zilizopo Mahakamani. Hivyo Kamati inaafiki uamuzi wa kuhamishia *Consolidated Holding Corporation* shughuli zilizobaki za *LART* iliyomaliza muda wake mwezi Juni, 2006 na kazi nyingine za aina hii zinazofanywa na vyombo vingine vikiwemo Shirika la *ATHCO* lililomaliza muda wake mwezi Desemba, 2006 na *SIMU 2000 Ltd* itakayomaliza shughuli zake ifikapo mwezi Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa kuwa shughuli za Mashirika ya *LART* na *ATHCO* zilizobaki mpaka hivi sasa na zinazoatarajiwa kuhamishiwa kwenye Shirika la *CHC* ni kama zile ambazo zilizungumziwa na Naibu Waziri wa Fedha. Ili kuiwezesha *CHC* kutekeleza majukumu yake mapya, Kamati imeridhika kuifanyia marekebisho Sheria ya *The National Bank of Commerce (Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) ACT, CAP 404*', ili:-

- Kuongeza muda wa uhai wa *CHC* kwa kipindi kingine cha miaka minne, baada ya uhai wake kumalizika itakapofika mwezi Septemba, 2007;

- Kuiongezea *CHC* majukumu mapya ya shughuli zilizoachwa na *LART*, *ATHCO* na zitakazoachwa na *SIMU 2000 Limited;* na

- Kuhamishia mali na madeni yaliyohusu Mashirika haya kwa *CHC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo ya Serikali kuhusiana na Muswada huu, isipokuwa tumetoa mapendekezo kadhaa ili kuuboresha muswada.

Kwanza, Kamati imefahamishwa kuwa baadhi ya Wafanyakazi wa *LART* walikwisha kulipwa mafao yao. Aidha, kwa vyombo vingine ambavyo shughuli zake zitahamishiwa *CHC* hapo baadaye Serikali ihakikishe kuwa Wafanyakazi watakaopoteza ajira zao, watalipwa haki zao ili yaliyotokea kwa waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yasijirudie tena. *(Makofi)*

Pili, Kamati imebaini kuwa Benki ya Posta inao mtandao mkubwa kama ilivyo Benki ya *NMB*. Hivyo, endapo Benki hii itajengewa uwezo inaweza kuja kuchangia kama Benki ya Maendeleo ya Wananchi. Kamati inapendekeza Serikali iangalie uwezekano wa kuipatia Benki hii jengo lililopo Mkwepu Dar es Salaam ambapo kwa sasa hivi wamepanga. Aidha, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Asasi za Serikali, Ofisi zao zipo kwenye majengo ya kupanga, mathalani *Public Procurement Regulatory Authority (PPRA), Gaming Board of Tanzania* na kadhalika. Hivyo, Kamati inapendekeza kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuzipatia Asasi hizo Ofisi katika majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha, namshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia H. Meghji, (Mb) na Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilika kwa kazi ya kuchambua Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa michango yao makini na ya kina iliyowezesha kuuboresha Muswada huu. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo: Mheshimiwa Adam K. Malima, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmoukh S. Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o na Mheshimiwa Elisa D. Mollel. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar S. Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Hamad R. Mohammed, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Mzee N. Zubeir, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo na Mheshimiwa Mossy S. Mussa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nataka kusema kwamba mpaka sasa ameomba kuchangia Mbunge mmoja tu.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MSEMAJI WA UPINZANI WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kutoa maoni kuhusu Muswada wa marekebisho ya sheria ya Kurekebisha na Kutwaa Mali na Madeni ya *NBC* kwa mujibu wa kanuni za Bunge Kanuni ya 43(5) (b)(c) na 70(2), toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha kwa uamuzi wake wa kuunda kampuni moja ambayo itajihusisha na ukusanyaji wa madeni na uuzaji wa mali za Makampuni ya Umma.

Kwanza, kwa kuunganisha Makampuni ya *ATHCO, SIMU 2000, LART* na kuzaliwa Kampuni mpya ya *Consolidated Holdings Corporation.* Aidha, ubunifu wake utaweza kuiokolea Serikali mabilioni ya Shilingi ambayo yalikuwa yakiingia katika mifuko ya watu binafsi.

Kambi ya Upinzani imetoa pongezi hizo kwa mantiki kuwa yapo mashirika kama Bima, Reli na mengine ambayo yatatakiwa kubinafsishwa. Tunashauri kuwa mashirika haya yatakapobinafsishwa mali zake ziwe chini ya *Consolidated Holdings*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani ina hoja kadhaa ambazo Serikali inatakiwa kuzitolea maelezo kwa faida ya walipa kodi wa nchi hii na Watanzania wote kabla ya Sheria hii mpya kupitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *ATHCO* mpaka sasa bado haijakusanya madeni yenye thamani ya Shilingi bilioni 27. Kwa mujibu wa sheria iliyoundwa na Bunge katika uanzishwaji wake, *ATHCO* haipo, kwani ukomo wa utendaji kazi wake ulimalizika rasmi Disemba, 2006. Kutokana na taarifa ya utendaji, inaonyesha kuwa miongoni mwa mali ambazo mpaka sasa bado zipo ni pamoja na nyumba zilizokuwa za *ATC* zilizopo Lusaka, Harare na Johannesburg.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa takwimu, inaonyesha kuwa *ATC* ilikuwa inamiliki nyumba zenye thamani ya Shilingi milioni 521 na imetolewa ufafanunuzi wa kila nyumba ipo wapi na thamani yake ni kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa historia ndiyo inayotoa maono ya mbele yatakavyokuwa, katika kikao cha bajeti cha mwaka uliopita Waziri kivuli wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji katika hotuba yake alihoji kuhusu nyumba ya *ATC* iliyoko Afrika Kusini, *Plot* 7/31 ambayo ipo *5th Avenue Edenvalley Johannesburg* ambayo ina thamani ya Shilingi milioni 68, lakini aliambiwa afute kauli yake kwamba alisema uongo. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoae taarifa kwa Wabunge kuwa ni kweli ama sio kweli kuwa nyumba hiyo imeuzwa kwa aliyekuwa au bado ni kiongozi wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inatoa ushauri kuwa, kwa kuwa sasa hivi *ATC* imefufuka na inamilikiwa na Serikali kwa asilimia mia moja na kwamba, kipindi kilichopita cha fedha Serikali ilitenga Shilingi bilioni kumi na tano kama mtaji wa

kuliendesha shirika hilo, nyumba na mali hizi zirejeshwe *ATC* ama kuziuza ili kukuza mtaji wa *ATC* kwa kuongeza Shilingi bilioni 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilifanya makosa toka mwanzo kuhusiana na suala la kuanzishwa kwa Kampuni ya Simu 2000. *SIMU 2000* ni Kampuni iliyoundwa na Sheria ya Makampuni *Cap. 212*. Kitu cha kuuliza ni kuwa, kwanini *SIMU 2000* haikutungiwa sheria na Bunge kuhusu utendaji wake wa kazi kama zilivyokuwa kwa Mashirika kama *LART, ATHCO* na kadhalika.

Kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Cap.212, lazima kampuni inayoanzishwa iwe na Wakurugenzi na idadi ya Wakurugenzi ni lazima ianzie Wakurugenzi wawili hadi 50. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilipe Bunge hili *MEMORUNDUM* na *ARTICLES OF ASSOCIATION* za Kampuni hiyo ya SIMU 2000 ili kuondoa dhana ya kuwa Kampuni hiyo iliundwa ili kuifilisi Tanzania na kuwanufaisha wakubwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Kampuni yetu ya Simu ya *TTCL* ni mali ya Watanzania kwa asilimia mia moja kama lilivyo Shirika la Ndege la *ATC*. Tunadhani yatakuwa sio makosa kama mali zilizokuwa za *TTCL* kabla ya ubinafsishwaji na ambazo bado zipo mpaka sasa zikawa chini ya mamlaka yake, badala ya kampuni kununua mali nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuhitimisha machache, tuliona kuwa ni bora tupate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Kambi ya Upinzani haina tatizo na uundwaji wa shirika jipya ambalo litafanya kazi kwa mashirika yote yanayobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa kama nilivyosema katika orodha ya wachangiaji, mimi nina Mbunge mmoja tu, Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa kuunganisha *Consolidated Holdings Article, LART* na *SIMU 2000.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa na mchango katika maeneo matatu tu. Eneo la kwanza kabisa, naunga mkono maelezo ambayo ameyasoma Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa maana ya kwamba tunaelekea kubinafsisha Shirika la Reli na tayari katika mpango wa kubinafsisha Shirika la Reli kuna mpango wa kuanzisha *Holding Company, Reli Limited* ambayo itasimamia mali zisizohamishika na madeni yote ya Shirika la Reli.

Sasa katika Muswada huu, nilitegemea kwamba *Consolidated Holdings* kama jinsi ambavyo tunaifanyia *amendment,* leo baada ya muda utakapokuwa umefikia, tungeweza kuweka *provision* ya kwamba Shirika lolote la umma litakalobinafsishwa kuanzia sasa liwe chini ya *Consolidated Holdings.* Sasa nimeangalia Muswada, hamna sehemu ya *provision* hiyo, kwa hiyo, matokeo yake ni kwamba tutajikuta tunabinafsisha

Shirika la Reli, tunaunda Kampuni nyingine au tunahitaji kuja kuunda tena Sheria nyingine kwa ajili ya hiyo Kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka kuchangia ni hili la suala zima la *ATC* na nyumba za *ATC*. Nyumba za *ATC* ziko maeneo mbalimbali. Maeneo ambayo Msemaji wa Upinzani Bungeni ameyataja ni yale machache tu ambayo yana matatizo. Kwa sababu taarifa tulinazo ni kwamba nyumba yetu iliyoko Harare ina matatizo, nyumba iliyopo Lusaka ina matatizo, watu ambao wamepangishiwa hamna maduhuli yanayokusanywa. Imekuwa ni kama mali ambayo haina mwenyewe na nyumba iliyoko Johannesburg ndiyo hiyo, jinsi ambavyo Msemaji wa Upinzani ametoka kuzungumza sasa hivi, inasemekana kwamba imeuzwa kwa Afisa wa Serikali, hatuna uhakika. Tunahitaji kupata ufafanuzi. Huyo Afisa ama yuko Serikali au hayupo Serikalini.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba mtupe haya maelezo ili tuweze kujiridhisha kwamba mali zetu ambazo kwa sisi vijana, wazazi wetu walizitolea jasho kuzianzisha, zinaweza zikapotezwa kirahisi namna hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nitapenda nipatiwe maelezo ni suala zima la *SIMU 2000.* Napenda niwakumbushe ambao ni watu wazima kidogo kwamba mara baada ya Shirika la Posta la Afrika Mashariki kuvunjwa, Tanzania ilikuwa katika wakati mgumu sana kwa sababu mali nyingi za Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki zilikuwa ama Uganda au Kenya. Kwa hiyo, tukaamua kwa uzalendo kabisa tena tukiwa ndani ya vita vya Kagera vya mwaka 1978 kuanzisha Shirika la Posta na Simu Tanzania.

Baadaye Shirika hili tukawa tumeligawa kuwa Kampuni ya Simu *TTCL* na Shirika la Posta. Ilipofikia wakati wa kubinafsishwa kwa *TTCL* tukawa tumeunda hiyo *SIMU 2000.* Kitu ambacho kinanitia mashaka na kinanifanya nione kwamba hapakuwa na nia njema ni kwamba, Makampuni yote ambayo yalikuwa ni *Holding Companies* yanatungiwa Sheria ya Bunge.

Ndiyo maana tuna *LART*, ndiyo maana tuna *Article*, ndiyo maana tuna *Consolidated Holdings* ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya mali zilizokuwa *NMB* na *NBC*. Lakini kwa Kampuni ya Simu ikaundwa kampuni binafsi ambayo ilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Makampuni kama jinsi ambavyo mzungumzaji aliyepita ametoka kuzungumza *Cap.212.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tupate maelezo kutoka Serikalini, ni sababu ipi iliyofanya mali ambazo, narudia tena kwa sisi ambao ni vijana, wazazi wetu walizitolea jasho tena baada ya vita wakahangaika, wakafungishwa mikanda kwa miaka 18, tukajenga Shirika, Shirika likawa linapata faida, tukaweka mitandao ya simu nchi nzima na majengo, inakuwaje Serikali ikaamua kuunda Kampuni binafsi ambayo mpaka sasa haifahamiki, Wakurugenzi ni akina nani na walipatikana namna gani? Haifahamiki leo hawa Wakurugenzi wana hisa kiasi gani na Serikali ina hisa kiasi gani?

Kwa hiyo, napenda niongezee nguvu kama jinsi ambavyo msemaji aliyepita amezungumza kwamba tunahitaji kabla ya kupitishwa kwa Sheria hii kwa maana ya

kwamba, leo ni jioni hii, tuone *memorandum* na *articles of association* za *SIMU 2000* ili tuweze kujua *subscribers* wa hiyo kampuni ni akina nani. Vile vile tupate hayo maelezo kutoka Serikalini kwamba ni kwa nini haikuundwa Sheria ya *Simu Holdings* kama jinsi ambavyo ilikuwa kwa *NDC* na mashirika mengine na mkaamua kuunda Kampuni binafsi?

Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo ambayo nilikuwa tunapenda tuyapate na naomba Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kweli atujibu kwa ufasaha bila kukwepesha, bila kuweka siasa kwa sababu moja ya jukumu letu sisi kama Bunge ni kuhakikisha kwamba tunalinda mali ya umma, tunalinda mali ambayo tumeitolea jasho mali ambayo tumeitengeneza kwa nguvu zetu, kwa sababu sisi wakati wanaondoka nchi hii hawakutuachia chochote. Kila kitu tulitengeneza sisi wenyewe. Sasa hii hali ya watu wachache kuja na kuamua kuuza kila kitu kwa kweli inatuweka katika wakati mbaya sana hasa sisi ambao ni vijana, tuna uhakika wa kuishi muda mrefu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemaliza. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa *Consolidated Holdings Corporation* kuongezewa nguvu kwamba wapatiwe madeni. Mimi moja kwa moja naunga mkono kwamba walichokifanya ni kitendo kizuri kabisa. *(Makofi)*

Tunasema hivyo kwa sababu utendaji wa *Consolidated Holdings Corporation* katika kukusanya madeni wamekuwa majabali, wamefanya kazi nzuri, ndiyo maana wanaongezewa na kazi nyingine zilizokuwa za *LART* na hao wenzetu wa *Simu 2000 Limited* ambao itaisha muda wake siyo muda mrefu. Lakini pamoja na kushukuru kwa kazi nzuri alizozungumzia Mheshimiwa Naibu Waziri, nilikuwa nataka nichangie kidogo tu kwamba haya madeni na hizi kesi ambazo zipo *LART* ni madeni na kesi ambazo ni *sensitive*.

Kwa hiyo, ninachoshauri hapa ni kwamba tuwe na uangalifu wa kutosha tunapohamisha yale madeni kutoka *LART* kwenda *CHC,* yaani *Consolidated Holding Corporation,* tuwe waangalifu tusije tukajiingiza sehemu ambayo tutapata hasara kubwa zaidi. Kwa sababu ni kweli tutawalipa hawa wafanyakazi ambao walikuwa *LART* tunawapa hela, yaani marupurupu yao wafanyakazi yaani waondoke haraka haraka. Lakini wale watu walikuwa na vitu vingi sana ambavyo vingekuwa msaada mkubwa kwa *Consolidated Holding Corporation*.

Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwamba pamoja na kwamba kweli tutawalipa wote, lakini isionekane tunawaondoa wote kwa sababu mkataba umekwisha walau angebakia hata mmoja, hata Mwanasheria wao au mtu anayefahamu vizuri kuhusu yale madeni isionekane tunafanya haraka haraka, kwa sababu hii ya kusema tunakurupuka tunavunja haraka haraka itatuletea athari kubwa zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwa wenzangu ambao mlikuwa mnahusika na kutoa hilo wazo au kuona kwamba kweli muda

umekwisha *LART* na hawa *Simu 2000 Limited* kwamba watahamishiwa kule *CHC*. Tuwe waangalifu kidogo, itatuletea madhara baadaye.

Kwa sababu hata hao wenzetu wa *LART* walikuwa wanafanya kazi nzuri sana sana. Hata *Simu 2000 Limited* walikuwa wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, kukurupuka kwamba tufute wote kabisa tusiache hata mtu mmoja ambaye anajua historia ya yale madeni, naona itatuletea madhara.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka nichangie kwamba kwamba uamuzi huu ni mzuri unaweza ukaliletea Taifa tija kubwa. Lakini tusiwaondoe wote *as if* muda umekwisha, basi waondoke haraka haraka itatuletea madhara. Kwa sababu naelewa kuna kesi ambazo ziko *sensitive* kule *LART* na kule *Simu 2000 Limited.* Kwa hiyo tuwe waangalifu kwa hilo.

Niwapongeze sana kwa kazi nzuri wenzetu wa *Consolidated Holding* kufanya kazi vizuri mpaka wanaaminiwa kwamba muda utakapokwisha wataongezewa. Kwa kweli na mimi nawapongeza sana. Sina mengi, nikushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika Muswada huu wa *Re-Organization of NBC* na kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zangu ni kwamba vyombo hivi hususan *LART* iliundwa na Serikali ili kuvipa nafasi mabenki yale *National Bank of Commerce* na kwa kweli vile vile pamoja na *CRDB* na *TIB* wakati zilipokuwa *re-capitalized*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Benki hizi katika utaratibu wa zamani wa kuendesha vyombo vyetu vya fedha, nasema utaratibu wa zamani ni kwamba vyombo vya fedha viligeuzwa kama sehemu ya Serikali Kuu na wakati mwingine Chama Tawala inapokuja katika kuelekeza mikopo iende wapi. Kwa hiyo, mikopo iliyotolewa na mabenki yetu haya *NBC*, *CRDB, TIB* baadhi ya mikopo hiyo ilikuwa ni ya kisiasa zaidi kuliko ya kibiashara na uchumi. Matokeo yake ni kwamba Benki hizi zilipokuja kufanyiwa *diagnostic study* ya *capital structure* zao ukilinganisha na *portfolio* zao ilikuja kukutwa kwamba kile tunachokiita kwa lugha ya kigeni *none performing assets,* yaani mikopo ambayo hailipiki ilikuwa ni mingi sana.

Kwa kweli katika wakati ule, mikopo hiyo ambayo ilikuwa hailipiki ilizifanya Benki zile ziwe kwa lugha ya kigeni *insolvent* yaani mufilisi. Sasa kilichofanyika ni nini? Serikali ilihamisha mikopo ile ikaipeleka *LART* ili *LART* iifuatilie. Lakini haikuishia hapo, Serikali vile vile ilitoa dhamana za muda mrefu takriban miaka 20 kwa thamani ya madeni yaliyohamishwa kutoka kwenye mabenki hayo kwenda *LART.* Hapa ndipo ninapotaka kutilia mkazo kwamba madeni hayo yaliyohamishwa katika vitabu vya mabenki haya yalihamishwa kupelekwa *LART* ili yafuatiliwe lakini ili vitabu vya mabenki hayo viweze ku-*balance* na *capital base* ya hayo mabenki iweze kuwepo kwa

ajili ya hayo mabenki yafanye kazi Serikali ilitoa dhamana za muda mrefu kama nilivyosema takriban miaka 20.

Ndani ya miaka hii 20 Serikali inalipa, ina-*service* hizo dhamana kwa kulipa *principal* pamoja na riba. Matarajio ya Serikali ilikuwa ni kwamba *LART* ingekusanya madeni yale kisha yangeingia katika Mfuko wa Serikali ili kuiwezesha Serikali ku-*service* zile dhamana za muda mrefu zilizotolewa kwa mabenki hayo. Hapa ndipo ninapotaka kutilia mkazo kwamba matarajio yalikuwa *LART* watafanya kazi nzuri, watakusanya madeni, yakija Serikalini sehemu ya yale madeni yaliyolipwa yatatumika ku-*service* zile dhamana zilizotolewa ili ku-*re-capitalize* kuzijenga upya hizi Benki zetu.

Sasa takriban miaka 10 imepita bado *LART* hawajatimiza kazi waliyopewa. Kwa hiyo, kinachotokea ni nini? Kinachotokea ni kwamba ulipaji wa zile dhamana za Serikali za muda mrefu zilizosaidia kujenga upya *capital base* ya mabenki yetu zinalipwa na walipa kodi Watanzania tukiwa na sisi miongoni mwao. Tunalipa kupitia kodi zetu kuipa nguvu Serikali kulipia zile dhamana za muda mrefu. Swali ni kwamba, kwa nini inachukua muda wote huu kukusanya madeni ambayo wakopaji wanajulikana, dhamana waliweka, tunaambiwa bado kuna kesi. Kesi miaka 10 inakwenda, hizi kesi haziishi? Sasa hapo ndipo kwenye tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku, nadhani haya madeni yatakuja kuwa *written off,* sisi Watanzania tubebeshwe huu mzigo kama ambavyo tunaubeba sasa wa ku-*service* hizi dhamana ambazo Serikali ilitumia kujenga upya uwezo wa haya mabenki yetu. Kwa mustakabali huo ninaunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwa matarajio kwamba ndiyo itakayowezesha Serikali kuendelea kuyafuatilia madeni haya mpaka yapatikane.

Lakini nataka nitie msisitizo, tusifanye dhihaka katika kuyafuatilia madeni haya na kule kwenye kesi, hizi kesi ziamuliwe basi, kuna tatizo gani? Kuziamua kesi hizi ni kwamba, wewe ulikopa ukaweka dhamana, hulipi dhamana, ichukuliwe iuzwe. Lakini ndiyo matatizo ya nchi yetu. Tunalea hata wakopaji wasiolipa. Ndiyo tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Mimi nilikuwa na machache tu ya kuzungumza ambayo nafikiri ni ya msingi sana Watanzania waelewe. Kwa sababu huu ni mfululizo au mtiririko wa ubinafsishaji ambao umekuwa ukiendelea kwa mashirika mbalimbali na kwa taratibu ambazo zinaonekana kwamba ni za kibepari. Mimi sina ugomvi na ubepari kwa sababu sisi hatukuugundua. Ulikuwepo lakini nchi yetu ilikuwa inafuata mfumo wa ujamaa kwa kujaribu kuharakisha maendeleo zaidi na mpaka leo Katiba yetu imeandika kwamba Tanzania ni nchi ya Ujamaa.

Sasa kwa kuwa Tanzania ni nchi ya ujamaa na utaratibu wa ujamaa unafahamika. Ujamaa ndiyo unakwenda na mapinduzi, yaani *revolution* na vile vile unakwenda na

kutaifisha mali za mabepari na baada ya kutaifisha mali za mabepari tunaanza kufuta tabaka za wale mabepari na kushughulika na uchumi ambao unaangalia wakulima na wafanyakazi na hiyo ndiyo misingi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Tumeendelea na ubinafshaji, mashirika yote yaliyoanzishwa wakati wa Mwalimu yanaendelea kubinafsishwa na karibu yanaisha, lakini hatujatangaziwa rasmi kwamba sasa tumeacha mfumo wa ujamaa tuna-*practice* mfumo wa ubepari. Sijui ni kwa nini Serikali inaona haya kutuambia moja kwa moja kwamba sasa tumeacha ujamaa tuna-*practice* ubepari? Kwa sababu ubepari nao una taratibu zake na taratibu zake ni pamoja na *primitive accumulation of capital* na ile *capital* inakuwa *invested* na *priority* inawekwa kama ni *industrialization* au kama ni ...!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wangwe, jadili Muswada!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ndiyo huo. Namalizia Mheshimiwa Naibu Spika kwa kusema ya kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Muswada huu unahusika na kuacha Makampuni madogo madogo yaliyokuwa yanakusanya mali za makampuni yaliyoundwa upya na kuweka katika chombo kimoja. Sasa ubepari unaingia wapi hapa?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Sawa Mheshimiwa Naibu Spika, nakubali. Mimi nafikiri nimeshauliza swali, ni kwamba nchi hii inaendeshwa kwa misingi ya kijamaa au kibepari? Watanzania wajue moja! Hilo ndilo swali langu. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Ukiangalia, bahati mbaya nimesema mimi, Waheshimiwa Wabunge mnapokaa kwenye Viti vingine sisi tuna *Board* hapa, Mheshimiwa Wangwe alipokuwa anazungumza alikuwa anaonekana Mheshimiwa Hemed ndiyo anaongea. Kwa hiyo, kila mtu akae kwenye Kiti chake. Kwa hiyo, *card* inasema ni Hemed!

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumia *card* yake maana ya kwangu nimeisahau. Samahani. *(Kicheko/Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE: KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 23 mwaka 2003/2004 hapakuwa na ukame. Sababu zipi nyingine?

Fungu 88 hapakuwa na Bajeti ya sherehe za uhuru? Hazikuchangiwa? *Statement of excess* ilipaswa kuja kwanza na kuidhinishwa na Bunge kabla ya Muswada. Mmekiuka sheria ya fedha kifungu cha 19(1)(2).

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote inasikitisha muda uliochukua kuwasilishwa hapa Bungeni matumizi ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujachukua hatua madhubuti juu ya matumizi na matumizi ya ziada yazingatie taratibu sahihi za Fedha, tutaendelea kila siku kupitisha ama hata kukataa kwa matumizi ya miaka mingi. Tatizo ni nini hadi hesabu zikachukua muda mrefu kama hizi za mwaka 2003/2004? Naomba nipate maelezo na ufafanuzi wa ucheleweshaji wa karibu miaka mitatu hivi.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni vyema tukawa makini sana katika makadirio yanayoletwa Bungeni kuepuka matumizi ya ziada. Matumizi ya ziada iwe katika hali ambayo haikuweza kutaribiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kwa mfano Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam kilitumika katika sherehe za uhuru 2003. Ni vyema matumizi ya ziada yaelekezwe kwenye maendeleo badala ya sherehe ambazo nina mashaka sana na matumizi yake na isiwe inaingia katika mifuko ya watu, sherehe zote ziheshimu fedha zilizotengwa katika Bajeti na kusiwepo matumizi ya ziada kwa sherehe. Sherehe muhimu kama uhuru zitengewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Sasa nitamwita Mtoa Hoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kupata michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa ujumla kumekuwa na michango sita. Lakini vilevile kumekuwa na michango miwili ya maandishi ambayo imetoka kwa Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila - Mbunge wa Kalambo na nyingine imetoka kwa Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati najibu hoja nyingine, nitazichanganya. Kwanza nianze kwa hoja mbili zilizotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi. La kwanza lile la mafao. Nataka kukubaliana na yeye kwamba mafao yatalipwa kwa wakati. Kwanza wafanyakazi wa *LART* wameshalipwa na vile vile wafanyakazi wa *ATHCO* wameshalipwa, wachache waliobakia watalipwa mara tu baada ya kukabidhi zile mali kwa *Consolidated Holiding Corporation* na wote wa *Simu 2000 Limited* watalipwa mara tu mali na madeni ya kampuni hiyo vitakapokuwa vimekabidhiwa kwa *CHC*.

Hoja ya pili iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Benki ya Posta kupewa majengo. Hoja hii imerudiwa tena na Wabunge kadhaa ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Mwambalaswa na Mheshimiwa Mwananzila. Nataka kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Hazina tumeshapokea maombi kutoka Benki ya Posta wakiomba kupewa jengo lile. Mazungumzo yanafanyika na kuna dalili kwamba wanaweza wakakabidhiwa lile jengo kabla ya mwisho wa mwezi wa Sita. *(Makofi)*

Wa pili, alikuwa Mheshimiwa Halima Mdee, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani. Nitapenda kuunganisha majibu ya hoja zake pamoja na hoja za Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa sababu zinafanana. Ya kwanza ilikuwa ni mashirika mengine yatakayobinafsishwa mali zake zikabidhiwe *Consolidated Holding Corporation.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba, Muswada umetamka wazi kwamba kwa sasa utashughulikia *LART*, *ATHCO* na mwezi Desemba, *Simu 2000 Limited* lakini baadaye mashirika mengine. Kwa mfano, *Tanzania Railways Corporation* na mengine ambayo yatabinafsishwa ikiwa pamoja na hilo la Bima mali zake zinaweza zikahamishiwa kwenye Shirika hili. Kwa hiyo, kuna kipengele kabisa tumekiweka kwamba huko baadaye mashirika yote ambayo yatabinafsishwa shughuli zake badala ya kuundiwa shirika lingine na kuongeza gharama zitahamishiwa kwenye *Consolidated Holding Limited*.

Lingine ambalo linafanana pia ni kuhusu nyumba zilizoko Lusaka, Harare na Johannesburg. Nataka kusema kwamba tumeyasikia na tutayafanyia kazi na kabla ya *Consolidated Holding Corporation* hawajakabidhiwa tutakuwa tumetafiti ukweli wa haya yote yaliyosemwa, kama ni ya kweli Serikali itayafanyia kazi na kama kuna nyumba Johannesburg aliuziwa kiongozi wa Serikali, Serikali itafanya utafiti na nina hakika Serikali itachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi kuahidi hapa kwa sababu yamesemwa na sisi kama Serikali hatuna hakika nayo. Ni vizuri yakafanyiwa kazi na kama ni kweli Kiongozi wa Serikali aliuziwa nyumba ya *Air Tanzania Corporation* Johannesburg, Bunge litataarifiwa kwa wakati muafaka hatua ambazo Serikali itakuwa imezichukua. *(Makofi)*

Kuhusu *Simu 2000 Limited* kuundwa kama kampuni binafsi badala ya Shirika, huu ni utaratibu wa kawaida. Kuna aina mbili za Kampuni za Serikali. Kampuni zilizoundwa na Sheria ya Makampuni *(Cap. 212)* au *Public Corporation Act*. *Simu 2000 Limited* iliundwa chini ya *Cap. 212*. Kuhusu MEMARTS za Simu 2000 Limited nimewaagiza wataalamu wazitafute na kabla hatujamaliza kikao hiki, Waheshimiwa Wabunge wataletewa wazione. *(Makofi)*

Suala la Mheshimiwa Stanley Yono, kwamba madeni ya *LART* ni *sensitive,* nakubali kwamba ni kweli ni *sensitive* na mengi ni makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wafanyakazi wachache wa *LART* kuhamishiwa *Consolidated Holdings* tulijaribu kulitazama hilo, lakini kwa sababu kazi zinazofanywa na *Consolidated Holdings* na zilizokuwa zinafanywa na *LART* zinafanana, tuliona kwamba wale wafanyakazi waliopo pale *Consolidated Holdings* wanatosha badala ya kuchukua wale wafanyakazi wengine waliopo *LART* au *ATHCO*. Lakini pia wale wafanyakazi waliokuwa *LART* wengi wao kwa kweli walikuwa ni watu wazima.

Kwa hiyo, ingekuwa ni kuchukua mzigo wa watu ambao tayari wanakaribia kustaafu ukawapeleka *Consolidated Holdings* ndiyo maana wamelipwa haki zao zote na wamestaafu. Lakini ikitokea kwamba *Consolidated Holdings* kuna tatizo la *staff* Hazina au Serikali kwa ujumla wake itafanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba tunapata wafanyakazi na *Consolidated Holdings* inaimarishwa.

Mheshimiwa Siraju Kaboyonga amezungumzia mengi lakini nadhani kubwa ilikuwa ni kesi za siku nyingi na kwa nini kesi haziishi kusikilizwa na Mahakama?

Waheshimiwa Wabunge, sote tunafahamu kuwa kuna mihili mitatu, kuna sisi hapa Wabunge ambao tunatunga sheria, kuna Serikali ambayo inatekeleza hizo sheria na kuna Mahakama ambayo inatafsiri sheria. Sasa Mahakama wamejiwekea utaratibu wao wa kufanya kazi, *LART* inapeleka mashtaka, Mahakama inaweza ikachukua miaka miwili kuamua kesi moja.

Kwa bahati mbaya Serikali hatuwezi kumlazimisha Jaji Mkuu kwamba kesi tuliyowapelekea iamuliwe katika muda fulani. Nadhani hiyo ni sababu mojawapo ya kesi kuchelewa, kwa kweli wanajitahidi kupeleka hizo kesi Mahakamani lakini Mahakama zinafanya kazi zake kwa utaratibu ambao wamejiwekea na Serikali inaiheshimu Mahakama kama muhimili wa tatu na tusingependa kuingilia maamuzi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tutajitahidi kuhakikisha kwamba, wanasheria wa kutosha wanapatikana ili kuhakikisha kesi zilizopo zinapelekwa Mahakamani. Natunaimani kwamba katika kipindi hiki cha miaka minne, nyingi ya kesi hizi zinaweza kuwa zimekamilishwa.

Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe nadhani hoja yake ilikuwa nje ya Muswada uliokuwa Mezani, kwa sababu kusema kwamba nchi hii sasa ni ya ubepari au ya ujamaa na kuhusisha na kupeleka shughuli za *LART Consolidated Holdings,* kwa namna fulani nafikiri kulikuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja. Kwa hiyo, kwa kweli sina jibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru wachangiaji waliozungumza, kama nilivyosema awali ni pamoja na Mwenyekiti ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mheshimiwa Stanley Yono S. Kevela na Mheshimiwa Chacha Wangwe.

Waliochangia kwa maandishi, kama nilivyowataja mwanzoni ni pamoja na Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kutoa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara wa Mwaka 2007 *(The National Bank of Commerce (Reorganisation and Vesting of Assets and Liabilities)***
***Bill 2007 Cap. 404))***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

**MHE. ZITTO Z. KABWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ibara ya pili ya Muswada huu. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri sana, kuhusiana na *Simu 2000 Limited* na *ATHCO*.

Kuna kitu kimoja ambacho napenda Mheshimiwa Naibu Waziri, akiweke wazi zaidi. Alituambia kwamba, Sheria hii ime-*provide* kwa Shirika lingine lolote, nimeangalia na *ATHCO* ambayo ilipaswa hilo liwepo lakini hakuna. Kwa hiyo, naomba maelezo katika hili kwa Mashirika ambayo yatakuja kubinafsishwa baadaye, hamna *provision* ambayo inaweza ikaifanya Serikali kwa mfano, ikaingiza *Rail Holdings* chini ya *Consolidated Holdings* au shirika litakaloundwa kwa ajili ya *assets* za bima? Naomba maelezo katika hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa mtoa hoja anasema wakati anajadili, alikuwa ameshauri kwamba kusiundwe tena mashirika mengine ya *holding* kwa mashirika yanayokuja kama reli au bima. Wewe ulipojibu ulisema ipo *provision* humu ndani inayoweza kuruhusu hayo mashirika kuingizwa, sasa anauliza kifungu hicho kipo wapi katika Sheria hii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika maelezo yetu katika Muswada tumeweka wanasheria, walitushauri kwamba shirika ambalo halijabinafsishwa kabisa, huwezi ukalitaja kwenye sheria kwamba na shirika fulani nalo litakapobinafsishwa, *assets* zitahamishiwa kwa *Consolidated Holdings.*

Tulichosema ni kwamba, kwa sasa hivi kuna *LART* tayari imeshakufa imehamishiwa huku, *Simu 2000 Limited* maamuzi yameshachukuliwa tayari kwamba ifikapo Desemba uhai wa *Simu 2000 Limited* utakuwa umekwisha. Kwa hiyo, lile linajulikana wazi, mengine yatakayokuja huko mbele ya safari ndiyo tunasema kwamba, yakija yatapelekwa *Consolidated Holdings.*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida na katika Bunge wakati mwingine tunaelimisha tu. *Section 2* ile ibara ya 2(b) ambayo ndiyo inaelezea zile *residue assets* na inataja mashirika husika, pale baada ya

*Simu 2000 Limited* ilitakiwa ifuate *"and any other," not necessarily mentioning specific company, just say, "and any other,"* ambayo Serikali itaona inafaa.

Sasa kwa kuwa tayari *schedule of amendements* imeshakuja, naomba tupate *commitment* ya Serikali kwamba katika siku chache zijazo, labda Bunge lijalo tutapata *amendment* ndogo kama sehemu ya *amendment* kuonesha hii kwamba *and any other*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nadhani umeipata hoja hiyo kama ni ya lazima kufanya hivyo, hakuna ugumu kwa Serikali kusema hivyo hapo, kama kuna ugumu fulani wa mazingira kwamba hayo mashirika labda hayajulikani, basi ushauri ndiyo unakubalika, sasa ni lipi Mwanasheria?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hoja ya Mheshimiwa Mbunge, tutaangalia kama kuna haja ya kufanya *amendment* kwenye hiyo Sheria, tutafanya hivyo. Nashukuru sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Kifungu cha 4

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niondolewe wasiwasi kwenye kifungu (d)(i), (ii) na (iii), kile hakioneshi *CRDB* na *TIB*, kwa uelewa wangu ni kwamba, haya mabenki nayo *assets liability* zao zilikuwa zinashughulikiwa na *LART.* Hapa inaoneshwa *NBC* na *NMB*, lakini *CRDB* na *TIB* hazioneshwi.

Nataka tu kuelewa kuwa je, kuachwa kwake ilikuwa ni *oversight* au ndani yake humo zitashughulikiwa vilevile, kwanini isiwe *explicitly?*

**MWENYEKITI:** Nadhani umeelewa hoja, Mheshimiwa wakati anajadili alisema kwamba kuwepo kwa *LART* kulitokana na madeni sugu yaliyokuwa katika mabenki ya *CRDB* na mabenki mengine ambayo yalifanya yale mashirika kama yamekufa kabisa na kupelekwa *LART* ili yaweze kufanya kazi; sasa hapa inaonekana *NMB*; je, *CRDB* haihusiki?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA MKULO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yaliyokuwa *LART* yalikuwa ya aina nyingi. Ni kweli kulikuwepo madeni ya *TIB, CRDB* na hata madeni ya makampuni mengine binafsi ambayo yalishindwa kukusanya madeni yao yakapelekwa kule.

Pale ambapo hatukuonesha ni kwamba, mfano Kampuni ya *TIB* ilikuwa imepelekwa *LART,* ina maana kwamba lile deni limeshalipwa, si kwamba madeni yote hayajalipwa, madeni mengi yameshalipwa.

Sasa *NMB* yako madeni ambayo bado hayajalipwa *specifically,* lakini kama kuna chochote kile, ndiyo maana tumeonesha pale *LART* kwamba kama kuna chochote ambacho kimebaki *residue,* kipo chini ya *LART*. Lakini kama hatukuonesha *CRDB* wala *TIB* ni kwamba madeni yao ambayo yalikuwa yamepelekwa *LART* yameshalipwa au kesi zao zimeshakwisha. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya BungeZima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 5

*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kutoa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara yaani *(The National Bank of Commence (The Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) Bill, 2007))***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kutoa Mali na Madeni ya Benki ya Taifa ya Biashara *(The National Bank of Commence (Re-Organization and Vesting of Assets and Liabilities) Amendment Act, 2007*, kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake. Hivyo, naomba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2007 *(The Supplementary Appropriation Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukuomba radhi wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kutofika kwa wakati, kuwasilisha Muswada huu ninaotaka kuuwasilisha kwa naiba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Ziada ya Shilingi 23, 576,131,613 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004, sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unawasilishwa kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura Namba 348. Chini ya kifungu hiki, Serikali inaweza kufanya matumizi ya ziada kuliko yale yaliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo, kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo za dharura na baadaye Bunge kuhalalisha kwa utaratibu wa kupitisha Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha ya Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha za ziada kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina *(The Supplementary Appropriation Bill)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ulijadiliwa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, iliyokutana Mjini Dar es Salaam, mnamo tarehe 27 Machi, 2007. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, kwa kujadili na kuutolea maoni Muswada huu. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Wizara imezingatia kwa dhati michango ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada huu.

Madhumuni ya Muswada huu ni kuliomba Bunge kuidhinisha matumizi ya ziada yaliyofanywa na Serikali ya shilingi 23,579,131,613 kugharamia mahitaji mbalimbali muhimu ikiwa ni pamoja na Serikali kupata huduma na vifaa zaidi kutoka kwa wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu, matumizi ya aina hii yanapaswa kukaguliwa na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na baadaye kuwasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, kwa ajili ya kujadiliwa na baadaye kuwasilishwa Bungeni. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali, ilijadili na kupitisha hesabu za Serikali kwa Mwaka 2003/2004 mnamo tarehe 27 Oktoba, 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyobainishwa kwenye hati ya matumizi ya ziada iliyoambatanishwa na Muswada huu, sehemu kubwa ya matumizi haya yalitokana na wahisani mbalimbali kuipatia Serikali msaada wa vifaa na huduma zaidi ya vile

vilivyokadiriwa na kujumuishwa katika bajeti ya Serikali iliyoidhishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

Serikali inafanya mashaurianao na wahisani ili kuweka utaratibu mbadala, ambao badala ya wahisani kuchangia mradi mmoja mmoja au programu moja moja, wachangie kwa utaratibu wa *general budget support*, ambapo chini ya utaratibu huu, misaada mingi ya wahisani itajumuishwa katika bajeti ya Serikali na hivyo kupunguza utaratibu huu wa matumizi yanayofanyika nje ya bajeti inayopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kwa kifupi kutoa maelezo ya matumizi haya ya ziada fungu kwa fungu kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali: Kiasi cha shilingi milioni mia tatu tisini na nne, mia moja ishirini na nane elfu, mia sita arobaini na sita kiligharamia mahitaji ya dharura ya *TANESCO*. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba katika kipindi hiki nchi yetu ilikabiliwa na ukame mkubwa na kuilazimu Serikali kufanya matumizi zaidi kukabiliana na dharura hii.

(ii) Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani: Kiasi cha ziada cha shilingi bilioni ishirini na mbili, milioni nne, mia moja themanini na moja elfu na mia tatu na tano kilitumika kutokana na wahisani kuleta vifaa na huduma kama vile magari na pikipiki kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Polisi; vyakula, madawa, nguo, maturubai na samani mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya wakimbizi, ambavyo havikuwemo katika Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka husika.

(iii) Fungu 57 – Mkoa wa Mara: Kiasi cha shilingi milioni mia moja arobaini, mia saba sabini na tisa elfu na mia tano na moja kilitumika kulipia gharama za uendeshaji magari na posho za kujikimu, pamoja na kupokea samani na vifaa kutoka kwa Wahisani.

(iv) Fungu 84 – Mkoa wa Singida: Kiasi cha shilingi milioni mia moja sabini na mbili, mia nane sitini na tano na hamsini kilitumika kutokana na mapokezi ya samani na vifaa vilivyotoka kwa wahisani.

(v) Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam: Kiasi cha shilingi milioni mia moja themanini na nane, mia tano kumi na tisa elfu na mia mbili thelathini na tisa kilitumika katika Sherehe za Uhuru za mwaka 2003.

(vi) Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa: Kiasi cha shilingi milioni sita, mia saba themanini na saba elfu kilitumika kufidia ongezeko la mishahara.

(vii) Fungu 95 – Mkoa wa Manyara: Kiasi cha shilingi milioni mia sita sabini na moja, mia nane sabini elfu na mia nane sabini na moja kilitumika kwa sababu wahisani walileta fedha zaidi ya zile zilizotengwa katika Bajeti. Fedha hizo zilitolewa na Serikali ya Sweden.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuhalalisha matumizi haya ya ziada, nje ya makadirio yaliyopitishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2003/2004, ambayo tayari yamekwishatumika, ili kuiwezesha Serikali kuweka kumbukumbu sahihi ya vitabu vya hesabu. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi, baada ya kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa Matumizi ya ziada bila idhini *(Supplementary Appropriation Bill, 2007 (For Financial Year 2003/2004),* kwa Mujibu wa Kanuni ya 70(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kutoa maoni ya Kamati, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa ushindi wa kishindo, alioupata Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura katika Uchaguzi Mdogo uliofanyika katika Jimbo la Tunduru. Ushindi huo ni kielelezo sahihi kwa Wapinzani wa Chama cha Mapinduzi kuwa wananchi wana imani kubwa kwa Serikali ya Awamu ya Nne katika utekelezaji wa Sera za CCM. Karibu katika Bunge hili Tukufu, tuwawakilishe wananchi waliotupa sote dhamana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeelezwa kuwa Muswada huu kwa ujumla wake, unalenga kuhalalisha matumizi ya jumla ya Sh.23,579,131,613 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu unawasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348 kikisomwa pamoja na ibara 137(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ambapo Serikali inaweza kufanya matumizi ya ziada kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na baadaye Bunge kuhalalisha matumizi hayo kupitia Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Ziada ya Fedha za Serikali *(The Supplementary Apprppriation Bill).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu imeridhika na maelezo ya matumizi hayo ya ziada, baada ya kupitia mafungu hayo kama ifuatavyo:-

(i) Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali: Kiasi cha Sh.394,128,646 kiligharamia mahitaji ya dharura ya *TANESCO* yaliyosababishwa na ukame mkubwa ulioikumba nchi yetu katika Mwaka wa Fedha 2003/2004, ambapo sisi sote ni mashahidi wa tatizo.

(ii) Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi: Kiasi cha ziada cha Sh.22,004,181,305 kilitumika kutokana na wahisani kuipatia Wizara hiyo

vifaa na huduma ambavyo havikuwemo katika Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka huo.

(iii) Fungu 77 – Mkoa wa Mara: Kiasi cha Sh.140,779,501 kilitumika kulipia gharama za uendeshaji magari na posho za kujikimu, pamoja na kupokea samani na vifaa kutoka kwa Wahisani.

(iv) Fungu 84 - Mkoa wa Singida: Kiasi cha Sh.172,865,050 kilitumika kutokana na mapokezo ya samani na vifaa vilivyotoka kwa wahisani. Aidha, kiasi hicho ni zaidi ya makadiriio yaliyoidhinishwa.

(v) Fungu 88 - Mkoa wa Dar es Salaam: Kiasi cha Sh.188,519,239 kilitumika katika Sherehe za Uhuru za Mwaka 2003.

(vi) Fungu 89 - Mkoa wa Rukwa: Kiasi cha Sh.6,787,001 kilitumika kufidia ongezeko la mishahara.

(vii) Fungu 95 - Mkoa wa Manyara: Kiasi cha Sh.671,870,871 kilitumika kwa kuwa wahisani walileta fedha zaidi ya zile zilizotengwa katika Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, Kamati yangu inakubaliana na mapendekezo ya Serikali, isipokuwa tumetoa mapendekezo kadhaa ili kuboresha mapendekezo haya. Kamati ilibaini kuwa matumizi haya yamechukua muda mrefu. Mwaka 2003/2004 hadi 2006/2007, ni takribani miaka minne hadi kuletwa Bungeni kuomba yahalalishwe. Kamati inasisitiza kuwa, pale inapotokezea kuwepo kwa matumizi ya ziada, Serikali isichelewe kuwasilisha maombi yake Bungeni, kwa sababu matumizi hayo yameruhusiwa kwa mujibu wa Kifungu cha 19 cha Sheria za Fedha za Umma, pamoja na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, ibara ya 137(3).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwa katika Bajeti ya Serikali, takriban asilimia 41 inatokana na wahisani. Hivyo, katika kutoa misaada *(General Budget Support),* Serikali inashindwa kujua kwa uhakikika, kiasi cha fedha au vifaa vitakavyotolewa na wahisani hao. Matokeo yake baadhi ya Wafadhili wamekuwa wakitoa misaada yao bila ya kupitia katika utaratibu wa *General Budget Support.* Hivyo, misaada hiyo inaonekana ni matumizi ya ziada kwa sababu fedha au vifaa hivyo, vinakuwa havikuingizwa katika Bajeti ya Serikali.

Kamati inaisisitiza Serikali kuwa iendelee na juhudi zake za kuwashawishi baadhi ya wahisani kupitisha misaada yao katika utaratibu wa *General Budget Support,* hii itasaidia Serikali kupanga vizuri mipango yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii. Aidha, namshukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Zakia H. Meghji, kwa ushirikiano anaoutoa kwa Kamati yangu na kufanikisha kukamilika kwa kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia niwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa michango yao ya kina iliyowezesha kuboresha Muswada huu. Naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mwenyekiti, Mheshimiwa Adam K. Malima, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mheshimiwa Charles M. Kajege, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Devota M. Likokola, Mheshimiwa Clemence B. Lyamba, Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed na Mheshimiwa Elisa D. Mollel. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Felix C. Mrema, Mheshimiwa Omar Sheha Mussa, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa Hamza A. Mwenegoha, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Dr. Mzeru O. Nibuka, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Esther K. Nyawazwa, Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto na Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE (K.N.Y. MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 70(2), Toleo la 2004 na kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na Muswada wa kupata idhini ya Bunge ya nyongeza ya matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli kuwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali inafanya kazi zake moja kwa moja na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kufanya mahojiano ya moja kwa moja na *Accounting Officers* wa Serikali. Aidha, inapata nafasi ya kupitia taarifa ya miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na wahisani *(Performance Appraisal)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, sehemu ya tatu, kifungu cha 19(1) (a), (b) na (c), inaeleza kwamba wakati Serikali ikiwa inafunga mwaka wa fedha, ikigundulika kwamba pesa zimetumika kuzidi makadirio yaliyowekwa ama kwa matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge, taarifa ya pesa husika ya ziada ambayo haikupangiwa inatakiwa iletwe Bungeni.

Kipengele kidogo cha pili cha sheria husika 19(2) kinaeleza kwamba, kama Bunge likikubaliana na matumizi ya ziada, matumizi husika yatajumuishwa katika Muswada wa Matumizi ya ziada kama ambavyo imeletwa leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka Mwaka wa Fedha 2003/2004, Bunge limefanya takribani mikutano 16, hiki ni kipindi kirefu. Serikali kwa muda wote imekaa kimya mpaka Kamati ilipowasilisha taarifa yake na inachokifanya sasa ni kuleta Muswada wa Matumizi ya Ziada kabla hata ya kuleta taarifa ya matumizi ya ziada Bungeni.

Kambi ya Upinzani inaona kuwa, Serikali kwa njia moja ama nyingine, inasababisha Bunge kushindwa kufanya kazi yake ya Kikatiba ya kupitisha matumizi ya pesa za walipa kodi, kwa kukataa kuleta maombi ya matumizi ya fedha nje ya zile zilizopitishwa rasmi katika bajeti. Aidha, Kambi inamtaka Waziri kwa niaba ya Serikali, alitake Bunge radhi kwa makosa hayo yanayotendeka na yasirudiwe tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunataka Bunge lielezwe kuhusiana na *reallocation* ya fedha. Kambi ya Upinzani inafahamu kwamba, Mheshimiwa Waziri ana uwezo wa kufanya *reallocation*, lakini ni muhimu Bunge lijulishwe hiyo *reallocation* ilikuwa ni kwa ajili ya mradi upi na Bunge liridhike na matumizi hayo. Mfano *reallocation* ambayo imefanywa ya kuchukua shilingi bilioni tano kutoka Bajeti ya Ofisi ya Spika, ni muhimu Bunge kufahamu *reallocation* hiyo ni kwa ajili ya nini na zinarudi vipi fedha hizo katika Ofisi ya Spika. Kitendo hicho ni nini madhara yake katika uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Spika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (Sheria Namba 1 ya 2001), kifungu cha 7(3)(a) kinaeleza kwamba, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali anatakiwa kuhakikisha kwamba, kunakuwa na utaratibu mahususi ili kuhakikisha kuwa kila pesa inayotolewa na Serikali inatumiwa kikamilifu kama ilivyokusudiwa, pasipo upungufu wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Mwaka wa Fedha 2003/2004, *Vote 22,* Kifungu cha 41 *(Excess Votes)* inaonesha Sh.31,439,752,838.00. Taarifa iliyoletwa na Serikali inaonesha matumizi ya ziada ni Sh.23,579,131,613.00. Kwa kuangalia taarifa zote mbili, kuna tofauti ya Sh.7,860,621,225.00. Hii inadhihirisha kuwa tayari Serikali imevunja sheria kwa kutokidhi matakwa yanayoendesha shughuli za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kambi ya Upinzani inataka kuelezwa hii tofauti ya shilingi bilioni 7.8 imekwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Kambi ya Upinzani tumekuwa tukipiga kelele kuwa bajeti ya jumla jumla inayofanywa na Serikali bila ya kutoa uchambuzi wa kina kwa kila kitu kinachoombewa fedha, kama ni mishahara kila mtumishi anatakiwa maslahi yake yawemo katika maombi ya awali. Hili litaondoa usumbufu kwa Serikali kwa kila mara kuliomba Bunge liidhinishe mishahara na matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuhakikisha kwamba, bajeti zitakazokuwa zikitayarishwa ziwe wazi *(more detailed)*.

Kifungu cha 18(1)(b) kinaeleza kwamba, katika kila mwaka wa fedha, Serikali inatakiwa kueleza mambo inayotarajia kuyafanikisha na vigezo itakavyotumia ili kufanikisha malengo husika *(outputs expected and performance criteria to be met in providing those outputs).*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana nzima ya kipengele husika ni kuitaka Serikali ibainishe mbele ya Bunge, mafanikio itakayokuwa imeyapata kwa fedha ilizoidhinishiwa na kwa vigezo ambavyo ilijiwekea ili kulipa fursa Bunge, kuhoji upungufu utakaokuwa umejitokeza hivyo, kutekeleza jukumu lake la kuisimamia Serikali kama ilivyoelekezwa na Katiba ya Jamuhuri ya Muungano. Imekuwa ni kawaida kwa Serikali kuleta makadirio ya mapato na matumizi kwa mujibu wa kipengele cha 18 (1)(a). Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali kutekeleza wajibu wake kama sheria inavyoitaka ili kuliwezesha Bunge kuhoji kwa mapana na kuwawezesha Watanzania kufahamu kwa mapana jinsi pesa zao zinavyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nataka kuchangia mambo machache sana. La kwanza, nataka kujua haya matumizi ya ziada ambayo leo tunayapitisha, kwa nini yametumia muda mrefu sana? Naomba Serikali kwa mara nyingine ijitahidi angalau tuwe *current* na haya mambo, kwa kweli miaka minne ni mingi sana kama walivyosema wenzangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili nataka kujua na ninadhani Waziri ataweza kutuambia *opinion* ya *auditor* inasema nini kuhusu matumizi haya *specifically* tunayoyaongelea leo, maana haya ni matumizi ya ziada, ni matumaini yangu, *auditor* atakuwa amefanya *auditing* kujua matumizi haya; *comment* yake ni nini? Kwa hiyo, naomba Waziri wakati anaelezea, atuambie *opinion* ya *auditor* kuhusu matumizi haya ambayo leo tunataka kuyapitisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni matumizi ya ziada na ili tuweze kufanya vizuri ni lazima tuishi ndani ya bajeti, pamoja na kwamba sheria inaturuhusu kwamba tukishatumia ziada tutakuja kuomba Bunge lipitishe. Nadhani tutengeneze tabia ya kubadilisha ili watu wawe wanajua kwamba waishi ndani ya bajeti, *unless it is so necessary* kwamba, sasa kama kuna *crisis* hapa tunakuwa hatuna *choice*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa najaribu kuangalia hapa unakuta nyingine ni mambo ya mishahara, matarajio yangu ni kuwa mambo ya mishahara lazima yamekuwa *budgeted,* lakini kwa sababu kuna *role* kwamba tunaweza tukatumia ziada ndio maana ni rahisi mtu anaweza akaamua akijua kwamba, anaweza aka-*account for.*

Katika matumizi mazuri ya fedha ni kuishi ndani ya bajeti na kwa kweli hapa ni rahisi hata kupanga maendeleo yetu. Lakini kama kila siku tutakuwa tunakuja, kwa sababu nitatumia ziada sheria inaniruhusu tutakwenda Bunge litapitisha, nadhani siyo

*culture* nzuri sana. Naomba wenzetu Serikalini wajitahidi, waanze kuipunguza tabia hii kadri siku zinavyokwenda ili tuanze kuishi ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na mimi pia naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wangu upo hasa katika sehemu zile ambazo matumizi ya ziada yalipelekwa. Nachukulia mfano wa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO),* nadhani si tu suala la kupokea matumizi ya ziada, bali ni pamoja na kuona kwamba hayo matumizi ya ziada yanajilipa vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba, kuna hali ambayo mimi naiona *TANESCO* bado haijabadilika kiutendaji hasa kulingana na kasi mpya zinazoendelea sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara ya mwisho ukiacha hii bajeti ambayo tunaipitisha ya 2004, bado wameweza tena kuomba hela kufuatia ukame uliojitokeza. Lakini kulikuwa na mipango mingi ambayo ilikuwa imewekwa katika bajeti hii ili iweze kutekelezwa na kuweza kuzalisha pesa zaidi, lakini unakuta mipango inasuasua, mpaka leo kuna baadhi ya mipango haijakamilika kabisa.

Natolea mfano wa hela ambazo zilitengwa zikapelekwa Sh.500,000,000 kwa ajili ya Wilaya ya Mbinga, ambayo ni wazalishaji wakubwa wa kahawa na wanachangia kwenye Pato la Taifa. Lakini cha kusikitisha ni kwamba, hata tulivyoenda kule mara ya mwisho hali bado ni ile ile, wananchi wanasikitika wanasema tunavunjwa moyo, sasa utaratibu huu na utamaduni huu wa wafanyakazi wa *TANESCO* nikianzia ninaona kama hatutajirekebisha, hali yetu ya kiuchumi itazidi kushuka na si tu katika Wilaya ya Mbinga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya, tuna-*discuss excess report* iliyopo mbele yetu, Mkoa wa Ruvuma wala Mbinga mbona sijaona? Endelea.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Niliizungumzia kwa sababu imetajwa katika sehemu ambazo zimeongezewa pesa za hayo matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo nilikuwa naomba ili kuhakikisha kwamba hizi pesa tunazoziidhinisha zinaweza kurudi tena, basi na utendaji wetu ubadilike.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuru waliochangia hoja hii, aliyekuja kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mwakilishi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Peter J. Serukamba na Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya. Wote nawashukuru kwa michango yao waliyoitoa na vilevile nisimsahau Mheshimiwa Said Amour Arfi, ambaye ametoa maoni yake kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana na ushauri wote uliotolewa na Kamati ya Fedha na Uchumi na tunakubali kwamba, siku nyingine *excess vote* iletwe mapema. Lakini wengi wenu kama mnavyojua, Waheshimiwa Wabunge hii ni mara ya kwanza ambayo tunapata *in time Report* ya *Controller and Auditor General*. Leo hii tunawasilisha Mezani *Report* ya *Controller and Auditor General* kwa mwaka unamalizikia 2005/2006, haijapata kutokea! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na *postmortem* ya muda mrefu, kwa hiyo, kwa upande wa pili na hii mlikuwa mnaisema siku nyingi Waheshimiwa Wabunge, lakini Serikali imesikia na imefikia hadi sasa hivi *Report* hii itakuwa *in time* na baada ya kujadiliana na *PAC* wakaiangalia wakatazama lipi la kurekebisha, lipi turejeshe, bila shaka huko tunakokwenda *report* ya *excess votes* itakuwa *timely* kama mlivyotushauri Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wa upande wa Upinzani kwanza ni-*draw attention* ya Mheshimiwa Halima J. Mdee kwamba, hii si *reallocation* ya kasma ya ofisi, tunapozungumza *reallocation,* kasma ya Ofisi ya Spika hii siyo. Hii ni *question* ya *excess votes* na tumeeleza zimetumika namna gani. Hatuwezi leo mfano mfadhili amekuja na fedha ametupa vitu mbalimbali kama nilivyovitaja halafu tuache tu tusivitaje kwamba fedha hizi jamani tumepata msaada na katika kupata msaada ilibidi lazima tuzitumie na tulizitumia mwaka fulani. Kwa hiyo, lazima tuziweke katika *excess votes* na lazima kama sheria inavyoturuhusu, turudi hapa Bungeni Waheshimiwa Wabunge tuwaombe ridhaa yenu kwamba, tunaziweka katika *excess votes* ya mwaka 2003 mpaka 2004.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimemjibu Mheshimiwa Peter J. Serukamba kwamba, tunaishi ndani ya bajeti lakini kama nilivyosema wahisani mara nyingi na nyie mnalalamika hapa Waheshimiwa Wabunge kwamba, fedha za maendeleo wakati mwingine zitakawia, kwa mwaka huu 2006/2007, kuanzia Julai ni Desemba na Januari ndio zimeanza kuingia fedha za maendeleo na pengine nyingine zitaingia mwezi huu. Mpaka tunafunga hesabu hawajatuletea katika programu au katika miradi wanayoiendesha, wamepeleka kiasi gani na ndio maana kama sheria inavyoturuhusu, tunakuja hapa si kwamba tumedharau Bunge, hapana.

Kama nilivyosema tangu hapo mwanzo, lazima kwanza *Controller and Auditor General* na *PAC* wayapitie, watoe maoni yao, waturuhusu haya jamani pelekeni Bungeni, ndio tufanye hivyo, ndio sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi mnaelewa mwaka 2006 hali tuliyokuwa nayo, nadhani Waheshimiwa Wabunge tusisema kwamba, *TANESCO* tusiipe hela, tusipoipa *TANESCO* pesa sisi tutapata wapi fedha *revenue*? Viwanda vinategemea umeme, uzalishaji mkubwa wa nchi hii unategemea umeme, sasa tuseme haya ufe na sisi ndio tutakufa, hata hapa tusingeweza kuja. Kwa hiyo, tulilazimika lazima tufanye hivyo na hilo ni jambo la lazima, maadamu ng'ombe yule anayetupatia maziwa kwa vyovyote vile lazima tumlee, tumpe chochote tuhakikishe maziwa yetu yanapatikana ili shughuli zetu za kila siku ziendelee tupate chakula cha asubuhi, cha mchana na cha usiku au siyo? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumaini Waheshimiwa Wabunge tumeelewana, samahani Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto sikukutambua, nakutambua kwamba ulitoa mchango wako pia nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2007 *(The Supplementary Appropriation Bill, 2007)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilishtuka sana Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa hakutambua mchango wangu wa maandishi, kwa sababu maana yake ni kwamba, nisingepata nafasi ya kushika vifungu lakini namshukuru Katibu kwa kumkumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nimemkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kuleta Muswada wa *Appropriation,* Serikali haikufuata sheria, hapa nina nakala ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, ambapo ibara ya 19 inazungumzia taratibu za *excess expenditure*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 19(2), naomba niisome: *Where the National Assembly shall by means of a motion, allows any excess or any amount expended but not appropriated to stand charged to public funds, the sum required to meet such excess or such amount as shall be allowed, shall be included in a Supplimentary Appropriation Bill*

*for appropriation.* Serikali ilichopaswa kufanya ni kuleta *statement of excess* kwenye Bunge, ikaletwa hoja ndani ya Bunge na Bunge likakubali *statement of excess,* Serikali ikarudi ikaandika sheria ndiyo ikaleta sheria ambayo tunaijadili hapa.

Sasa wanachokifanya Serikali ni kuleta sheria kabla Bunge halijapitisha hoja ya matumizi ya ziada, huu ni uvunjaji wa sheria na ni aibu kwa Serikali kuvunja sheria kwa kutofuata taratibu zinazopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niurudie, kwa sababu hatuwezi kusema kwamba, sasa tuanze kujadili na mara nyingi mkosaji wa kwanza husamehewa.

Lakini tunaomba Serikali iliombe radhi Bunge rasmi, kwa kukiuka utaratibu ambao umewekwa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, ambayo inahitaji walete kwanza kauli ya ziada na ndio baadaye walete sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupate maelezo kutoka Serikalini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mstaafu, karibu.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa mchango wa Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini unaposema *by motion, motion* ni hoja, inatolewa hoja ya kuwalisha *Statement* ya *Excess*. Ukisema kwamba Serikali haikufuata hata utaratibu wa *motion,* kidogo naanza kushangaa kwani wewe ni Mwanasheria na ni vizuri tunapoyatumia maneno haya '*motion'* nadhani nimempa *title* ambayo si yake, niwie radhi.

Lakini *motion* maana yake ni kwamba una hoja rasmi mbele ya Bunge na maana ya hoja ni kwamba naomba kutoa hoja kwamba niwasilishe *Statement* ya *Excess* kwa mwaka 2003/2004, hoja hiyo inaungwa mkono na tayari imeiva. Ndiyo maana yake. Unakuja kwa hatua ya pili kwa sababu tunaomba sasa zile pesa ziingizwe kwa utaratibu wa *appropriation,* ndiyo Muswada unawasilishwa kama ilivyofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ulipoanza kusema kwamba asubuhi *Order Paper* ilikuwa na mtiririko huo na kilichofanyika ni sahihi kabisa, wala hakuna sheria ambayo imekiukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, hata hati ambazo mmeweza kuwasilisha au taarifa za Wabunge mnaweza kuwasilisha hapo mezani lakini mtu akasimama na kusema naomba taarifa hii ijadiliwe, ama unaweza kuwasilisha ukaweka. Sasa Serikali iliwasilisha halafu ikaleta na hoja yake, *this is the motion* tunayojadili sasa hivi. Kwa hiyo, nadhani tusingeota.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima bila Marekebisho yoyote)*

Kifungu cha 2
Kifungu cha 3
Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

(*Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote*)

Jedwali

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Said Amour Arfi.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama nilivyotoa katika mchango wangu wa maandishi, nilikuwa nimehoji matumizi ya ziada kwa *Vote* ya 88 ya Mkoa wa Dar es Salaam, nimeeleza katika mchango wangu umuhimu wa sherehe za Uhuru, ni sherehe muhimu sana na tunapaswa tuwe tumetenga fedha za kutosha kukidhi Sherehe zetu hususan za kitaifa.

Lakini katika fedha hizi ambazo zinaombwa hapa katika *Statement* ya *Excess* inaonesha *employment allowance* ya Sh. 5,450,000/= nilikuwa nataka nipate maelezo ya mahusiano ya *Employment Allowance* na Sherehe za Uhuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante, ulipewa na maandiko pia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa naelezea kwamba kitu chochote ambacho kimetumika hata kama ni kidogo *5 million* kwa sherehe zote za uhuru, makisio ni makisio na kwa wale wote ambao wanatengeneza makisio mbalimbali hata ya shughuli yako mwenyewe.

Wakati wingine kile unachokisia kwamba utatumia inakuwa unatumia zaidi na kama umetumia zaidi ya kile ulichokisia na kwa utaratibu wa Serikali ni lazima tulete hapa tuseme kwamba, jamani tulikisia hiki, lakini hakikutosha kwa sherehe za uhuru. Kweli tulitumia fedha na kweli tulifanya bajeti lakini haikutosha.

Kuhusu *allowance* ya mishahara ni kwamba wafanyakazi kwa utaratibu mbalimbali wamepandishwa vyeo na wengine wamepewa kazi kwa mfano kwenye *Refugees Camps* wafadhili walipoleta magari ambayo hatukuwa na *drivers* lazima kuwe na *allowance* ya kuweza kuwalipa hawa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuchukua *statement*, hii *Vote* ya Dar es Salaam 88 ukisoma pale maelezo kuna *Employment Allowance five million, hospitality, five million* tena *employment,* nyingine sasa hii wanasema matumizi yaliyosababisha gharama zaidi za maadhimisho ya Sherehe ya Uhuru. Mbunge anauliza *Employment* na Sherehe za Uhuru ziliingiliaje? Ndiyo swali. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naeleza hivi, *Employment Allowances* kuna watu bila shaka wameajiriwa katika maandalizi ya Sherehe hizi kwa kufanya shughuli hizi. Kwa hiyo, hizo fedha zilipelekwa kwa ajili hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitalizungumzia hili jedwali kwa ujumla wake kwa sababu katika maelezo yangu niliyokuwa nikiyatoa wakati nikiwasilisha hoja za Kambi ya Upinzani, nilionyesha kwamba kuna *difference* ya bilioni saba baina ya ripoti iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Taarifa hii hapa ambayo Serikali imetupatia.

Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake hajazungumzia chochote ambacho kinahusiana na hilo, sasa naomba atupe ufafanuzi hii tofauti imekwenda wapi na imefanyiwa shughuli gani?

**MWENYEKITI:** Nawe pia utatakiwa ueleze vizuri kwani sisi hatujaiona iko wapi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka huu ambayo tumeletewa ambayo ina taarifa zote, yaani ripoti ya 2003/2004 *Vote* 22, ni 2003/2004. Kwa sababu hapa tunazungumzia *excess vote* ile ya huu mwaka, kwa hiyo sasa kuna tofauti kati ya Taarifa ya Serikali kuhusiana na haya matumizi husika na Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali tofauti ni *seven billion*.

Sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze hiyo tofauti ya Shilingi bilioni saba imekwenda wapi? Au kama hawajaisoma ile taarifa watutaarifu lakini tofauti ndiyo hiyo *seven billion*.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, naagiza kwamba ikaangaliwe halafu maelezo yatatolewa. *(Makofi)*

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

***Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2007***
***(The Supplementary Appropriation Bill, 2007)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae tafadhali. Mtoa hoja taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya kuidhinisha matumizi ya ziada ya Sh. 23,579,131,613/= kutoka

Mfuko Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2003/2004 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona shughuli tulizokuwa nazo katika *Order Paper* ya leo tumezimaliza.

Sasa ningependa kufafanua jambo moja. Wakati Mheshimiwa Zitto anaomba nafasi ya kupata ufafanuzi kwenye Kamati ya Matumizi alikuwa amesema anashukuru aliandika asingeandika asingekuwa na nguvu hii, si kweli!

Katika Kamati ya Matumizi unaweza ukasimama ukahoji kifungu chochote hata kama hukujadili ama hukusema kitu maana pengine usingepata nafasi, una ruhusa kabisa kuhoji. Kwa hiyo, siyo lazima uongee wala siyo lazima uandike, ukifika kifungu unachotakiwa kama una swali la kupata ufafanuzi ama kuhoji unaweza kufanya hivyo bila kuhitaji kuandika. *(Makofi)*

Lakini la pili, sisi tunapenda kama mtu anapenda kutushauri kwa vikaratasi aandike majina yake, maana kuna mmoja hapa ameniandikia ujumbe, lakini anasema ahsante. Wewe nani? Sasa ni vizuri tukaandika kwani ukiandika jina la Mheshimiwa mnaweza mkajadiliana kwa kirefu hata baadaye, lakini ikiwa hivi hivi tu, sitaki hata kuisoma hii kwa sababu naona kama ni majungu. Kwa hiyo, mnapotushauri andikeni majina yenu, si tunashauriana?

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za kikao hiki mpaka kesho saa 03:00 asubuhi.

*(Saa 01.16 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 13 Aprili, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*